

**TATHMINI YA MAKOSA YA KISARUFI YA WANAFUNZI WA KINGWANA
WANAOFUNZA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI KIFANI WA VYUO
VIKUU VYA BURUNDI**

DIEUDONNE BUTOYI

**TASNIFU HII ILIWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUKAMILISHA
BAADHI YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA
KISWAHILI-ISIMU YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2022

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Aliyeweka saina hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii itwayo:

Tathmini ya Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana Wanaojifunza

Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Kifani wa Vyuho Vikuu vya Burundi na ameridhika

kwamba tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa

utahini wa shahada ya uzamili (M.A. Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

Tarehe.....

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Dieudonné Butoyi**, nathibitisha kwamba tasnifu hii yenye mada ya **Tathmini ya Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Kifani wa Vyuho Vikuu Burundi** ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa na wala haitahudhurishwa kwenye chuo kingine kwa lengo la kutunukiwa shahada kama hii.

Saini.....

Tarehe.....

HATI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile sehemu yoyote ya tasnifu hii, kwa njia yoyote ile kama vile kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine, bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mke wangu mpendwa Floride Nkurunziza. Mchango wake katika utekelezaji wa kazi hii umezidi kiwango cha kawaida. Uwu uboná yangíze “Ndahîrâje”.

SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kupambana na masomo ya uzamili hadi kuimaliza kazi hii. Apewe sifa milele na milele.

Pili, namshukuru sana msimamizi wangu, Dkt. Zelda Elisifa, kwa uvumilivu, busara na namna alivyonipa moyo ili nipate kuifanya na kuikamilisha. Ushauri na maelekezo yake yamefanikisha utekelezaji wa kazi hii. Ninamshukuru pia kwa upendo na mapokezi yake alipotupokea kituoni Kigoma siku ya kwanza kabisa ya safari hii ya uzamili. Ingawa tulikuwa katika wasiwasi wa kukamilisha matakwa ya chuo, tuliridhika na upendo wake.

Tatu, niwashukuru sana walimu wote wa Idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania waliotuelekeza katika masomo mbalimbali; Baadhi yao ni Dkt. Nasra Habibu, Mwl. Bakari Kombo na mratibu wetu Dkt. Mohamed Omary.

Nne, shukurani za dhati zimfikie Mama mlezi wa wadau wa Kiswahili nchini Burundi, Mwl. Dorothée Nshimimana. Mchango wake mzuri katika kueneza lugha ya Kiswahili nchini Burundi ulinifanya nielewe kuwa lugha yoyote huwa nyenzo ya kueleza na kueneza sayansi.

Tano, shukurani ziwafikie Wizara ya Elimu na Utafiti kwa ufadhili wao ulioleta ufanisi wa kazi hii.

Vilevile shukurani za pekee kwa mke wangu Floride Nkurunziza, watoto wangu Jean Fleuri Bukuru, Adriel Ndanga na Ael Ntore kwa uvumilivu wao wakati wa utafiti huu.

Namalizia shukurani zangu kwa watafitiwa walioshiriki katika kutoa taarifa za utafiti na wote walioshiriki katika kufanikisha kazi hii kwa namna moja au nyingine, shukurani zangu za dhati ziwafikie na kazi hii iwe tuzo kwao.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kutathmini makosa ya kisarufi ya wanafunzi wanaoongea Kingwana kama L1 wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni. Malengo mahususi yaliyoongoza utafiti huu yalikuwa kubaini aina za makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu, kutathmini viwango vya ujitokezaji wa aina mbalimbali vya makosa hayo na kuchunguza sababu za makosa ya kisarufi katika Kiswahili Sanifu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi makosa (UM) iliyoasisiswa na Stephen Pit Corder (1967). Utafiti huu ulifanyika kwenye vyo vikiu vitano na wanafunzi mia moja walishiriki. Mbinu za kukusanyia data zilikuwa mapitio ya nyaraka, ushuhudiaji na hojaji. Uchanganuzi wa data ulidhihirisha makosa ya kifonolojia yaliyojitokeza kwa kiasi cha 41.76%, makosa ya kimofolojia kwa kiasi cha 24.48% na makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia kwa kiasi cha 33.75%. Uhamishaji wa mifumo ya Kingwana kwenda Kiswahili sanifu, kutojua kanuni za sarufi ya Kiswahili sanifu, ufupishaji wa vipashio na matumizi ya kanuni fulani kupita kiasi ndivyo vilivyodhihirika kuwa sababu za makosa hayo. Uhamishaji ulisababisha makosa yanayolingana na 55.60% ambapo kutojua kanuni kulisababisha makosa 31.92%. Matumizi ya kanuni fulani kupita kiasi yalisababisha makosa 8.12% ilihali ufupishaji ulisababisha makosa 4.34% kwa jumla ya makosa yote 874. Kutokana na matokeo hayo, utafiti huu umependekeza kuwa walimu wa Kiswahili nchini Burundi waimarishe ufundishaji wa Kiswahili na wanafunzi wafanye juhudi kujifunza Kiswahili. Pia utafiti unaiomba serikali ya Burundi kuweka na kuboresha sera ambayo ingeyapa kipau mbele mafunzo ya lugha ya Kiswahili. Mwishoni, kumependekezwa tafiti zingine kama vile uchunguzi wa makosa ya kisemantiki na uchunguzi wa launi za lahaja ya Kingwana.

YALIYOMO

TAMKO LA MTAHINIWA.....	ii
HATI MILIKI.....	iii
TABARUKU	iv
SHUKURANI.....	v
IKISIRI..	vii
YALIYOMO.....	viii
MAJEDWALI.....	xiii
MICHORO.....	xiv
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xv
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.1.1 Lugha ya Kiswahili	1
1.1.2 Lahaja ya Kingwana.....	2
1.1.3 Uamiliaji na Ujifunzaji Lugha	3
1.1.4 Dhana ya Makosa Katika Ujifunzaji Lugha.....	5
1.2 Tatizo la Utafiti	9
1.3 Malengo ya Utafiti	10
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti	10
1.3.2 Malengo Mahususi.....	10
1.4 Maswali ya Utafiti.....	11
1.5 Umuhimu wa Utafiti	11
1.6 Upeo wa utafiti.....	12

1.7	Muhtasari	12
-----	-----------------	----

SURA YA PILI : MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA

	NADHARIA.....	14
2.1	Utangulizi.....	14
2.2	Mapitio ya Kazi Tangulizi	14
2.2.1	Dhana ya Ujifunzaji wa Lugha ya Pili	14
2.2.2	Makosa katika Lugha	18
2.2.3	Uhusiano wa L1 na L2 katika Muktadha wa Ujifunzaji	24
2.3	Pengo la utafiti	28
2.4	Mkabala wa Kinadharia	29
2.4.1	Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa	29
2.4.2	Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Makosa	30
2.5	Hitimisho.....	32

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

3.1	Utangulizi.....	33
3.2	Eneo la Utafiti na Watafitiwa.....	33
3.3	Sampuli Lengwa ya Watafitiwa na Usampulishaji	34
3.3.1	Sampuli Lengwa	34
3.3.2	Usampulishaji	34
3.4	Mbinu za Utafiti.....	36
3.4.1	Mbinu za Kukusanyia Data.....	37
3.4.1.1	Hojaji.....	37
3.4.1.2	Ushuhudiaji	38

3.4.1.3	Mapitio ya Nyaraka.....	38
3.4.2	Mkabala wa Uchanganuzi wa Data.....	39
3.5	Maadili ya Utafiti	40
3.6	Hitimisho.....	40
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHUNGUZI WA DATA.....		42
4.1	Utangulizi.....	42
4.2	Uwasilishaji wa Data	42
4.3	Aina za Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Lahaja ya Kingwana na Viwango vya Ujitokezaji Wake	43
4.3.1	Makosa ya Kifonolojia.....	46
4.3.1.1	Udondoshaji wa Fonimu	47
4.3.1.2	Ubadilishanaji wa Fonimu	49
4.3.1.3	Uzalishaji wa Fonimu katika Mazingira Yasiyoruhusika Kiisimu	51
4.3.2	Makosa ya Kimofolojia.....	55
4.3.2.1	Udondoshaji wa Viambishi Vinavyohitajika	56
4.3.2.2	Ongezeko la Viambishi Kimakosa.....	58
4.3.2.3	Matumizi ya Viambishi Kimakosa	60
4.3.3	Makosa ya Kisintaksia na Kimofosintaksia	65
4.3.3.1	Upatanisho wa Kisarufi Usiokubalika	66
4.3.3.2	Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno.....	70
4.3.3.3	Kukata na Kuunganisha Maneno Visivyo	72
4.4	Vyanzo vya Makosa ya Kisarufi katika Kiswahili Sanifu	76
4.4.1	Makosa kutokana na Uhamishaji wa Lugha	80

4.4.1.1	Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Uhamishaji.....	80
4.4.1.2	Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Uhamishaji.....	83
4.4.1.3	Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Uhamishaji	88
4.4.2	Makosa Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha Lengwa	92
4.4.2.1	Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha	93
4.4.2.2	Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha.....	94
4.4.2.3	Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha.....	96
4.4.3	Makosa Kutokana na Ufupishaji.....	99
4.4.3.1	Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Ufupishaji.....	100
4.4.3.2	Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Ufupishaji	101
4.4.3.3	Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Ufupishaji.....	102
4.4.4	Makosa Kutokana na Sababu ya Matumizi ya Kanuni Kupita Kiasi.....	103
4.4.4.1	Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Matumizi Kupita Kiasi ya Kanuni.....	103
4.4.4.2	Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Matumizi Kupita Kiasi ya Kanuni.....	104
4.5	Uhusiano baina ya Matokeo na Kiunzi cha Nadharia.....	106
4.6	Hitimisho.....	106
SURA YA TANO: MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO		108
5.1	Utangulizi.....	108
5.2	Muhtasari	108
5.2.1	Muhtasari kwa Ujumla.....	108
5.2.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	109

5.3	Hitimisho.....	111
5.4	Mapendekezo ya Utafiti.....	111
	MAREJELEO	113
	VIAMBATANISHO	123

MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1:	Mchanganuo wa Watafitiwa	36
Jedwali Na. 4.1:	Ujitokezaji wa Makosa ya Kifonolojia	46
Jedwali Na. 4.2:	Udondoshaji wa Herufi	48
Jedwali Na. 4.3:	Ubadilishanaji wa Fonimu	50
Jedwali Na. 4.4:	Uzalishaji wa Fonimu Usio Sahihi.....	52
Jedwali Na. 4.5:	Ujitokezaji wa Makosa ya Kimofolojia	55
Jedwali Na. 4.6:	Udondoshaji wa Viambishi Vinavyohitajika	57
Jedwali Na. 4.7:	Ongezeko la Viambishi Kimakosa.....	59
Jedwali Na. 4.8:	Matumizi ya Viambishi Kimakosa	61
Jedwali Na. 4.9:	Ujitokezaji wa Makosa ya Kisintaksia na Kimofosintaksia	65
Jedwali Na. 4.10:	Upatanisho kati ya Nomino na Kitenzi	67
Jedwali Na. 4.11:	Upatanisho kati ya Nomino/Kiwakilishi na Kivumishi	69
Jedwali Na. 4.12:	Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno.....	71
Jedwali Na. 4.13:	Kukata na Kuunganisha Maneno Visivyo	73
Jedwali Na. 4.14:	Kiasi cha Makosa Kulingana na Vyanzo Vyake.....	78

MICHORO

Mchoro Na. 4.1: Aina za Makosa ya Kisarufi na Viwango vya Ujitokezaji wake . 44

Mchoro Na. 4.2: Sababu za Utokeaji wa Makosa 79

ORODHA YA VIFUPISHO

KAKAMA	:	Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki
L1	:	Lungha ya kwanza
L2	:	Lungha ya pili
ML	:	Mwingiliano wa Lugha (Nadharia ya Mwingiliano wa Lugha)
UL	:	Uchanganuzi Linganishi (Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi)
UM	:	Uchanganuzi Makosa (Nadharia ya Uchanganuzi Makosa)

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Sehemu hii ya usuli wa mada, pamejadiliwa mambo ya msingi katika kupata uelewa wa awali kuhusu tofauti iliyopo baina ya Kiswahili sanifu ambacho huchukuliwa kama lahaja rasmi na lahaja ya Kingwana. Hivyo, sehemu hii inahusika nalugha ya Kiswahili, lahaja ya Kingwana, uamiliaji na ujifunzaji lugha nadhana ya makosa katika kujifunza lugha.

1.1.1 Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu (G.42) ambayo huzungumzwa katika masharki, kati na kusini mwa Afrika. Kwa mujibu wa Massamba (2016: 54), “Kiswahili ni lugha inayotumiwa na wananchi wengi wa Afrika Masharki na Kati. Asili yake ni pwani ya Afrika Mashariki. Kutokana na safari za kibiashara, wahubiri na waeneza dini, lugha hii ikaweza kusambaa hadi bara.” Fasili hii inadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili iliwavutia wana jamii wa jamii tofauti na wenye majukumu mbalimbali, hivyo ikaenea kwenye sehemu nyingi. Kwa mujibu wa KAKAMA (2019:15), “Lugha ya Kiswahili imeenea na sasa inatumiwa sana na raia wengi wa asili ya Afrika Mashariki. Mbali na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kabisa, ilipitishwa mnamo Agosti 2019 kama mojawapo ya lugha nne rasmi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).” Hii ina maana kuwa, hata kama si kwa kiasi sawa, Kiswahili ni lugha rasmi kwa maeneo maalum kimawasiliano, hususani katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Pia, KAKAMA (2019:15-16) wanafafanua,

Licha ya EAC na SADC, Kiswahili pia ni mojawapo ya lugha za kikazi za Umoja wa Afrika (AU). Akademia ya Lugha ya Afrika (ACALAN) na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA), wameamua na kujitoa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Kiswahili kinatambulika na kukuzwa kama lugha yenye kuwezesha mawasiliano mapana katika Muungano wa Waafrika.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili huifanya kuwa lugha yenye hadhi kubwa, hivi kwamba huzungumzwa si tu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, bali hutambulika Afrika na duniani kote kwa ujumla.

1.1.2 Lahaja ya Kingwana

Kwa mujibu wa Ngugi na Chacha (2004:37), “Lahaja ni aina ya uzungumzaji unaotumiwa na kikundi cha watu aghalabu katika eneo maalumu, na hutofautiana na uzungumzaji na vikundi vingine vya lugha hiyo moja katika matamshi, msamiati na kwa nadra sarufi.”

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha ambazo zimeenea sana na kuzungumzwa na raia wengi barani Afrika na kwingineko, na hii ikiwa mojawapo ya sababu za kuzuka kwa lahaja zake, ikiwemo lahaja ya Kingwana. Kipacha (2002: 40), akizungumzia lahaja za Kiswahili na watafiti waliozishughulikia, anazitaja lahaja ambazo zimejitokeza kwa kila mmoja wao: “Chimwini, Kitukuu, Kipate, Kisiu, Kiamu, Kimvita, Chifundi, Kivumba, Kimtang’ata, Kipemba, Kitumbatu, Kiunguja na Kimakunduchi. Jumla ya idadi hizo ni 13.” Lahaja ya Kingwana haikuorodheshwa hapa. Hata hivyo, Kipacha (ameshatajwa) anakazia kuwa “Lahaja ya Kingwana iliyopo nchini Zaire (DR-Congo) imetajwa na wataalamu watatu tu, ambao ni Heine, Chiraghdin na Nurse.” Nshimirimana na wenzake (2019: 2)

wanaongeza kuwa “lahaja ya Kingwana hutumiwa na raia wa sehemu za mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, nchini Burundi na Rwanda.” Naye Kang’ethe (2002: 34) anasema kuwa, “lahaja za Kingwana na Shingazija (lahaja ya Komoro) huwa ni lahaja za Kiswahili ambazo hutofautiana kabisa kiisimu na Kiswahili sanifu ambayo nayo hutokana na lahaja ya Kiunguja ambayo huzungumzwa Zanzibar.”

Akizungumzia asili ya Kingwana, Polome (1967: 27) anasema kuwa, “jamii za Waswahili kimsingi zinajumuisha wasaidizi au watumwa wa Kiafrika wa wafanya biashara wa Kiarabu ambao wenyewe walijiita Wangwana, yaani watu wenye uhuru; na lahaja yao ikajulikana kwa jina la Kingwana.” Naye Casco (2007: 4), alipoibaini miongoni mwa lahaja zingine za Kiswahili, alisema kuwa “miongoni mwa lahaja za bara, Kingwana ndiyo lahaja inayotofautiana sana na Kiswahili sanifu.” Hivyo, ni dhahiri kuwa lahaja ya Kingwana hutambulika miongoni mwa lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili ambazo huzungumzwa na baadhi ya wana jamii wa bara hususan katika nchi za Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Burundi na Rwanda.

1.1.3 Uamiliaji na Ujifunzaji Lugha

Lugha ni chombo muhimu kinachoweza mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Hivyo, mwanajamii mara anapozaliwa na kuanza kuishi katika jamii ndipo michakato ya matumizi ya lugha huanza kukua ndani yake bila yeye kutarajia. Hii ina maana kuwa wakati anapojaribu kuyaelewa mambo yanayomzunguka, ndipo lugha ya jamii yake huibuka. Hapa, ndipo dhana ya uamiliaji lugha inapoeleweka kwa mwanadamu yeyote. Wanapofasiri uamiliaji, Krashen na Terrell (1983)

wanasema kuwauamiliaji ni mchakato unaotokea katika nafsi iliyofichika akilini mwa mtu ambayo ndiyo imuongozayo kuongea au kuandika kwa urahisi. Hivyo, uamiliaji hujitokeza kwa mtu pasipo mwenyewe kujua au kujitambua. Pia, ingawa uamiliaji wa lugha unamhitaji mtoto, mwanafunzi au mjifunzaji yeyote kuwa katika mazingira ya lugha husika (Mutombe, 2015: 21), hauzingatii sheria au kanuni za lugha husika, kwani mhusika mwenyewe, kwa mfano mtoto aamilipo lugha ya jamii yake, yaani lugha mama, huibua matumizi ya lugha hiyo bila utambuzi wa kanuni za msingi za lugha hiyo. Kwa mujibu wa Chomsky (1971), kama anavyonukuliwa na Berwick na wenzake (2011), hili hutokana na hali kwamba akilini mwa mzungumzaji, kuna uwezo aliozaliwa nao, ambao unatokana na uzoefu; uwezo ambao unaweza kuhusishwa katika upatikanaji wa maarifa. Hivyo, kama anavyohakikisha Chomsky mwenyewe (Chomsky, 1975: 61):

Mzungumzaji (muamiliaji) wa lugha ambaye ameshapata seti ndogo ya tungo za lugha yake, anaweza kutoa idadi kubwa ya tungo mpya ambazo zinakubalika mara moja na wanajamii lugha husika, kwa msingi wa uzoefu huu mdogo wa lugha. Anaweza pia kuelewa baadhi ya tungo sahihi kutokana na seti za tungo ambazo alikuwa hajawahi kusikia wala kutunga mwenyewe.

Hivyo, ni dhahiri kuwa uamiliaji hutofautiana na ujifunzaji lugha. Kwa mujibu wa Massamba (2016: 138), “ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani.” Nao Krashen na Tracy (1983) wanadai kuwa ujifunzaji lugha ni mchakato wa kiufahamu wa kiakili au utambuzi wa nafsi unaojionyesha katika kujifunza sheria na kanuni na miundo ya lugha.

Ujifunzaji lugha ni tukio ambapo mjifunzaji anafahamu au kutambua mwenyewe kuwa anajifunza kanuni na miundo ya lugha; na uamzi wake na bidii zake katika

ujifunzaji vitawezesha na kufanikisha ufahamu atakaopata. Aidha, mchakato wa ujifunzaji lugha hutokea pale ambapo mtu anashughulika na lugha ambayo si L1.

Hivyo, ni dhahiri kwamba dhana za ujifunzaji na uamiliaji lugha hutofautiana sana, kwani ujifunzaji lugha huzingatia ujuzi na utambuzi wa vipengele muhimu vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia; ilhali katika uamiliaji wa lugha vipengele hivyo huja vyenyewe pasipo utambuzi wala ujuzi wa mwanajamii husika.

1.1.4 Dhana ya Makosa Katika Ujifunzaji Lugha

Kwa muda mwingi, tafiti kadhaa zilifanyika ili kuelewa mchakato wa uamiliaji wa L1 na ujifunzaji wa L2. Matokeo ya tafiti hizi yalidhihirisha kuwa mchakato wa uamiliaji wa L1 na ujifunzaji wa L2 hutokea kwa namna sawa, kwa maana kwamba waamiliaji wa L1 na wajifunzaji wa L2 huhusika na makosa tofautitofauti.

Kujitokeza kwa makosa aghalabu katika L2 na ufafanuzi wake vilijadiliwa na wataalamu mbalimbali hadi ikaibuka kuwa uwanja muhimu wa utafiti. Baadhi ya waanzilishi na walioshughulikia dhana hii ni Corder (1973, 1978, 1981); Selinker (1972), Richards (1974) na Ferris (2011). Kwa mfano, kwa mujibu wa Ferris (2011:3), “makosa katika lugha ni mifumo ya kimofolojia, kisintaksia na kileksikolojia inayotofautiana kabisa na kanuni za L2, ambayo inakiuka matarajio ya wazungumzaji asili wazima wa lugha hiyo waliosoma.” Naye Corder (1981:10) anaelezea “kosa kama upungufu wa kimfumo uliosababishwa na ukosefu wa umilisi wa lugha kwa mwanafunzi.” Kutokana na fasili hizo, makosa ya mwanafunzi wa L2 hutokana na yeye kutofikia ukamilifu wa umilisi wa lugha hiyo, na udhaifu wake katika utendaji kwa kutumia lugha hiyo. Hivyo, ni muhimu kuelewa kuwa kuna

tofauti kubwa kati ya ughafilishaji au kuteleza kwa bahati mbaya katika lugha na makosa yenyewe ya lugha.

Kwa mantiki hiyo, makosa yanayofanywa na wanafunzi au wajifunzaji wowote wa L2 hugawanyika katika makundi mawili : (1) makosa ya kiumilisi na (2) makosa yanayotokana na utendaji wa mtu, kama yanavyoainishwa na Corder (1974: 259). Kutokana na (1), Corder anaeleza kuwa: “makosa katika lugha hutokana na ujifunzaji usiokamilika na ukosefu wa umilisi wa lugha kwa wajifunzaji; tena mjifunzaji hawezi kujikosoa makosa hayo mwenyewe.” Kwa hiyo, makosa ya kiumilisi hutokana na ujuzi duni wa mwanafunzi au mjifunzaji wa L2. Ili kujirekebisha, mwanafunzi atalazimika kupata mafunzo kuhusu muundo sahihi wa hiyo L2. Kuhusu (2), Corder (ameshatajwa) anaeleza kuwa nimakosa yanayotokana na utendaji duni wa lugha kutokana na sababu nyingi kama vile uchovu, kutojali kwa wanafunzi, n.k. Makosa ya kiutendaji hayahusiani na ujuzi wa mwanafunzi bali yanatokana na kughafilika kwake au kuteleza kwa bahati mbaya, kwani mwanafunzi tayari ana ujuzi kamili wa lugha. Aidha, katika mazingira ya ujifunzaji wa L2, wataalamu wengi kama Nickel (1973), Lee (2001), Hsin (2003)(kama alivyonukuliwa na Chen, 2006) na Zhang (2007) huona kuwa L2 huathiriwa na L1 ambayo mwanafunzi au mjifunzaji alilelewa nayo, hivi kwamba kughafilika na kutokea kwa makosa kwa mwanafunzi au mjifunzaji wa L2 hutokana na L1.

Kutokana na maelezo hapo juu, makosa katika lugha huwakumba watumiaji wa lugha, hususan wanafunzi wanaojifunza L2. Makosa hayo hujitokeza katika viwango vyote vya lugha, yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kwa kuwa wajibu wa lugha ni kuwezesha mawasiliano baina ya watu, kughafilika na kutokea

kwa makosa hayo huweza kupotosha lugha na kuzuia ujumbe au kusababisha ujumbe usiokusudiwa. Maswali yanayoibuka hapa yanahusiana na namna makosa yanavyoweza kushughulikiwa: Walimu wanapaswa kusahihishaje makosa ya wanafunzi ? Wanapaswa kutoa maoni gani ? Je, kila kosa linahitaji kusahihishwa ? Inadhihirika wazi kuwa uchunguzi wa makosa huchangia sana katika kujibu maswali haya.

Katika muktadha huu, kazi kuu ya mwalimu huwa ni kudhihirisha tatizo la mwanafunzi na kuchunguza kama anaweza kujirekebisha mwenyewe; na hivyo akajua kuwa alichokisema au kukiandika ni kosa au kuteleza tu katika lugha. Kama anavyosema Erdogan (2005: 267-268), “mwalimu anatakiwa aelewe kwanza chanzo cha makosa ili aweze kutoa suluhisho faafu, ambalo litamwezesha kumwondoa shida mwanafunzi na kumruhusu kugundua kanuni husika.” Kwa hivyo, chanzo cha kosa ni kidokezo muhimu kwa mwalimu ili kuamua juu ya aina ya suluhisho kwa matatizo ya mwanafunzi. Kwa mujibu wa Harmer (1998), mwalimu anatakiwa kufuata hatua tatu makosa yanapotokea. Kwanza, mwalimu husikiliza wanafunzi, pili, hujaribu kutambua tatizo (kosa), na, tatu, hutafuta namna nzuri ya kulisahihisha. Hii ina maana kuwa, uwezo wa kushughulikia makosa hutokana na mwalimu kuchagua data mwafaka na mbinu nzuri ya kuziwasilisha kwa wanafunzi husika.

Aidha, kutokana na muktadha wa kimatumizi wa lugha, namna za usahihishaji makosa hutokana na hali ya kosa husika, hivi kwamba masuluhisho kwa makosa ya kimaandishi na kimazungumzo hutofautiana (Erdogan, 2005: 268). Kosa likitokea katika mazungumzo, mwalimu hutakiwa kutomkatisha kauli mwanafunzi, bali kuyanukuu makosa ili kumkumbusha na kumwelezea makosa hayo na sababu zake

kutokea. Ikiwa ni kosa la kimatamshi, mwalimu anapaswa kurekebisha kosa hilo bila kumkatiza mzungumzaji (Ur, 1996). Katika kazi za kimaandishi, inambidi mwalimu asisahihishe makosa ya wanafunzi papo hapo, bali baada ya kazi yenyewe kwa kutumia alama kama vile “sp” kuwakilisha kosa la kiorthografia na “rw” kwa kosa la kimuundo ambalo linasababisha tungo kuandikwa upya; na hivyo kutoa sentensi sahihi (Erdogan, 2005: 269). Kwa hivyo, wanafunzi wanaweza kujirekebisha wakitambua chanzo cha makosa yao. Ur (1996), kama alivyonukuliwa na Erdogan (2005: 269), anaongeza kuwa kulitokea mielekeo mingi juu ya usahihishaji makosa hadi mikabala mbalimbali ikaibuka. Baadhi ya mikabala hiyo ni kama vile mkabala wa mwathiriano unaodai kwamba makosa ni sehemu muhimu ya ujifunzaji wa lugha, hali kwamba kuyasahihisha huwa mbinu muhimu ya kumrahisishia mwanafunzi kupata uelewa wa L2 ; mkabala wa mawasiliano ambao unadai kuwa si makosa yote yanayohitaji kusahihishwa kwani, kilicho muhimu huwa ni kueleweka kwa ujumbe uliomo ; nadharia elekezi ambayo inadai kuwa usahihishaji hauchangii ujifunzaji wa lugha, n.k.

Mwisho, katika muktadha wa ufundishaji wa lugha, Corder (1973) anaeleza kwa ufupi mchakato wa usahihishaji makosa akisema kuwa “ ujifunzaji lugha si marudio kama kasuku anavyofanya, kwani hatujifunzi wala kuamili mifano, bali misingi ambayo ni malighafi ya mfumo wa lugha. Uwezo katika usahihishaji makosa hutokana na mbinu za kuishughulikia mfumo duni (isiyo sahihi) ya lugha kwa namna sahihi.”

1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguza makosa ya kisarufi yanayojitokeza kwa wanafunzi wa Kingwana wanaoongea Kiswahili sanifu kama lugha ya pili (L2) wanachofundishwa vyuo vikuu. Kama ilivyo kawaida ya lugha, kutokana na kukua na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili Sanifu katika mazingira ama ya kawaida au rasmi, kimeendelea kuathiriwa na lugha za kijamii au lahaja za Kiswahili zizungumzwazo na jamii mbalimbali.

Tafiti za uwanja huu huegemea ama kwenye mtazamo wa Lado au wa Corder. Kwa mujibu wa Lado, kama anavyonukuliwa na Krashen (1981: 64), “chanzo cha makosa katika matumizi ya L2 kwa watu wazima huwa ni L1.” Naye Corder (1967: 161) kwa upande wake anaeleza kuwa “kuwa mahiri wa L1 humrahisishia mwanafunzi kujifunza L2.” Na hivyo, makosa ya mwanafunzi atumiapo L2 hutokana na yeye kutoamili sarufi ya lugha hiyo.

Tafiti mbalimbali kuhusiana na makosa yanayojitokeza kwa wanafunzi au wajifunzaji wa L2 zilifanywa na wataalamu mbalimbali. Katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kama L2, tafiti zilizidhihirisha kuwa makosa yanatokana na lugha za kijamii au lahaja zingine za Kiswahili. Pia, ilibainika kuwa tafiti hizo ziliegemea ama upande wa fonolojia, mofonolojia, sintakisia au semantiki. Kwa mfano, Hepkwony (2011), Rukia (2017) na Mashaka (2015) walitafiti makosa na athari kutokana na lugha za asili katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu na wamebainisha matatizo na athari za kimatamshi, kimofolojia na kisintaksia. Naye Aruba na wenzake (2017) walichanganua makosa ya kisemantiki yanayojitokeza kwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Oduor na wenzake (2017) waligundua kuwa wanafunzi wa Kiluo

hufanya makosa ya upatanishi wa kisarufi katika kipengee cha ngeli kutokana na uhamishaji wa sintaksia ya lugha hiyo kwa upatanishi wa sarufi ya Kiswahili. Hata hivyo, tafiti kuhusu makosa na athari za Kingwana katika Kiswahili sanifu hazijafanyika.

Kwa muktadha huo, utafiti huu ulinuia kutathmini makosa ya kisarufi kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu wanaoongea Kingwana kama L1, ili kubaini aina za makosa hayo, kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za makosa hayo na kuchunguza vyanzo vyake katika Kiswahili Sanifu.

1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni haya yafuatayo:

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini makosa ya kisarufi ya wanafunzi wanaoongea Kingwana kama L1 wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni katika baadhi ya Vyuo Vikuu vya Burundi.

1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

- (i) Kubaini aina za makosa ya kisarufi wanayofanya wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu.
- (ii) Kutathmini viwango vya ujitokezaji wa aina mbalimbali vya makosa hayo.
- (iii) Kuchunguza sababu za makosa ya kisarufi katika Kiswahili Sanifu.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

- (i) Ni makosa ya aina gani hufanywa na wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu ?
- (ii) Ni kwa viwango gani vya ujitokezaji wa makosa mbalimbali ya kisarufi ya Kiswahili hutokea kwa wanafunzi hao ?
- (iii) Nini sababu za makosa yanayojitokeza kwa wanafunzi hao ?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kama wanavyosema Nyangwine na Massebo (2016 : 256), “luga ni chombo muhimu cha mawasiliano baina ya watu.” Ili luga itimize dhima hiyo, inawabidi wanajamii luga au watumiaji wowote wa luga husika kuzingatia taratibu na sheria za luga hiyo kwa kuepuka makosa ambayo yangezuia mawasiliano kati yao. Hii ina maana kuwa luga ya Kiswahili kama luga nyingine yoyote ile, huwa na kanuni maalum ambazo ni msingi wa kufanikisha mawasiliano. Hivyo, utafiti huu utakaoshughulikia makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa asili ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu kama luga ya kigeni, utatoa mchango wake wa kipekee katika uwanja wa isimu na luga, aghalabu luga za kibantu.

Kwanza, uchunguzi wa makosa ambayo hutokana na uzoefu wa Kingwana ambayo hujitokeza katika Kiswahili sanifu kinachofundishwa vyaoni, utasaidia katika kutambua tofauti kati ya lahaja ya Kingwana na Kiswahili sanifu. Pili, utafiti huu utasaidia kutambua na kubainisha mifumo ya lahaja ya Kingwana ambayo hutokea katika Kiswahili sanifu. Tatu, utafiti huu ambao utajikita katika uainishaji wa makosa ya kisarufi utakuwa fursa ya kutambua ni makosa gani yanajitokeza kwa wingi na

kutambua chanzo cha makosa hayo na namna ya kuyaepuka. Nne, utafiti huu utakadiria ni kwa kiasi gani makosa haya hujitokeza pamoja na sababu zake kutokea.

Mwisho, pamoja na kusomwa na wanafunzi na wataalamu wengine hususan wa lugha na isimu, matokeo ya utafiti huu yatawafaa kwa kurejelewa katika tafiti zitakazofuata, na hivyo kuziba mapengo ambayo yapo kwa Waswahili kutokana na lahaja au lugha zao za kwanza. Hivyo, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika uchunguzi na uchambuzi wa isimu na lugha za Kibantu.

1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa Kingwana (L1) wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni kwenye vyuo vikuu vya Burundi. Utafiti huu umeangalia kimsingi makosa hayo katika vipengele mbalimbali vya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu haukushughulikia nyanja ya semantiki, bali ulijikita kwenye makosa ya kifonolojia, kimofolojia na sintaksia na pia makosa ya kimofosintaksia yanayohusiana na upatanishi wa kisarufi.

Aidha, utafiti huu ulilenga pande mbili za matumizi ya lugha, yaani lugha ya maandishi na lugha ya mazungumzo. Hivyo, makosa yaliyobainika ni yale yanayotokana na mwanafunzi kutokuwa na umilisi wa kutosha wa Kiswahili sanifu.

1.7 Muhtasari

Sura hii ya utangulizi ilishughulikia mambo ya msingi ya utafiti huu. Kulijadiliwa usuli, tatizo, malengo na maswali ya utafiti huu. Kulizungumziwa pia umuhimu na upeo wa utafiti huu. Hivyo, sura hii imekuwa kama chanzo na kichocheo cha utafiti

huu na imetoa fufunu ya mpangilio wa utafiti wenyewe na njia itayopitiwa kuelekea kwa ufumbuzi wa matokeo. Sura ifuatayo itashughulikia kazi tangulizi ambazo zinashabihiana na utafiti huu kwa ajili ya kutambua pengo lililopo.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusika na tathmini ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kabla ya huu ambazo zilichapishwa kwenye vitabu, makala na tasnifu ili kupata maarifa yanayohusiana na mada hii kwa ajili ya kubainisha pengo lililopo ambalo utafiti huu ulishughulikia. Pia sura hii itawasilisha na kufafanua kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Sehemu hii inahusisha maandishi yaliyotangulia ambayo yanahusu ujifunzaji wa L2, makosa katika lugha na namna ya kuyashughulikia, na athari ya L1 katika uamiliaji au ujifunzaji wa L2. Aidha, tafiti zilizohusika katika sehemu hii zinahusiana na nyanja za lugha ambazo hushughulikiwa na utafiti huu, yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia.

2.2.1 Dhana ya Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Dhana hii ilishughulikiwa na wanazuoni wa lugha tangu miaka ya 1940. Waasisi wake ni pamoja na Robert Lado, Pit Corder, Larry Selinker na Stephen Krashen. Kwa mujibu wa Xie na Jiang (2007), katika miaka ya 1950 Robert Lado alianza kushughulikia kwa utaratibu makosa katika lugha, halafu akaasisi nadharia ya upambanuzi linganishi kwa ajili ya kuyashughulikia makosa katika lugha. Mkabala wa kinadharia wa upambanuzi linganishi unadai kuwa kikwazo kikubwa katika ujifunzaji au uamiliaji wa L2 huwa ni mwathiriano wa L1 na L2, hivi kwamba uchanganuzi linganishi wa lugha zote hizo ungewawezesha watalaamu kutabiri na

kueleza ambayo ni matatizo na ambayo siyo. Mkabala huu ulilenga kufanya “ulinganishi wa lugha ama mbili au zaidi ili kubainisha tofauti na ufanano baina ya lugha hizo” (Fisiak, 1981: 1). Mkabala wa kinadharia wa upambanuzi linganishi ulionyesha madhaifu mbalimbali. Kwanza, katika ulinganishi wa lugha mbili au zaidi, makosa yoyote yanayofikiriwa hayalazimiki kutokea. Pili, makosa yoyote yanayofanywa na mjifunzaji au muamiliaji wa lugha wa L2 hayatokani na L1 wala tofauti baina ya L2 na L1. Hivyo, kutokana na madhaifu ya mkabala huo, nafasi yake ilichukuliwa baadaye na nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM) ambayo iliasisiwa na Pit Corder.

Naye Corder (1967) alichukua msingi wa dhana zilizoasisiwa na Chomsky, yaani umilisi na utendi, akibainisha makosa kama matatizo yanayotokana na ukosefu wa umilisi, na ughalifikaji au kuteleza tu katika lugha kutokana na matatizo katika utendi. Katika makala yake *The significance of Learner Errors* (1967), Corder aliipa mwelekeo mpya nadharia ya UM kwa kujibu swali la kwamba mchakato wa uamiliaji wa L1 ni uleule wa L2 au la. Kwa hilo Corder alitoa pendekezo lifuatalo: “Mchakato uleule unaotumika katika uamiliaji wa L1 ndio unatumika katika L2.” Hivyo, sababu zifuatazo zilitolewa na Corder (1967: 166): Kwanza, binadamu huzaliwa wakiwa tayari na uwezo wa kuamili lugha yoyote. Pili, binadamu wasipotumia uwezo huo katika utoto, basi unawatoka bure. Tatu, binadamu wakitumia uwezo huo katika uamiliaji wa L1, basi hali itatokea hivyo hivyo katika ujifunzaji wa L2. Nne, tofauti kubwa hutokana na motisha ya mwanafunzi au mjifunzaji yeyote. Kwa hiyo, Corder anapendekeza nadharia tete kuwa, baadhi ya michakato inayotumiwa na mwanafunzi au mjifunzaji wa L2 huwa, kwa kiasi

kikubwa, hiyohiyo katika uamiliaji wa L1. Hata hivyo, haimanishi kuwa hali hii ya uamiliaji hukamilika hivyohivyo kila wakati, kwani binadamu huamili lugha kwa namna tofauti.

Selinker (1972) kwa upande wake alibuni na kushughukia nadharia ya mwingiliano wa lugha (ML tangu sasa). Huu ni mwongozo wa utafiti juu ya wajifunzaji wa L2 ambao sasa umekubalika katika uchunguzi wa makosa. Kwa mujibu wake, katika ujifunzaji au uamiliaji wa L2, ukweli ni kwamba mfumo wa lugha ya mwanafunzi au mjifunzaji sio ule wa L1 wala L2, bali mfumo mpya ambao humiliki sifa kutoka lugha zote mbili, hivi kwamba mjifunzaji wa L2 huongea lugha yenye mfumo unaotokana na mwingiliano wa L1 na L2. Hivyo, nadharia ya ML inadai kuwa kauli au ujumbe kutoka kwa mjifunzaji au mwamiliaji wa L2 hauwezi kabisa kulingana na matarajio ya wazungumzaji asili wa hiyo L2, kwani si tafsiri kamili ya L1; tena hutofautiana kimfumo na L2. Aidha, miundo ya tungo zitolewazo na mjifunzaji au mwamiliaji wa L2 hazijitokezi kwa unasibu. Mkabala wa kinadharia wa ML unapendekeza kuwa, data faafu ya nadharia ya ujifunzaji wa L2 lazima izingatie kauli kutokana na kujaribu kutunga tungo zenye maana kutoka kwa L2. Kutokana na hayo hapo juu, kigezo muhimu ni kwamba mjifunzaji au mwamiliaji wa L2 hujikita zaidi katika kuwasilisha ujumbe kuliko kuzingatia kanuni na mazoezi ya kimuundo yaliyofanyika darasani.

Kwa mujibu wa Krashen (1981:1), “uamiliaji wa lugha ni kama vile mchakato ambao watoto huhusisha katika kuamili L1 au L2. Hili linahitaji kujikita kwenye mawasiliano katika lugha lengwa ambapo wazungumzaji hawajali mfumo wa tungo, ila tu ujumbe uliomo kwenye tungo hizo.” Anaposhughulikia ujifunzaji wa lugha na

maendeleo yake, Krashen (1987) anaeleza kuwa, katika kujifunza L2 haihitajiki mhusika kuelewa au kujua kanuni za kisarufi, bali kinachohitajika huwa ni ushirikiano wake na watu wengine kwa ajili ya kuipata L2, yaani ujifunzaji asili. Hivyo, mzungumzaji huwa ni msikilizaji ambaye hajihusishi katika matamshi bali katika ujumbe unaowasilishwa na uelewa wao.

Pamoja na waanzilishi hapo juu, wataalamu wengine walishughulikia ujifunzaji wa L2. Baadhi yao ni kama wafuatao: Masebo na Nyangwine (2016:27), wanapozungumzia ujifunzaji wa L2 wanasema kuwa

ufasaha wake katika kujifunza L2 ni lazima ulingane na ule wa L1 kwa kusikiliza, kuzungumza, kufuatilia au kusoma na kuandika. Vilevile kunakuwepo na mazingira dhahiri yenye kuleta maana. Kuwe na mazoezi mengi ya mara kwa mara. Mwisho, lazima kuhusisha mazingira ya lugha ya pili na yale ya lugha ya kwanza.

Wanahakikisha kuwa ujifunzaji wa L2 huchukua muda mrefu na ni changamani. Kwa mujibu wa Gardner (1985), umri, akili, kipaji, mielekeo ya lugha, muktadha wa kujifunza na matokeo ya kujifunza huwa ndiyo mambo muhimu yanayochangia ujifunzaji wa L2. Huyu anazingatia vigezo vya Saikolojia Jamii. Aidha, kama anavyonukuliwa na Mpangala (2015:31) “uamuzi wa kuendelea kujifunza na kuitumia L2 hutegemea sifa mbalimbali zinazohusiana na mielekeo pamoja na motisha.”

Sarah (2018), akishughulikia ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2, anabainisha sababu zinazomfanya mjifunzaji atumie kimakosa kanuni za lugha anayojifunza. Sababu hizo ni kama vile mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, tofauti zakimuundo kati L1 na L2, athari ya L1, walimu kutokuwa na

ujuzi wakufundisha Kiswahili kama L2 kwa wajifunzaji hao na uhaba wa vifaa vyakujifunzia na kufundishia.

2.2.2 Makosa katika Lugha

Tafiti mbalimbali kuhusiana na makosa yanayojitokeza katika lugha zilifanywa na wataalamu mbalimbali. Tafiti hizi huegemea kwenye pande za maandishi na mazungumzo. Aidha, zinahusu nyanja tofauti za lugha aghalabu fonolojia, mofolojia, sintaksia, leksikolojia na sematiki. Miongoni mwa wanazuoni wa lugha walioshughulikia makosa katika lugha ni wafuatao:

Corder (1967), aliyekuwa mwanzilishi wa dhana ya makosa katika lugha, anabainisha mikabala miwili inayopendekeza mitazamo miwili tofauti juu ya makosa ya lugha. Kwanza, kwa mujibu wa baadhi ya wanaisimu, makosa katika lugha huwa ni dalili ya udhaifu wa mbinu za kufundishia. Pili, wengine huhakikisha kuwa, ingawa wazungumzaji hufanya bidii iwezekanavyo kwa ajili ya kuzuia makosa, yatalazimika kutokea iwapo lugha itatumiwa katika mawasiliano kwani dunia yenyewe huwa hivyo. Vilevile, anaeleza kuwa makosa yanayojitokeza katika L2 hutokana na mwathiriano wa L1. Msimamo wake ulitokea kuwa, umilisi wa L1 huwa chanzo cha uamiliaji wa L2, hivi kwamba makosa yafanywayo na mjifunzaji sio dalili za vikwazo, bali ni dalili za mbinu za kufundishia.

Pia, Corder (1973) anaainisha makosa kwa kuzingatia tofauti baina ya lugha ya mwanafunzi au mjifuzaji wa L2 na kauli yake au mfumo wake mpya. Hivyo, makosa katika lugha huangukia katika vikundi vinne, yaani (i) udondoshaji wa viambishi, (ii) ongezeko la viambishi au vipashio visivyohitajika au visivyo sahihi,

(iii) uteuzi wa viambishi au vipashio visivyo sahihi na (iv) mpangilio mbaya wa viambishi. Hata hivyo, Corder (1973) mwenyewe anatahadharisha kuwa uainishaji huu hautoshi kuelezea makosa. Hii ndiyo sababu anajumuisha kiwango cha makosa ya kiisimu chini ya nyanja za mofolojia, sintaksia na leksimu (Corder, 1973). Kwa mfano, kuna udondoshaji wa kimofolojia (mf. Watu *tatu* badala ya *watatu*), udondoshaji wa kisintaksia (Mf. “Ameondoka nyumbani”, badala ya “Ameondoka *kwenda* nyumbani”); ongezeko la kimofolojia (mf. “Walijenga *mashule*” badala ya *shule*), ongezeko la kisintaksia (mf. “Watafika mwezi *wa* Januari” badala ya “mwezi Januari”), ongezeko la kileksimu (mf. “Wameingia *ndani ya* nyumbani” badala ya “Wameingia nyumbani”) ; uteuzi wa kisintaksia (mf. “Walipanda *juu ya* mti” badala ya “Walipanda mti”), n.k. Mifano hii inahakikisha kuwa kosa huweza kuhusu fonimu, mofu, neno, sentensi na hata aya. Hivyo, makosa huweza kuathiri ama tungo nzima (*global*) au sehemu tu (*local*) (Brown, 2000). Makosa yanayoathiri tungo hupotosha mawasiliano hali kwamba sentensi nzima hupoteza maana (mf. “Kucheza mpira hospitalini mgonjwa”), ilhali makosa yanayoathiri sehemu ya tungo kama vile fonimu au mofu hayazuii mawasiliano na huweza kusahihishwa (mf. “Mugonjwa hatachezaga mpila hospitalini”).

Nao James (1989, 1998), Ellis (1995), Ziahosseiny (1999), Keshavarz (2003, 2006), Şanal (2007), Darus (2009) na Kazemian & Hashemi (2014) walishughulikia vyanzo vya makosa yafanywayo na wanafunzi wajifunzao lugha fulani kama L2. Wanazuoni hawa wanakubaliana kuwa sababu kuu za makosa huwa ni pamoja na (i) uhamishaji wa lugha, (ii) matumizi kupita kiasi ya kanuni fulani, (iii) ufupishaji, (iv) kwa mwanafunzi kujali sana nyanja za kisarufi za L2 badala ya zile za L1, (v) kutozijua kanuni za lugha lengwa na (vi) mwingiliano.

Nao Massebo na Nyangwine (2016) walibainisha aina kuu mbili za makosa katika lugha, yaani makosa ya kisarufi ambayo yanatokana na ukiukaji wa kanuni za lugha na makosa ya kimantiki ambayo yanatokana na kukosekana kwa utaratibu wa kufikiri. Kwa mujibu wao, makosa ya kisarufi ni kama vile makosa ya matamshi, makosa ya muundo, makosa ya msamiati, makosa ya kuacha maneno, makosa ya kuongeza viambishi au vitamkwa na makosa ya tafsiri sisisi. Wao wanaegemea kwenye msimamo usemao kuwa makosa yataendelea kufanyika iwapo lugha itaendelea kutumiwa. Hata hivyo, wanapendekeza kuepuka na makosa ya lugha hasa katika vituo rasmi kama vile ofisini, kanisani, shuleni na vyuoni.

Pamoja na kazi hizi zilizoshughulikia makosa kwa ujumla, baadhi ya tafiti zilishughulikia makosa yanayojitokeza katika nyanja tofautitofauti za lugha kwa wanafunzi wajifunzapo lugha husika kama L2. Tafiti hizi zinadhihirisha kuwa katika ujifuzaji wa lugha fulani kama L2, makosa hutokana na sababu mbalimbali hasa athari za L1.

Kwa mfano, Jabeen na wenzake (2015) walishughulikia makosa ya wanafunzi wa vyuo vikuu vya Pakistani na Iraniwajifunzao Kiingereza kama L2. Wakitumia makundi au aina za makosa kama zilivyopendekezwa na Corder (udondoshaji, ongezeko, uteuzi, mpangilio mbaya), waligundua kuwa wanafunzi hao hufanya makosa ya kisarufi aghalabu katika maandishi, mengi yakihusu matumizi mabaya ya nyakati za vitenzi.

Kwa upande wake, Cioroianu (2015) alishughulikia makosa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiromania kama L2. Sababu za matatizo na makosa ya

wanafunzi wanapojifunza lugha hiyo hupatikana katika kiwango cha fonetiki na katika nyanja za msamiati, mofolojia na sintaksia. Upande wa mfumo wa kifonetiki, makosa mengi hutokea katika matamshi au maandishi ya irabu \check{a} , \hat{a} , \hat{i} na konsonanti ř na ř . Upande wa makosa ya msamiati ambayo huwa si mengi, hutokana na mwathiriano wa kisemantiki iwapo maneno mawili au zaidi kutoka Kiromania yana maana moja katika L1. Nayo makosa ya kimofosintaksia hutokea kwa wingi kutokana na wanafunzi kutoweza kubainisha kanuni za kisarufi za L1 na L2. Hivyo, wanafunzi hushindwa kubainisha tofauti kuhusu mpangilio wa maneno na upatanisho wa kisarufi katika sentensi, kutambua tofauti za matumizi ya nyakati na alama zake, hali za vitenzi na matumizi ya jinsia katika L1 na L2.

Katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, baadhi ya tafiti zilishughulikia makosa ya kisarufi yanayotokana na athari za lugha za kijamii au lahaja zingine za Kiswahili katika Kiswahili sanifu. Oduor na wenzake (2017) walishughulikia makosa yanayotokana na athari za uhamishaji wa sintaksia ya Kiluo katika upatanishi wa kisarufi wa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa kenya ambao L1 ni Kiluo hufanya makosa mengi ya kisarufi hali ambayo huathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Katika utafiti huu, iligundulika kuwa uhamishaji wa sarufi ya Kiluo huathiri upatanishi wa kisarufi katika Kiswahili kwa sababu kanuni za lugha hizi mbili hutofautiana kabisa. Kiluo ni lugha ya kinilotiki ambayo maneno yake machache tu huambishwa, ilihali Kiswahili ni lugha ya kibantu ambayo kila neno huambishwa. Aidha, viwango vya kisarufi vilivyobainika kuwa huathiriwa na athari za uhamishaji wa sarufi ya Kiluo kwenye sarufi ya Kiswahili ni vitatu, yaani kiwango cha ngeli, nafsi na idadi.

Mpangala (2018) alishughulikia athari ya lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Akitumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia, aligundua kuwa wanafunzi wa Kimakonde wa shule za msingi za wilaya ya Mtwara Vijijini hufanya makosa ya matumizi ya L1 katika lugha ya Kiswahili (L2). Makosa hayo ni ya kimatamshi, msamiati, maana na matatizo ya kisarufi.

Naye Nyanda (2015) alitafiti athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Mtafiti huyu anaeleza kuwa wanafuzi wa Kinyamwezi wa eneo hilo wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama L2 hufanya makosa kutokana na hiyo L1. Mtafiti huyu alibainisha makosa ya kimsamiati kama vile kusema '*lino linasata*' badala ya kusema '*jino linauma*', au '*mama anasunta*' badala ya kusema '*mama anachechemea*'; makosa ya kimatamshi kama vile matumizi ya fonimu /l/ badala ya /r/ au /z/ badala ya /ð/ (mf.: *lusha* badala ya *rusha*, *malazi* badala ya *maradhi*). Kuhusu makosa ya kimaana, kwa mfano, mzungumzaji wa Kinyamwezi husema kuwa, '*Namsanga kuduhu*' akimaanisha '*Sijamkuta*' lakini azungumzapo Kiswahili akimaanisha '*Sijamkuta*' husema, '*Nimemkuta hayupo*'; hili likiwa kosa la kimantinti. Pia, husema '*Nitakuja jana*' akimaanisha kuwa, '*Nitakujakesho*'. Hili hutokana na sababu kwamba maneno ya Kiswahili *kesho* na *jana* hutafsiriwa na neno moja *igolo* katika Kinyamwezi.

Aruba na wenzake (2017) walichanganua makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Matokeo ya kazi yao yanaonyesha kuwa wanafunzi wanaojifunza L2 hufanya makosa ambayo yanaweza kubainishwa, kuchanganuliwa, kuainishwa na kutathminiwa ili kubainisha mfumo unaofanya kazi. Baadhi ya makosa

waliyoyabaini ni pamoja na matumizi ya msamiati usiofaa (mf.: Baba alienda baharini *kumshika* papa <kuvua>, Chungu kilichopikiwa samaki hunuka *chombo* <shombo>), kuunganisha maneno visivyo (mf.:Yohana *anasifanjema* <ana sifa njema>, Mwalimu wa Kiswahili ana *dukakubwa*<duka kubwa>), kuacha sauti katika neno (mf.:**Mag eti* yana umuhimu lakini wanafunzi *hawa omi*, **Ni vi uri* kusoma magazeti ili *kubo es a* lugha yetu) na mrundiko wa maneno katika Sentensi (mf.: *Sukari ilimwagika sakafuni yote na mtoto* <Mtoto alimwaga sukari yote sakafuni>). Kwa mujibu wao, iwapo makosa yatatokea katika maandishi au mazungumzo, mawasiliano kama shughuli kuu ya kibinadamu hayatafaulu.

Hepkwony (2011) alitafiti matatizo ya kisarufi ya wanafunzi wa Kikipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu na alibaini chanzo cha makosa ya wanafunzi hao watumiaapo Kiswahili sanifu kama L2, na mbinu mwafaka za kufundishia Kiswahili sanifu kwa wanafunzi hao. Mtafiti alijikita katika matatizo ya kimofolojia na kisintaksia. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa makosa mengi ya kisarufi hutokana na athari za lugha ya Kikipsigis. Mtafiti aliona pia kuwa makosa haya huhusu ujumlishaji mno wa baadhi ya maumbo ya sarufi ya Kiswahili.

Pia Rukia (2017) alitafiti athari ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu nakugundua kuwa matumizi ya matamshi, maumbo ya misamiati na misamiati yenyewe ya Kimakunduchi huathiri Kiswahili sanifu. Kwa mfano, Kimakunduchi hudondosha nazali katika msamiati wake, wakati nazali inapokutana na sauti [pj] na kikwamiza [tʃ] na nazali kama vile [ɲ]. Pia nazali hudondoka zinapofuatana na vikwamiza ghuna kama vile [z], na [v] katika baadhi ya msamiati. Neno *mnyama* hutamkwa *nyama*, *mpya* hutamkwa *pya*, *mvua* hutamkwa *vua*, *nchi* hutamkwa *chi*,

nzi hutamkwa *zi*. Aidha, matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa kuna baadhi ya misamiati ya Kimakunduchi inayofanana na ya Kiswahili, hali ambayo hukwamisha mawasiliano na kuleta athari kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi wanapoongea Kiswahili sanifu. Misamiati hiyo hugawika katika misamiati ya majina ya siku, nyakati, misamiati ya walemavu, misamiati ya majina ya ukoo, misamiati ya kazi ambazo hufanywa na jamii husika. Utafiti huu ulibaini kuwa wazee wa Kimakunduchi walitoa athari kwa 65%, vijana walitoa 45% ambapo walimu walipata 60%.

Ame (2017) alitafiti athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili sanifu. Mtafiti huyu aligundua kuwa lahaja ya Kitumbatu huathiri msamiati, mazungumzo, maandishi na maumbo ya maneno katika Kiswahili Sanifu. Pia alibaini sababu na athari hizo katika Kiswahili sanifu kama vile ukosefu wa vitabu vya kufundishia, kutumia Kitumbatu kuliko Kiswahili sanifu madarasani, kutokuwa na ujuzi wa Kiswahili Sanifu na umbali wa kijiografia kati ya Tumbatu na Unguja.

2.2.3 Uhusiano wa L1 na L2 katika Mukadha wa Ujifunzaji

Kamailivyokwishaelezwa, lugha yoyote ni mfumo wenye sheria ambao unatumiwa na jamii kwa ajili ya mawasiliano. Hata hivyo, ingawa kila lugha ina upekee wake, kuna sifa za kimajumui ambazo humfanya mwanafunzi wa L2 au lugha ya kigeni kuzingatia kanuni za L1 aliyolelewa nayo. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa mazoea ya L1 ya mwanafunzi au mjifunzaji kuathiri L2 anayojifunza ni ya kawaida, kwa sababu huyahamisha kutoka L1 kwenda L2. Kwa mujibu wa Lado (1957: 58),

matumizi ya mfumo wa kisarufi hutegemea mazoea ya mzungumzaji. Kwani isingewezekana kufikiria mabadiliko yote, upanukaji na vizuizi katika utoaji wa sentensi hata moja kwa kuitamka karibu kwa namna ya kawaida. Mzungumzaji wastani, tangu utotoni mwake, hujaribu kuifanya lugha yake kuwa jambo la kawaida.

Kutokana na maoni ya Lado, kuamili L2 ni kujizoeza lugha hiyo badala ya L1, hasa pale L2 inapotofautiana na L1.

Aidha, suala la kuhusiana na umuhimu wa L1 katika kujifunza L2 lilishughulikiwa na wataalamu mbalimbali wakiwa na misimamo kinzani. Kama anavyoeleza Noor (1994), “tafiti zilihusu hasa uchunguzi wa pande mbili za uhusiano kati ya L1 na L2. Kwanza, uhamishaji faafu wa maarifa kutoka L1 katika mchakato wa kujifunza L2, pili, uhamishaji hasi au mwathiriano.”

Uhamishaji faafu huhusu uhamishaji katika L2 wa misingi ya L1 ambayo humwezesha mwanafunzi au mjifunzaji kuamili L2 au kupata umilisi wa lugha hiyo, kutokana na kufanana kwake. Upande mwingine, uhamishaji hasi au mwathiriano huwa ni uhamishaji kutoka L1 wa misingi ambayo hudunisha uamiliaji wa L2 kutokana na tofauti kati ya mifumo hiyo miwili (Van Els et al., 1984:49).

Kutokana na maelezo hapo juu, katika muktadha wa ujifunzaji L2 au lugha ya kigeni, uhusiano baina ya L1 na L2 umedhihirika na hutokea pale ambapo L1 inachangia katika ujifunzaji wa L2.

Hata hivyo, kwa muda mwingi uliopita, uhusiano huo haukuzingatiwa sana, kwani umuhimu wa L1 katika kufundisha L2 haukupewa kipaumbele. Walimu waliwaza kama wangetumia L1 katika kufundishia L2. Kwa mujibu wa Sharma (2006: 80),

“suala la walimu wa lugha kutumia L1 ya wanafunzi katika kufundishia L2 au lugha ya kigeni liliibua utata kabisa.”

Upande mmoja, baadhi ya watafiti walihimiza matumizi ya L2 kama mbinu mwafaka katika kufundishia L2. Kwa mfano, katika kufundisha Kiingereza, Willis (1981), kama alivyonukuliwa na Sharma (2006: 80), anaona kuwa ni bora “kufundisha Kiingereza kwa Kiingereza katika mazungumzo au matumizi ya Kiingereza iwezekanavyo.” Naye Auerbach (1993:5) anaunga mkono wazo hilo kwamba “kadiri wanafunzi wanavyohusika na Kiingereza, kadiri wanavyokielewa zaidi; kadiri watakavyosikia na kutumia Kiingereza, wataanza kupata umilisi na kutafakari kwa Kiingereza. Njia muhimu ya kujifunza lugha hiyo itakuwa kuwahimiza wanafunzi kuitumia.”

Upande mwingine, uhusiano baina ya L1 na L2 au ya kigeni ulizingatiwa na L1 ikapewa hadhi kubwa, hivi kwamba kulihimizwa kutumia L1 katika ufundishaji L2 au ya kigeni. Kama alivyonukuliwa na Forman (2005: 65), Cook (1999) anaeleza kuwa “wazungumzaji wa L2 tayari wana umilisi wa L1 akilini mwao. Kila wanachokisema kwa uwazi katika L2 kinahusisha L1 ingawa ni kwa namna isiyodhihirika.” Hivyo, kuna haja ya kutumia L1 katika kufundisha L2. Kwa mujibu wa Harbord (1992: 352), sababu zifuatazo huwafanya walimu kuzingatia L1 katika kufundisha L2 au ya kigeni. “Kwanza, kuwezesha mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi, pili, kuwezesha uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi na, tatu, kurahisisha ujifunzaji.” Naye Atkinson (1987: 242) anasema kuwa “jukumu jingine muhimu la L1 katika kufundisha L2 au ya kigeni ni kuwawezesha wanafunzi kueleza

wanachopenda kabisa kusema mara kwa mara, hakika kilicho muhimu sana darasani.”

Kutokana na maelezo yote hapo juu, imedhihirika kuwa kuna uhusiano baina ya L1 na L2 katika ujifunzaji wa L2. Kwanza, L1 na L2 au ya kigeni huchangia sifa za kimajumui ambazo humrahisishia mwanafunzi au mjifunzaji wa L2 kufunuliwa baadhi ya mihimili ya lugha hiyo. Pili, msingi wa uzungumzaji kwa binadamu yeyote huamilika kupitia L1. Hivyo, L1 ndicho kielelezo muhimu katika kujifunza L2 au ya kigeni, kwani L1 huwa ndiyo chombo kinachohifadhi utamaduni wa mzunguzaji. Tatu, katika muktadha wa ujifunzaji na ufundishaji wa L2, L1 huwa zana ya kurahisishia ushirikiano baina ya wanafunzi na walimu. Tafiti mbalimbali zilihakikisha kuwa wanafunzi wengi hujaribu kuelewa walimu wao kwa kutumia L1 (Mahmutoğlu na Kicir, 2013:54). Aidha, kwa wanafunzi, L1 huweza kutumiwa kwa ajili ya kueleza kazi zao. Hivyo, wanafunzi wanaweza kujikita kwenye kazi bila tatizo lolote. Matumizi ya L1 hufanikisha ujifunzaji wa L2 kwa sababu husaidia katika kuchakata na kukamilisha kazi za wanafunzi. Matumizi ya L1 huwasababisha wanafunzi kufurahia majukumu yao. Hivyo, ni dhahiri kuwa wanafunzi wanapaswa kuzingatia L1 kujifunza L2.

Hata hivyo, ingawa kuna faida za kuzingatia L1 katika kujifunza L2, kutumia kwa kiasi kikubwa L1 hudunisha ujifunzaji wa L2. Katika hali hii, wanafunzi hutegemea zaidi L1 kuliko L2 au ya kigeni inayohusika na ujifunzaji. Pia, katika hali hii, wanafunzi hushindwa kutambua umuhimu wa kujifunza L2 au ya Kigeni, hivi kwamba “hupoteza nia na tamaa ya kushiriki katika kuitumia katika siku zao zijazo” (Jones, 2010).

2.3 Pengo la utafiti

Maandishi yaliyojadiliwa hapo juu yamedhihirisha shughuli za watafiti mbalimbali kuhusu makosa katika lugha kwa ujumla na yanayofanywa na wajifunzaji wa L2 kwa namna ya pekee. Kwa mujibu wa maandishi hayo, tafiti nyingi kuhusu makosa ya kisarufi katika Kiswahili hutokana na kuathiriwa na lugha zingine za kibantu au lahaja za jamii ambazo huchukuliwa kama L1. Pia, imedhihirika kuwa wanafunzi wa L2 ikiwemo Kiswahili hufanya makosa katika mazungumzo au maandishi yao. Makosa hayo yanajitokeza katika kiwango cha fonolojia, morfolojia, sintaksia na semantiki.

Isitoshe, kuna tafiti mbalimbali ambazo zilishughulikia lahaja za Kiswahili, ikiwemo lahaja ya Kingwana. Ingawa wataalamu kama Van Der Kerken (1944), Polome (1967), Whiteley (1969), Nshimirimana na wenzake (2020) n.k. walishughulikia lahaja ya Kingwana, kutalii tafiti hizo kumetoa mwanga kuwa hakuna andiko lililoshughulikia ama athari za Kingwana (L1) katika uamiliaji wa Kiswahili (L2) sanifu au makosa yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu kutokana na athari za Kingwana. Hivyo, utafiti huu umeonekana muhimu katika ukuzaji wa Kiswahili kwa kutoa mchango wake katika uwanja wa ufafanuzi wa makosa katika lugha ili kuziba pengo. Utafiti huu utajikika katika kutathmini makosa ya kisarufi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni katika baadhi ya vyuo vikuu vya Burundi wazungumzao Kingwana kama L1 kwa kubaini aina za makosa hayo, kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za makosa hayo na kuchunguza vyanzo vyake.

2.4 Mkabala wa Kinadharia

Massamba (2004:89) anasema kuwa “nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kueleza jambo.” Hivyo, utafiti wowote hufanyika kwa kutumia nadharia inayowiana kabisa na uwanja wa utafiti husika. Kwa mujibu wa Nshimirimana (2014:6), “ utafiti wa kiisimu huweza kufanyika kwa kutumia nadharia moja, mbili au zaidi ; matumizi ya nadharia zaidi ya moja yakitokana na utata wa swala linalochambuliwa.” Naye Novakova (2010:8) anasema kuwa “utafiti wa kisayansi huhitaji misingi thabiti ya kinadharia.” Vilevile, lugha huwa ni jambo tata sana hivi kwamba huwa vigumu kuichunguza na kuichambua kwa kuzingatia mfumo mmoja wa kinadharia. Hata hivyo, ili kulifanyia kazi suala hili, nadharia ya “Uchanganuzi Makosa” (kuanzia sasa UM) imedhihirika kuwa muhimu zaidi, kwa maana kwamba utafiti huu utahusu uchanganuzi wa makosa ya wanafunzi katika maandishi na mazungumzo ya lugha ya pili.

2.4.1 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Nadharia ya UM iliasisiwa na Stephen Pit Corder (1967) ili kutambua na kuainisha makosa, na kufafanua chanzo chake. Hii inadhihirisha kuwa nadharia hii inatumika kuchunguza jinsi gani makosa katika lugha yanaweza kushughulikiwa. Kwa mujibu wa nadharia ya UM, baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza L2 hutokana na athari za lugha ya kwanza. Ijulikane kuwa nadharia ya UM ilitokea kuwa kibadala cha nadharia ya Uchanganuzi Linganishi (UL) iliyoasisiwa na Fries (1945) na kuendelezwa na Robert Lado (1957). Kama anavyosema Ntawiyanga (2018:18) , “Kulingana na Nadharia ya UL makosa yalitazamwa kama matokeo ya

maingiliano ya L1 na L2 tu ambapo mwalimu aliweza kutabiri makosa ya wanafunzi kwani lengo lake lilikuwa kufundisha tofauti za kiisimu kati ya L1 na L2.”

Hii ina maana kuwa, kwa mujibu wa nadharia ya UL, uchanganuzi wa makosa ulikuwa kazi ya ulingalishi wa mifumo sahihi ya lugha moja na nyingine, yaani L1 ya mwanafunzi na L2 anayojifunza. Tofauti na nadharia ya UL, nadharia ya UM inazingatia kuwa makosa yanayofanywa na mwanafunzi katika kujifunza L2 ni ishara kwamba ametilia mkazo kujifunza na kuelewa kanuni za lugha hiyo. Isitoshe, nadharia ya UM inaelekeza kuwa makosa katika lugha yanaweza kuchunguzwa na kuainishwa kulingana na kiwango cha lugha, hivi kwamba yanapatikana makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati, kisintaksia na kisemantiki.

2.4.2 Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Kama inavyoelezwa na Corder (1967:21-25), nadharia ya UM inatumika kwa hatua tatu zifuatazo :Kwanza, ni utambuzi wa ughairi. Msingi wa hatua hii ni kwamba “Kila sentensi ichukuliwe kuwa na ughairi hadi ibainike kuwa sivyo” (Corder, 1967:21). Hii ina maana kuwa sentensi inaweza kudhihirisha muundo sahihi kulingana na L2 ikiwa na ughairi usiodhihirika kwa uwazi. Hivyo mtafiti anatakiwa kuchunguza kuwa sentensi iliyotolewa na mwanafunzi inawiana na kanuni za L2 kwa njia dhahiri au isiyodhihirika. Hatua hii huzingatia pia muktadha wa matumizi, hivi kwamba sentensi sahihi hulingana na muktadha.

Pili, ni kueleza sababu za lahaja ghairi ya mwanafunzi. Mtafiti anachunguza kama mwanafunzi anatumia L2 kwa kuzingatia L1. Anachunguza ni kwa kiasi gani mwanafunzi anafanya makosa kutokana na L1 kuathiri L2. Kwa maneno mengine,

sentensi za lugha mbili, yaani L1 na L2 huchunguzwa na kufafanuliwa kwa kulinganishwa kwa msingi wa mfumo mmoja kimuundo.

Tatu ni maelezo. Hii ni hatua muhimu na ya mwisho katika mchakato kulingana na nadharia ya UM. Wakati hatua mbili za kwanza hutumika kwa misingi ya kiisimu, hatua ya maelezo inazingatia misingi ya kisaikolojia, yaani kiisimu nasfia. Katika hatua hii, mtafiti anajaribu kutambua na kueleza sababu zinazomfanya mwanafunzi kukiuka yarufi ya L2.

Upande mwingine, kwa mujibu wa Corder (1974), nadharia ya UM inaweza kutumiwa kwa kufuata hatua zifuatazo :

Kwanza, kukusanya data : ambapo mtafiti anakusanya sampuli ya lugha ya mwanafunzi kwani hutoa data za UM. Inambidi mtafiti atambue jinsi asili ya sampuli inayokusanywa inavyoweza kuathiri asili ya sampuli kutokana na makosa yanayofanywa na mwanafunzi.

Pili, kutambua makosa : ambapo mtafiti analinganisha sentensi au kauli za mwanafunzi na zile ambazo zingetolewa na mzawa wa lugha husika katika muktadha uleule.

Tatu, kuainisha makosa : ambapo mtafiti anaainisha makosa kulingana na kategoria za kisarafu ambazo zinahusika katika utafiti wake.

Nne, kueleza makosa : ambapo mtafiti anachunguza chanzo cha makosa kwa minajili ya kutambua na kuonyesha sababu za makosa hayo. Mtafiti anafaa kutambulisha vipengele vinavyotatiza wanafunzi na kusababisha makosa kutokea.

Tano, kutathmini makosa : ambapo, baada ya kuainisha makosa, mtafiti anajikita katika uchanganuzi wa kiwango cha athari ya kila kosa. Kutathmini makosa huweza kupendekeza ni kosa gani linaweza kushughulikiwa katika ufundishaji.

Kutokana na hatua hizi, ni dhahiri kuwa nadharia ya UM inaweza kutoa picha ya aina za makosa ya wanafunzi wanaojifunza L2. Kukusanya data, kutambua, kuainisha, kueleza na kutathmini makosa ni njia mwafaka ziongozazo mtafiti katika kuchakata makosa ya wanafunzi wa L2. Isitoshe, nadharia ya UM inaweza kusaidia walimu katika kushughulikia na kusahihisha makosa ya wanafunzi, pamoja na kuwaelekeza wanafunzi ili kuzuia utokeaji wa makosa wanapojifunza L2. Kuelewa mifumo ya L1 na L2 ni jambo muhimu katika kuchakata, kuchambua na kufafanua makosa kwa msingi wa nadharia ya UM.

2.5 Hitimisho

Katika sura hii kumejadiliwa kazi zilizotangulia ambazo zinahusiana na mada hii. Maudhui ya sura hii yamedhihirisha mtazamo wa wataalamu mbalimbali ambao kazi zao zinahusiana na mada ya utafiti huu. Baada ya utangulizi, kumetokea sehemu ya mapitio ya kazi tangulizi ambayo nayo imefuatwa na ile ya pengo la utafiti. Mwishoni, mtafiti amejadili mkabala wa kinadharia ambao utaongoza utafiti huu. Sura ifuatayo itajikita katika uchambuzi wa mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2015), mbinu ni namna ya kufanya jambo. Hivyo, sura hii itazungumzia mbinu mbalimbali zitakazotumika katika kuufanyia kazi utafiti huu. Kutabainishwa eneo ambapo utafiti utafanyiwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji wa data na mkabala wa utafiti. Mwishoni, kuna muhtasari wa sura hii.

3.2 Eneo la Utafiti na Watafitiwa

Kwa mujibu wa KAKAMA (2019:49), “nchi ya Burundi ina vyuo vikuu arobaini ambavyo miongoni mwake vitano vinamilikiwa na serikali ilhali thelathini na vitano ni vyuo vya kibinafsi.” Utafiti huu unaohusika na makosa ya wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vitano ambavyo vinne miongoni mwake viko mjini Bujumbura kwa sababu Bujumbura ndio mji mkuu ambapo lahaja ya Kingwana inatumika kiasili. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Burundi (Université du Burundi, U.B), Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d’Afrique, USA), Chuo Kikuu cha Mwanga cha Bujumbura (Université Lumière de Bujumbura, ULBu), Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des Grands Lacs, UGL) na Chuo Kikuu cha Mwaro kipatikanacho mkoani Mwaro (Université de Mwaro, UM). Uteuzi wa vyuo tafitiwa ulifanyika kwa usampulishaji wa makusudi na ulijikita kwenye vyuo ambavyo hufundisha Kiswahili kama kozi muhimu ya lazima. Mtafiti alichagua vyuo ambavyo alikuwa anajua kuwa vina wanafunzi wazawa wa Kingwana. Uteuzi huu wa kimakusudi wa madarasa na

vyuo tafitiwa ulitokana na idadi ya wanafunzi wa Kingwana kutoka ama Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo au Burundi wajifunzao Kiswahili kwenye chuo husika. Watafitiwa ni wale wanafunzi wa mwaka wa pili (Bac 2) na mwaka wa tatu (Bac 3) kutoka hivyo vyuo vikuu vitano ambavyo vina wanafunzi wengi wa Kingwana, ambao tayari walisoma Kiswahili sanifu katika mwaka wa kwanza na ambao wanaendelea kujifunza lugha hiyo katika mwaka wa pili na wa tatu.

3.3 Sampuli Lengwa ya Watafitiwa na Usampulishaji

3.3.1 Sampuli Lengwa

Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo mtafiti humpatia data na kutoa mahitimisho yake. Hivyo, ni dhahiri kuwa sampuli hutokana na kundi lengwa ambalo nalo “ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteua watafiti wake akiwa anatambua kwamba watamsaidia kupata data anazozihitaji ili kujibu maswali yake ya utafiti” (Salim, 2015:27). Aidha, naye Walliman (2011) anapofafanua kundi lengwa katika utafiti, anasema kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio kwa ujumla. Kwa maneno mengine, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli ya utafiti inaweza kuchaguliwa.

Katika utafiti huu, kundi lengwa lilikuwa ni wanafunzi wa Kingwana wasomao kwenye vyuo vikuu vya Burundi mjini Bujumbura.

3.3.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa (Sigh, 2007). Hii ina maana kuwa,

katika utafiti wowote, inambidi mtafiti kuteua mbinu mwafaka ya kuichagua sampuli ya watafitiwa. Ziko njia mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji nasibu ambapo uwezekano wa kumchagua mwana kundi lengwa yeyote huwa mkubwa, na usampulishaji usio nasibu ambapo kuchagua sampuli kunatokana zaidi na maamuzi ya mtafiti.

Katika utafiti huu, michakato ya usampulishaji yote miwili ilitumiwa. Kwanza, usampulishaji usio nasibu ulitumika katika kuwachagua wanafunzi waliokuwa wanafundishwa Kiswahili sanifu vyuoni waliokuwa tayari wazungumzaji wa Kingwana (L1). Pili, usampulishaji nasibu ulitokea baada ya kuwapata wenyeji wa Kingwana (L1) wasomao Kiswahili sanifu (L2) ambapo miongoni mwao walitegemewa kujibu maswali ya mtafiti.

Hivyo, utafiti huu ulichagua vyuo vitano ambapo wanafunzi ishirini (20) kwa kila chuo walishirikishwa ili kujibu maswali kutokana na malengo ya utafiti huu. Hivyo, sampuli kamili ilikuwa na wanafunzi mia moja (100) wanaojifunza Kiswahili sanifu kama L2 L1 kwao ikiwa Kingwana ambacho ni mojawapo ya lahaja ya Kiswahili itumikayo nchini Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Wanafunzi wote wa darasani walipewa karatasi ambazo 20 ziliandikwa namba 1 hadi 20. Kila mmoja aliokota karatasi na waliookota zenye namba ndio walioshiriki katika utafiti huu. Wanafunzi 100 walichaguliwa na mtafiti kutoka katika wanafunzi 346 kutoka vyuo vikuu tafitiwa, kwani idadi hii ilimhakikishia kupata data tosha. Mchanganuo wa watafitiwa hao ni kama unavyoonyeshwa katika jedwali Na.3.1.

Jedwali Na. 3.1 Mchanganuo wa Watafitiwa

Na.	Jina la chuo	Idadi
1	Chuo Kikuu cha Burundi	20
2	Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika	20
3	Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu	20
4	Chuo Kikuu cha Mwanga cha Bujumbura	20
5	Chuo Kikuu cha Mwaro	20
	JUMLA	100

3.4 Mbinu za Utafiti

Utafiti wowote unalenga kuzua kitu kipya na kuibua uhakika. Kwa hiyo, ni lazima mtafiti azingatie taratibu maalumu au mbinu ambazo zitamsaidia kupata majibu kutokana na malengo ya utafiti na kuufikisha utafiti huo kileleni. Kama anavyosema Kothari(2004), mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa na mtafiti katika kuufanyia kazi utafiti wake. Ziko aina kuu mbili za mbinu za utafiti, yaani mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganua data. “Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti” (Ame, 2017:23), ilhali mbinu za kuchanganua data ni njia au michakato ya kufasiri na kutathmini data zilizokusanywa.

Vilevile, data zinazokusanywa huwa za aina mbili, yaani data za msingi au za awali na data ya upili. Kwa kawaida, data za awali hokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake kulingana na utafiti, na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote. Upande mwingine, data ya upili ni aina ya

data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti (Kothari, 2008). Lengo la data za upili ni kujaliza data za awali ili kusaidia kujibu maswali ya utafiti.

3.4.1 Mbinu za Kukusanyia Data

Katika sehemu hii, kuliwekwa bayana na kujadiliwa mbinu ambazo mtafiti alitumia katika mchakato wa kukusanya data zilizotumika katika utafiti huu. Hivyo, mtafiti alitumia mbinu tatu ambazo zilishirikiana kwa kukamilishana kwa minajili ya kupata taarifa, kuibua ukweli na kujibu maswali ya utafiti huu. Mbinu hizi ni hojaji, ushuhudiaji na mapitio ya nyaraka.

3.4.1.1 Hojaji

Hojaji ni mojawapo ya mbinu za kukusanyia data ambayo mtafiti amenunia kutumia katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Buliba na wenzake (2014: 90), “hojaji ni seti ya maswali au kauli zinazohusiana na swala linalotafitiwa ambayo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa minajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mikabala ya utafiti.”

Naye Kothari (1990), kama alivyonyukuliwa na Ame (2017:17), anasisitiza kuwa hojaji ni “mbinu ya utafiti ambapo mtafiti ameandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani.” Hivyo, kabla ya hojaji kutolewa kwa sampuli ya wasailiwa waliolengwa na utafiti fulani, inatakiwa iandaliwe vizuri hasa kwa kuyafunga au kuyabana maswali ili kipatikane kinachotarajiwa na mtafiti. Hojaji inaweza kuwa ama na maswali funge ambapo msailiwa hufungwiwa maswali kwa

kupewa orodha ya majibu ili achague mojawapo, au maswali wazi ambapo msailiwa huwa na fursa ya kutoa maoni yake na kuyafafanua apendavyo.

Katika utafiti huu, hojaji yenye maswali funge na wazi ilitolewa kwa sampuli ya watafitiwa. Mtafiti aliamua kuitumia hojaji ambayo ina maswali funge ili kupata taarifa inayotarajiwa. Baadhi ya maswali hayo yalikamilika na maswali wazi, ili kuchunguza ukweli wa msailiwa. Hivyo, hojaji yenye maswali funge na wazi ilitumika ili kushadidia matokeo ya njia ya upitiaji wa nyaraka, aghalabu kuhakikisha ukweli wa taarifa zilizopatikana kutokana na njia hiyo ya upitiaji wa nyaraka.

3.4.1.2 Ushuhudiaji

Kama wanavyosema Buliba na wenzake (2014:96), “hii ni ratiba au mpango wa mambo au matukio ambayo mtafiti ananua kuyatazama.” Hii ina maana kuwa, mtafiti mwenyewe anapaswa kushuhudia mambo fulani kuhusiana na utafiti wake. Katika mbinu hii, inawezekana mtafiti akawatazama watafitiwa akiwa anajulikana na kushiriki apendavyo tendo la watafitiwa, au asijulikane. Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumiwa na mtafiti watafitiwa walipokuwa wakiongea wao kwa wao, au wakiongea na mtafiti mwenyewe. Mbinu hii ilitoa fursa kwa mtafiti katika kukusanya makosa ya wanafunzi walipokuwa wakizungumza na kumsaidia pia kupata matini mbalimbali zilizoandikwa na wanafunzi kama mazoezi ya kawaida.

3.4.1.3 Mapitio ya Nyaraka

Katika utafiti huu kulishughulikiwa pia makosa ya kiuandishi ambayo hufanywa na wanafunzi wasailiwa. Hivyo, hii ni mbinu nyingine ambayo mtafiti alitumia hapa katika kiwango hiki cha makosa. Katika kulitekeleza jambo hili, mtafiti alikusanya

data kutoka kazi mbalimbali za maandishi zilizofanywa na wanafunzi, hasa wa mwaka wa pili ambao kwenye somo lao, kuna kozi inayohusu makosa katika lugha. Kazi waliyofanya ilikuwa ni kuandika matini katika Kiswahili sanifu wakijaribu kuepuka dosari kutokana na lahaja yao ya Kingwana.

Kwa hiyo, mbinu ya mapitio ya nyaraka ilitumiwa na mtafiti ili kubaini na kuchanganua makosa katika maandishi ya wanafunzi waliotafitiwa. Mbinu hii ilisaidia katika kutathmini kiwango cha makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kimofosintaksia, hususan makosa ya udondoshaji au ongezeko la viambishi au vipashio fulanifulani katika maneno au tungo za wanafunzi wa Kingwana wajifunzao Kiswahili sanifu.

3.4.2 Mkabala wa Uchanganuzi wa Data

Mkabala wa utafiti ni njia ya kupitia katika utafiti aghalabu katika uchanganuzi wa data. Kwa mujibu wa Walliman (2006), mkabala wa utafiti ni utaratibu ambao mtafiti anateua ili kukusanya na kuchambua taarifa kwa mujibu wa kupata majibu ya maswali aliyojiuliza au kupima mabunio aliyojiwekea kwenye utafiti wake. Hii ina maana kuwa, mtafiti yeyote ana njia moja au zaidi ili “kuufichua ukweli uliofichika na ambao haujavumbuliwa bado” (Kothari, 1985 : 2). Katika utafiti wa kisayansi, hutumika mkabala ama wa kimaelezo au wa kitakwimu, au mchanganyiko wa hii mikabala yote miwili.

Kutokana na data zilizohusika katika utafiti huu ambazo uchanganuzi wake ulilenga kuchunguza makosa ya wanafunzi kwa kutathmini, kuyaainisha na kuchunguza sababu za utokeaji wake, kulihusishwa mchanganyiko wa mikabala ya kimaelezo na

kitakwimu. Upande mmoja, mkabala wa kimaelezo ulihusika kwa sababu ya tukio la data za kiuthamano katika utafiti huu. Upande mwingine, mkabala wa kitakwimu ulihusika na data za kiwingidadi kwa sababu utafiti huu ulihusu uchambuzi wa vipashio au viambajengo vya lugha ya Kiswahili kutokana na malengo ya utafiti huu.

3.5 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2015), “maadili ni mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii au katika kazi.” Naye Mligo (2012) anaeleza kuwa “maadili ni mwenendo mzima wa mwanadamu na tabia yake mahali popote awapo, katika maisha ya kawaida na katika utaalumu unaotumikiwa.” Kwa upande wake, Mukuthuria (2010) anakazia akisema kuwa “maadili ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotungamana nao katika utafiti, uelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa ajili ya binaadamu.”

Kwa hiyo, katika kuutekeleza utafiti huu, baadhi ya maadili yalizingatiwa. Kwanza, mtafiti alinunia kupata kibari cha utafiti. Pili, aliwaelezea watafitiwa wake kile alichokuwa anataka bila kuegemea upande wowote ule katika kuuchakata utafiti huu. Tatu, mtafiti aliheshimu hali za watafitiwa wake ili kuwahamasisha kujibu bila wasiwasi wowote. Mwisho, watafitiwa walikubaliwa kuwa siri zao zitatunzwa na mchango wao utatumika katika utafiti huu tu na si kwingine. Kwa ujumla, mchakato wa kukusanya data ulitokea kwa kuzingatia ruhusa ya watafitiwa.

3.6 Hitimisho

Sura hii imejadili vipengele mbalimbali kuhusiana na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla, imezungumzia eneo la utafiti na watafitiwa, sampuli

lengwa ya watafitiwa na mchakato wa usampulishaji. Kumezungumziwa pia mbinu za kukusanyia data na mkabala wa kuzichanganua data. Sura ifuatayo itajikita katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data zilizopatikana kutokana na mbinu za utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHUNGUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii imezingatia data iliyokusanywa wakati wa utafiti kutoka kwa wanafunzi wa Kingwana (L1) wanaojifunza Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vitano vya Burundi. Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data, mtafiti alitumia nadharia ya UM iliyoasisiwa na Corder (1967). Sura hii inatoa taarifa faafu juu ya ukusanyaji wa data, uainishaji wa makosa kutokana na data iliyokusanywa, uchunguzi wa viwango vya utamalaki wa makosa haya na vyanzo vyake. Mwisho wa sura unahusisha hitimisho la kutamatisha mjadala utakaokuwa umefanyika katika sura hii.

4.2 Uwasilishaji wa Data

Mtafiti alikusanya data zilizotoa taarifa kutoka katika uwanda ulioteuliwa. Data zilizokusanywa zilipatikana kwa njia ya mapitio ya nyaraka, hojaji na ushuhudiaji. Idadi ya wanafunzi waliolengwa na utafiti huu walikuwa mia moja (100) kutoka katika vyuo vikuu vitano. Miongoni mwa wanafunzi hao, wakongo kutoka nchi ya D.R Congo walikuwa 41, ilhali warundi walikuwa 59. Mwanafunzi yeyote aliombwa kutunga matini fupi juu ya mada fulani iliyotolewa. Hivyo, zilipatikana nyaraka mia moja (100). Waliotarajiwa kujibu maswali ya hojaji walitakiwa kuwa haohao, bali walioitika walikuwa 22. Mbinu ya hojaji ilitumiwa ili kushadidia matokeo ya njia ya kwanza ya upitiaji wa nyaraka. Mbinu ya ushuhudiaji ilitumiwa na mtafiti katika kazi za mazungumzo zilizotekelezwa na wanafunzi, akilenga kusikiliza na kupata makosa yanayomjia mwanafunzi moja kwa moja anapozungumza hadharani, na kuyalinganisha na makosa yaliyopatikana kutoka katika nyaraka ili kupata data


kamili. Kuwashirikisha wanafunzi wa Kingwana ambao wanaotoka nchini Burundi na D.R. Congo kulisaidia kubainisha launi tofauti za lahaja ya Kingwana.

Mtafiti alisoma kwa mara ya kwanza nyaraka zote ili kutambua kwa ujumla fikra zilizokuwemo. Baadaye alisoma kwa kina kwa ajili ya kuorodhesha na kukusanya makosa katika makundi tofauti kwa kuzingatia sifa zinazofanana. Kama ilivyoielezwa katika sura ya kwanza (1.6), utafiti huu ulijikita kwenye makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia yanayotokana na mifumo ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia ya Kingwana kuathiri Kiswahili sanifu.

4.3 Aina za Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Lahaja ya Kingwana na Viwango vya Ujitokezaji Wake

Katika sehemu hii, mtafiti alishughulikia malengo ya kwanza na pili ya utafiti huu. Lengo la kwanza ni kubaini aina za makosa ya kisarufi wanayofanya wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu, ilihali lengo la pili ni kutathmini viwango vya ujitokezaji wa aina mbalimbali za makosa hayo. Katika hatua zifuatazo, mtafiti aliainisha makosa yaliyotokea na kutathmini viwango vya ujitokezaji wake akitumia nadharia ya UM kama ilivyoielezwa awali. Uchambuzi wa data ulidhihirisha jumla ya makosa 874 yaliyogawanyika katika aina tatu kuu za makosa, yaani makosa ya kifonolojia, makosa ya kimofolojia na makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia. Aina yoyote miongoni mwa aina hizi tatu iligawanyika katika aina ndogondogo zinazotofautiana ila zikichangia sifa zinazofanana, yaani sifa za kifonolojia, kimofolojia au kisintaksia kwa makosa ya kifonolojia, kimofolojia au kisintaksia na kimofosintaksia. Mchoro Na.4.1 hapa chini unaonyesha kwa ujumla aina kuu za

makosa zilizotambulika na utafiti huu na viwango vya ujitokezaji wa kila aina ya makosa hayo .



Mchoro Na. 4.1 : Aina za Makosa ya Kisarufi na Viwango vya Ujitokezaji wake

Mchoro huu unadhihirisha kwa ujumla aina ya makosa yaliyotokea kwa wanafunzi wa Kingwana wajifunzao Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vya Burundi, na viwango tofauti vya ujitokezaji wa makosa hayo. Makosa ya kifonolojia yalijitokeza kwa kiasi cha 365 kwa 874, sawa na 41.76%. Kwa upande wa makosa ya kimofolojia, haya yalijitokeza kwa kiasi cha 214 kwa 874, sawa na 24.48% ; ilihali makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia yalijitokeza kwa kiasi cha 295 kwa 874, ikiwa ni 33.75%. Kwa ujumla, makosa ya kifonolojia ndiyo yaliyochukua nafasi kubwa, yaani yaliyotokea kwa wingi zaidi, yakifuatwa na makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia ilhali makosa ya kimofolojia yalitokea kwa kiasi kidogo kuliko mengine yote.

Kulingana na tafiti tangulizi mbalimbali zinazoshabihiana na utafiti huu, kuna mambo mawili yaliyotambulika. Kwanza, wanafunzi waongeo Kingwana (L1) hufanya makosa ya kisarufi ambayo baadhi yake yalilandana na matokeo yatafiti tangulizi zilizoshughulikia makosa ya wanafunzi wa L1 zingine wajifunzao Kiswahili sanifu (L2). Kwa mfano, Nyanda (2015), Aruba na wenzake (2017), Mpangala (2018) na Hepkwony (2011) walipotafiti makosa yanayotokea katika matumizi ya Kiswahili (L2) yanayotokana na lugha mbalimbali za jamii (L1) (Kiluo, Kimakonde, Kinyamwezi) walibaini makosa ya kimsamiati, makosa ya kimatamshi, makosa ya kimaana, makosa ya kuunganisha maneno visivyo na makosa ya mrundiko wa maneno katika sentensi. Utafiti huu ulichunguza makosa ya kifonolojia, makosa ya kimofolojia na makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia.

Pili, utafiti huu ulidhihirisha kuwa makosa ya wanafunzi wa Kingwana katika Kiswahili sanifu hayakuwa mengi zaidi ya yaliyotambulika katika tafiti zingine. Hivyo, wakati ambapo utafiti huu ulionyesha jumla ya makosa ya kisarufi 874, Ying (1987) alipochunguza makosa ya kimaandishi ya Wataiwani wanaojifunza Kiingereza, jumla ya makosa 1250 yalipatikana kutoka katika nyaraka 120 za wanafunzi. Naye Kim (1987), utafiti wake juu ya makosa ya wanafunzi wa Kikorea wajifunzao Kiingereza kama L2 ulidhihirisha jumla ya makosa 2455. Pia Kim (1988) utafiti wake juu ya makosa yanayohusiana na nyakati, hali na kauli za vitenzi vya Kiingereza ulidhihirisha jumla ya makosa 2508; ilhali utafiti wake wa mwaka 1989 juu ya makosa ya wanafunzi kutoka Korea wanaojifunza Kiingereza ulidhihirisha makosa 1122. Katika kazi hii, mtafiti anaona kuwa sababu kubwa ya kiasi kidogo cha utokeaji wa makosa kulingana na matokeo ya tafiti tangulizi ni kwamba, utafiti

huu ulishughulikia Kingwana na Kiswahili ambapo Kingwana chenyewe ni lahaja ya Kiswahili, na zote huchangia sifa za kisarufi kwa kiasi kikubwa; ilhali tafiti tangulizi zilizoelezwa hapo juu zilishughulikia lugha kutoka katika jamii lugha zinazotofautiana sana, na ambazo hazina uhusiano wowote. Sehemu zifuatazo zitashughulikia kila kundi la makosa kwa kuonyesha aina ndogondogo za makosa ya kundi hilo, kiasi cha utokeaji wake na kutoa na kujadili mifano yake.

4.3.1 Makosa ya Kifonolojia

Makosa ya kifonolojia hujitokeza katika maandishi au mazungumzo pale ambapo fonimu husika hutumiwa visivyo kwa kudondoshwa, kubadilishana na nyingine au kwa kuzalisha fonimu ambazo kwa usahihi zisingetokea. Hivyo, katika uchunguzi wa aina za makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa Kingwana, makosa ya kifonolojia yalidhihirika kwa kiasi cha makosa 365 yaliyogawanyika katika makundi matatu: udondoshaji wa fonimu, ubadilishanaji wa fonimu na uzalishaji wa fonimu katika mazingira yasiyoruhusika kiisimu. Jedwali Na. 4.1 hapa chini linaonyesha makosa ya kifonolojia na utamalaki wake.

Jedwali Na. 4.1 : Ujitokezaji wa Makosa ya Kifonolojia

Na.	AINA ZA MAKOSA	IDADI YA UTOKEAJI	%
	Jumla	365	100
1	Ubadilishanaji wa Fonimu	104	28.49
2	Uzalishaji wa Fonimu	125	34.24
3	Udondoshaji wa Herufi	136	37.26

Miongoni mwa makosa yote ya kifonolojia, makosa ya udondoshaji wa herufi yalijitokeza kwa kiasi cha 136 kwa 365, sawa na 37.26%. Makosa yanayohusiana na

ubadilishanaji wa fonimu yalijitokeza kwa kiasi cha 104 kwa 365, sawa na 28.49%, ilihali makosa ya uzalishaji wa fonimu yalipatikana kwa kiasi cha 125 kwa 365, sawa na 34.24%.

4.3.1.1 Udondoshaji wa Fonimu

Udondoshaji wa fonimu ulitokea pale ambapo fonimu fulani ya lazima katika Kiswahili sanifu ilidondoshwa kutoka katika maneno inapohusika. Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, jumla ya makosa ya kifonolojia ni 365 ambapo makosa ya udondoshaji ni 136, sawa na 37.26%. Wanafunzi waliotafitiwa walitoa sentensi ambazo zinadhihirisha udondoshaji wa baadhi ya fonimu ambazo ni za lazima. Ifuatayo ni mifano ya sentensi zilizonukuliwa kutoka katika kazi za wanafunzi :

1. (a) *Nimekutana na magari mengi balabalani *ivo* nimefika *apa* chuoni.
→ Nimekutana na magari mengi barabarani, hata *hivyo* nimefika *hapa* chuoni
- (b) *Safari yangu leo *imekua* nzuri sana.
→ Leo safari yangu *imekuwa* nzuri sana.
- (c) *Nimekutana na rafiki yangu *ambae* tunasoma *nae*.
→ Nimekutana na rafiki yangu *ambaye* tunasoma *naye*.

Jedwali Na.4.2 linatoa mifano zaidi ya maneno yaliyodondoshwa fonimu fulani fulani. Kosa lolote limelinganishwa na neno sahihi la Kiswahili sanifu.

Jedwali Na. 4.2 : Udondoshaji wa Herufi

Na.	Kosa	Sahihi
1	apa	hapa
2	ivi	hivi
3	atukufanya	hatukufanya
4	apo	hapo
5	asubui	asubuhi
6	ame ubiri	amehubiri
7	awajiwezi	hawajiwezi
8	kuusu	kuhusu
9	alafu	halafu
10	maali	mahali
11	nae	naye
12	ambae	ambaye
13	imekua	imekuwa
14	iliojitokeza	iliyojitokeza
15	mda	muda

Jedwali Na.4.2 linaonyesha kuwa wanafunzi walidondosha baadhi ya fonimu kutoka kwenye baadhi ya maneno walipokuwa wanaandika au kuzungumza Kiswahili sanifu. Kwa mfano, katika maneno Na.1 (**apa*><*hapa*), 2(**atukufanya*><*hatukufanya*) na 10 (**kuusu*><*kuhusu*) kumedondoshwa fonimu /h/. Aidha, katika Na. 11, 12, 13, 14, na 15 fonimu /y/, /w/ na /u/ zilidondoshwa kutoka katika maneno *naye* (**nae*), *ambaye* (**ambae*), *kuwa* (**kua*), *iliyojitokeza* (**iliojitokeza*) na *muda* (**mda*).

4.3.1.2 Ubadilishanaji wa Fonimu

Kwa kiasi kikubwa, fonimu za Kiswahili huwa zilezile zinazohusika katika lugha za kibantu zilizoko katika maeneo kunakozungumzwa lahaja ya Kingwana. Ufanano huo unasababisha hali ya ubadilishanaji wa fonimu hivi kwamba baadhi ya maneno asili ya Kiswahili hutamkwa na kuandikwa kwa namna tofauti. Makosa ya aina hii yalitokea mara 104 kati ya jumla ya makosa 365; sawa na 28.49%. Baadhiya sentensi zilizonukuliwa kutoka nyaraka na mazungumzo ya wanafunzi hudhihirisha ubadilishanaji wa fonimu katika maneno:

2. (a) *Nimekutana na *magali* mengi *balabalani* ivo nimefika apa chuoni.

→ Nilipokuwa *barabarani*, nimekutana na *magari* mengi; hivyo ndivyo nilivyofika hapa chuoni

(b) *Kufikisha muda huu nimevumiliya na kusikiliza *mwarimu*.

→ Hadi sasa, nimevumilia nikimsikiliza *mwalimu*.

(c) *Nimepiga chayi.

→ Nimepika chai.

(d) *Padri akaingiya *kicha* akaanza mafundisho.

→ Padri akaingia *kisha* akaanza mahubiri.

Jedwali Na. 4.3 hapa chini linatoa mifano zaidi ya ubadilishanaji wa fonimu unaojitokeza waswahili wa Kingwana waandikapo au kuzungumza Kiswahili sanifu.

Jedwali Na. 4.3 : Ubadilishanaji wa Fonimu

Na.	Kosa	Sahihi
1	magali	magari
2	balabalani	barabarani
3	nilijitayalisha	nilijitayarisha
4	mwarimu	mwalimu
5	vyashure	vya shule
6	ni mepiga	nimepika
7	gusoma	kusoma
8	gukojoa	kukojoa
9	nimechika	nimeshika
10	kicha	kisha
11	bangu	wangu
12	syafika/ siyafika	sijafika
13	hadisi	hadithi
14	visuri	vizuri
15	kuya	kuja

Jedwali Na.4.3 hapo juu linatoa mwanga juu ya maneno ambayo fonimu fulanifulani zimebadilishana. Kwanza, katika maneno Na. 1 (*magali><magari), 2 (*balabalani><barabarani), 4 (*mwarimu><mwalimu) na 5 (*shure><shule) kumbainika ubadilishanaji wa fonimu /l/ na /r/. Pili, katika 7 (*gusoma><kusoma) na 8 (*gukojoa><kukojoa) kumetokea ubadilishanaji wa fonimu /k/ na /g/. Tatu, wanafunzi walitumia /f/ (ch) badala ya /ʃ/ (sh) (*kicha><kisha), /j/ badala ya /ʒ/ (*siyafika><sijafika), (*kukuya><kuja), /s/ badala ya /θ/ (*hadisi><hadithi) na /s/ badala ya /z/ (*visuri><vizuri).

4.3.1.3 Uzalishaji wa Fonimu katika Mazingira Yasiyoruhusika Kiisimu

Kwa muda mrefu, lahaja ya Kingwana iliathiriwa na lugha za kijamii zinazopakana nayo kama vile Kishi, Kibembe, Lingala, Kirundi, Kinyarwanda, n.k., hali ambayo iliisababisha kuathiriwa kifonolojia na mifumo ya kimatamshi ya lugha hizo. Hivyo, mfuatano wa fonimu usio sawa katika Kingwana na Kiswahili sanifu kulisababisha mchanganyiko wa fonimu na uzalishaji wa fonimu ambazo zisingetokea wanafunzi wanapotumia Kiswahili sanifu. Makosa yanayohusiana na uzalishaji wa fonimu katika mazingira yasiyofaa yalitokea kwa kiasi cha 125 kwa jumla ya makosa ya kifonolojia 365; sawa na 34.24%. Sentensi zifuatazo ni mifano iliyotoka katika kazi za wanafunzi.

3. (a) **Akaniambiya* mwanangu usiache masomo.

→ *Akaniambia*: mwanangu usiache shule.

(b) *...*kujuwa* namna *yakutatuuwa* tatizo fulani fulani.

...*kujua* namna ya *kutatua* matatizo fulanifulani.

(c) **Nimeamuka* asubuhi mapema sana nikajiandaa ili niende.

→ *Nimeamka* asubuhi mapema sana nikajiandaa kwenda/ kuondoka.

(d) **Nilikuta* bado wanafunzi wapo *inje*.

→ *Niliona* bado wanafunzi wapo *nje*.

Pamoja na mifano iliyotolewa katika tungo hizo hapo juu, jedwali Na. 4.4 linatoa mifano zaidi ya maneno ambayo wanafunzi walihusisha uzalishaji wa fonimu ambazo zisingetokea katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Jedwali Na. 4.4: Uzalishaji wa Fonimu Usio Sahihi

Na.	Kosa	Sahihi
1	akaniambi <u>y</u> a	akaniambia
2	tulionge <u>y</u> a	tuliongea
3	pi <u>y</u> a	Pia
4	kuj <u>u</u> wa	kujua
5	mu <u>t</u> u	mtu
6	nimeamu <u>k</u> a	nimeamka
7	nimeham <u>k</u> a	nimeamka
8	i <u>n</u> ne	nne
9	i <u>n</u> chi	nchi
10	i <u>n</u> je	nje
11	nimeva <u>l</u> a	nimevaa
12	tuka <u>h</u> anza	tukaanza
13	yakutatu <u>w</u> a	ya kutatua
14	alioni <u>l</u> am <u>u</u> sha	aliyeniamsha
15	amemkatar <u>a</u>	amemkataa

Kutokana na jedwali Na. 4.4 hapo juu, baadhi ya maneno yaliongezewa fonimu. Katika baadhi ya maneno, kati ya irabu moja na nyingine kumezalishwa kasonanti fulani (*Akaniambiya >< Akaniambia, *amemkatara >< amemkataa, *alionilamusha >< aliyeniamsha). Katika maneno Na. 5 na 6 kulizalishwa irabu /u/ baina ya konsonanti halisi mbili /m/ na /t/ (mtu><*mutu), au /m/ na /k/ (Nimeamka><*Nimeamuka). Upande mwingine, kulijitokeza fonimu /i/ kwenye maneno nje, nne na nchi.

Kutokana na maelezo na idadi hapo juu, imedhihirika kuwa viwango vya ujitokezaji wa makosa ya kifonolojia yaliyotambulika vilitofautiana kutokana na kila aina.

Katika jedwali Na. 4.1 imedhihirika kuwa, miongoni mwa makosa ya kifonolojia, yaliyotokea kwa kiasi kikubwa ni makosa ya udondoshaji wa herufi (37.26%), yakifuatwa na makosa ya uzalishaji wa fonimu (34.24%) ambayo nayo yalifuatwa na makosa ya ubadilishanaji wa fonimu (28.49%).

Ni dhahiri pia kuwa makosa hayo yote yalitokea kwa kiasi kikubwa, kwani aina hizi tatu za makosa hazikutengana sana kiidadi; tofauti kubwa inalingana na kiasi cha 8.77%. Kutokea kwa makosa ya udondoshaji kwa kiasi kikubwa kumetokana na hali kwamba zipo fonimu ambazo hudondoshwa katika Kingwana zikilazimika katika Kiswahili sanifu. Mfano wake ni /h/ popote inapotokea na /w/ ikitokea baina ya irabu mbili. Hivyo, kama inavyoonekana katika jedwali la makosa ya kifonolojia kwenye viambatanisho, makosa ya udondoshaji wa /h/ yalitokea kwa kiasi cha 71 kwa jumla ya makosa ya udondoshaji 127.

Makosa ya uzalishaji wa fonimu yalitokea kwa kiasi kikubwa kwa sababu kunakotokea (i) mfuatano wa irabu katika neno moja katika Kiswahili sanifu, Kingwana hulazimisha kutokea kwa konsonanti baina ya irabu hizo, ilhali (ii) baina ya konsonanti halisi zinazofuatana hupachikwa irabu, kwani Kingwana huhakikisha kutokea kwa muundo wa silabi wa KI. Hivyo, kupachikwa kwa konsonanti au irabu katika mfuatano wa irabu au konsonanti halisi za neno moja kulitokea mara 109 kati ya jumla ya makosa ya uzalishaji 119; ilihali makosa 16 kwa 119 yalitokana na kudhoofika kwa /n'/ ikipachikwa irabu ya mwanzo katika maneno kama “nne” (inne) “nchi” (inchi) na “nje” (inje) na uzalishaji wa fonimu /h/ mwanzoni mwa baadhi ya maneno (mf. *helimu >< elimu).

Makosa ya ubadilishanaji wa fonimu nayo yalitokana na kutokuwepo kwa baadhi ya fonimu za Kiswahili sanifu katika Kingwana na utata wa kimatumizi baina ya fonimu fulani. Hivyo, kwa mfano, kutotumika kwa fonimu /θ/, /ð/ na /ɣ/ katika Kingwana kuliwafanya watafitiwa kuziwakilisha na fonimu /s/, /z/ na /g/. Aidha, utata wa kimatumizi baina ya /l/ na /r/ umetokana na hali kwamba baadhi ya launi za Kingwana hutumia ama /l/ au /r/, au zote kutokana na athari za lugha zinazozungumzwa katika maeneo kinakotumiwa. Kwa mfano ubadilishanaji wa /l/ na /r/ ulitokea mara 51 kati ya jumla ya makosa 100 ya ubadilishaji wa fonimu.

Kulingana na kazi tangulizi zilizoshughulikia makosa au athari za kifonolojia, ni dhahiri kuwa utafiti huu unashabihiana kwa kiasi fulani na kazi tangulizi zilizoshughulikia makosa ya kifonolojia yanayotokana na L1 ya mwanafunzi. Kwa mfano, Aruba na wenzake (2017), waliona kuwa wanafunzi wa shule za upili hubadilishana kitambaza /l/ na kimandende /r/, fonimu /v/ na /f/ na /ʃ/ na /tʃ/ (*mahari><mahali, *yutahi ><futahi, *jini ><chini) kutokana na athari za L1 zao, na hivyo kubadili au kuharibu maana iliyokusudiwa. Vilevile, Niyomugabo (2019), alibaini matumizi ya kimandende /r/ badala ya kitambaza /l/ katika Kiswahili kwa wanafunzi wa Rwanda kwa sababu ya Kinyarwanda kuhusisha /r/ kwa kiasi kikubwa, /l/ ikihusika katika neno “Kigali” na maneno mkopo tu. Pia, alitambua matumizi ya fonimu asili za Kinyarwanda badala ya fonimu asili za Kiswahili zisizopatikana katika Kinyarwanda kama vile /t/, /f/ au /s/ badala ya /θ/ (*telatini, *felafini, *selasini><thelathini), /g/ au /h/ badala ya /ɣ/ (*luga, *luha><lugha); /d/ au /z/ badala ya /ð/ (*dambi, *zambi><dhambi). Hali sawa na hii ndiyo iliyotambulika na Ame (2017) alipotafiti athari za Kitumbatu katika Kiswahili sanifu kinachotumika

katika shule za Tumbatu Zanzibar. Tafiti hizi, tofauti na utafiti huu, hazikushughulikia ujitokezaji wa makosa haya ya kifonolojia yaliyotambulika.

4.3.2 Makosa ya Kimofolojia

Makosa ya kimofolojia huwa ni yale yaliyotokana na utumiaji usio sahihi wa mofu au viambishi katika maneno. Kutokana na uchunguzi huu, makosa ya kimofolojia yalitambulika kwa kiasi cha makosa 214 yanayogawanyika katika makundi matatu: udondoshaji wa viambishi vinavyohitajika, makosa ya ongezeko la viambishi kimakosa na matumizi ya viambishi visivyokubalika. Jedwali na.4.5 linaonyesha namna makosa haya yalivyotamalaki.

Jedwali Na. 4.5 : Ujitokezaji wa Makosa ya Kimofolojia

Na.	AINA ZA MAKOSA	IDADI YA UTOKEAJI	%
	Jumla	214	100
1	Matumizi ya Viambishi Kimakosa	124	57.94
2	Udondoshaji wa Viambishi Vinavyohitajika	53	24.76
3	Ongezeko la Viambishi Kimakosa	37	17.28

Jedwali Na. 4.5 hapa juu linaonyesha kuwa makosa ya kimofolojia yalitokea kwa kiasi cha makosa 214. Miongoni mwa makosa hayo, makosa ya udondoshaji wa viambishi vinavyohitajika yalidhihirika kwa kiasi cha 53 kwa 214, sawa na 24.76%. Makosa yanayotokana na ongezeko la viambishi kimakosa yalitokea kwa kiasi cha 37 kwa 214, sawa na 17.28 %, ilhali makosa ya matumizi ya viambishi kimakosa yalitokea kwa kiasi cha 124 kwa 214, sawa na 57.94%.

4.3.2.1 Udondoshaji wa Viambishi Vinavyohitajika

Udondoshaji wa viambishi ulitokea pale ambapo kiambishi fulani kiliondolewa au kilidondoshwa kutoka katika neno fulani. Utafiti huu ulidhihirisha kiasi cha makosa 53 ya udondoshaji wa viambishi vinavyofaa kwa jumla ya makosa ya kimofolojia 214; yaani 24.76%. Ifuatayo ni mifano mbalimbali ya sentensi zilizotungwa na wanafunzi zidhihirishazo makosa ya aina hiyo:

4. (a) *Wakati *tulifika* pande la soko ya COTEBU...

→ Wakati *tulipofika* karibu na soko la COTEBU...

(a) *Niliwasalimia *rafiki* zangu.

→ Niliwasalimia *marafiki* zangu.

(a) *Elimu inatusaidia *kuweza ichi* na watu.

→ Elimu inatuwezesha *kuiishi* pamoja na watu wengine.

Jedwali Na.4.6 hapa chini linatoa mifano zaidi juu ya udondoshaji wa viambishi ambavyo vingekuwepo katika Kiswahili sanifu.

Jedwali Na. 4.6 : Udondoshaji wa Viambishi Vinavyohitajika

Na.	Kosa	Sahihi
1	wakati <i>tulifika</i>	wakati <i>tulipofika</i>
2	mtu <i>aliumia</i>	mtu <i>aliyeumia</i>
3	<i>rafiki</i> zangu	<i>marafiki</i> zangu
4	<i>kuweza ichi</i>	inatuwezesha <i>kuishi</i>
5	hajawahi <i>elimika</i>	hajawahi <i>kuelimika</i>
6	wakati <i>tulimaliza</i>	wakati <i>tulipomaliza</i>
7	Si	Usio
8	uzima <i>alitupa</i>	uzima <i>aliotupa</i>
9	Nifika	Nilifika
10	<i>Maisha</i> mwetu	<i>Maishanimwetu</i>
11	mtaa <i>moja</i>	mtaa <i>mmoja</i>
12	siwezi <i>weza eleza</i>	siwezi (<i>kuweza</i>) <i>kueleza</i>
13	nikaenda <i>nawa</i>	nikaenda <i>kunawa</i>
14	<i>lengo zetu</i>	<i>malengo yetu</i>
15	<i>wana fikiria</i>	<i>Wanaofikiria</i>

Jedwali hili linaonyesha maneno tofauti yaliyokosa viambishi katika virai au vishazi ambavyo uwiano wake ungelidhihirishwa na viambishi hivyo. Kwa mfano, katika vishazi Na. 1 na 2 viambishi rejeshi {-po-} na {-ye-} vilidondoshwa kutoka katikavitenzi (**tulifika*>< *tulipofika*, **aliumia*>< *aliyeumia*). Kuhusu virai Na. 3 na 14 kulidondoshwa viambishi vya wingi kutoka katika nomino husika (**rafiki*>< *marafiki*, **lengo*>< *malengo*). Mfano mwingine unahusu Na. 4 na 5 ambapo kiambishi *ku-* kilidondoshwa kutoka katika vitenzi *kuishi* na *kuelimika* (*kuweza* **ichi*>< *kuwezakuishi*, *hajawahi* **elimika*>< *hajawahi kuelimika*).

4.3.2.2 Ongezeko la Viambishi Kimakosa

Makosa ya ongezeko la viambishi yalitokea pale ambapo wanafunzi walipachika viambishi au mofu ambazo kwa kawaida zisingelikuwepo katika muktadha husika. Makosa ya aina hii yalijitokeza mara 37 kati ya jumla ya makosa ya kimofolojia 214 sawa na 17.28%. Sentensi zifuatazo zinadhihirisha makosa ya aina hii.

5. (a) *Niliamka *nikakula*.

→ Niliamka, *nikala*.

(b) *Usiache masomo ili *usikuwe* kama mimi.

→ Usiachane na kisomo ili *usiwe* kama mimi.

(c) *Hio siku *ilikuwaga* siku ya shangwe kweli.

→ Hiyo siku *ilikuwa* siku ya shangwe kweli.

(d) *Ata *wa mama, wababa, wakaka, wadada* wanaitaji kuwa na elimu.

→ Hata (*akina*)*mama, baba, kaka na dada* wanahitajikuelimika.

Jedwali Na. 4.7 hapa chini linaonyesha mifano zaidi ya makosa yanayohusiana na kuongeza viambishi katika maneno mbalimbali.

Jedwali Na. 4.7 : Ongezeko la Viambishi Kimakosa

Na.	Kosa	Sahihi
1	nikak <u>u</u> la	nikala
2	usiku <u>u</u> we	usiwe
3	tukaku <u>u</u> ya	tukaja
4	ilikuw <u>a</u> ga	ilikuwa
5	balichez <u>a</u> ga	walicheza
6	<u>w</u> a mama	(akina) mama
7	<u>w</u> a baba	(akina) baba
8	<u>w</u> a kaka	(akina) kaka
9	<u>w</u> a dada	(akina) dada
10	wajamani <u>b</u> angu	jamaa <u>z</u> angu
11	nik <u>i</u> maliza nika <u>a</u> enda	nilipomaliza nilienda
12	mjini <u>w</u> a Bujumbura	mjini Bujumbura
13	wali <u>y</u> o shiriki	walio <u>sh</u> iriki
14	<u>m</u> a nyumbani kwetu	nyumbani kwetu

Jedwali Na.4.7 hapo juu linaonyesha maneno kadhaa ambayo yaliongezewa viambishi visivyohitajika katika Kiswahili sanifu. Katika maneno Na. 1, 2 na 3 kiambishi {-ku-} kilipachikwa katika vitenzi vyenye silabi moja *kula* (*nikakula><nikala), kuwa (usikuuwe><usiwe) na kuya (kuja) (tukakuuya><tukaja). Pia, katika mifano Na. 4 na 5 kiambishi {-ag-}kiliongezwakwenye mzizi wa kitenzi(*ilikuwaga><ilikuwa, *balichezaga><walicheza). Upande mwingine, viambishi ngeli, hasa vya wingi, vilipachikwa katika nomino ambazo zingelipata viambishi kapa visivyodhihirika kifonolojia. Hili lilijitokeza kama katika maneno Na. 6 (*wa mama><mama), 7 (*wa baba><baba), 10 (*wajamani><jamani), 14 (*manyumbani><nyumbani) n.k.

4.3.2.3 Matumizi ya Viambishi Kimakosa

Katika kazi zilizotekelezwa na wanafunzi kulitokea makosa yanayohusiana na matumizi ya viambishi kimakosa. Makosa ya aina hii yalijitokeza mara 124 kati ya jumla ya makosa ya kimofolojia 214, sawa na 57.94 %. Viambishi husika hapa ni pamoja na vipatanishi baina ya nomino na vitenzi au nomino na vivumishi katika kirai nomino. Pia, alama za nyakati zilitumika kwa kubadilishana hivi kwamba kulifananishwa wakati uliopita na hali timilifu au wakati uliopita muda kidogo. Mifano ifuatayo inadhihirisha hilo :

6. (a) *Banafunzi benye balifika mapema awakuchelewa.
→ Wanafunzi waliofika mapema hwakuchelewa.
- (b) *Asubuhi ya leo nilitoka nyumbani saa moja na dakika hamsini na tano.
→ Asubuhi ya leo nimetoka nyumbani saa 1:55.
- (c) *Nikimaliza nikaenda kuchunga gari la kunileta mjini.
→ Nilipomaliza nilienda kusubiria gari la kunipeleka mjini.

Jedwali Na.4.8 linatoa mifano zaidi ya makosa ya matumizi ya viambishi.

Jedwali Na. 4.8 : Matumizi ya Viambishi Kimakosa

Na.	Kosa	Sahihi
1	<u>b</u> anafunzi	w <u>a</u> nanafunzi
2	<u>b</u> enye <u>b</u> alifika	w <u>a</u> liofika
3	<u>a</u> wakuchelewa	<u>h</u> wakuchelewa
4	<u>b</u> achache	w <u>a</u> chache
5	<u>b</u> akashuka	w <u>a</u> akashuka
6	<u>b</u> engine	w <u>e</u> ngine
7	<u>b</u> akaingia	w <u>a</u> kaingia
8	mambo <u>m</u> ingi	mambo <u>m</u> engi
9	<u>b</u> ako	w <u>a</u> ko
10	<u>b</u> anaelekea	w <u>a</u> naelekea
11	<u>n</u> ilitoka	<u>n</u> imetoka
12	<u>t</u> ulisoma	<u>t</u> umesoma
13	<u>n</u> ikimaliza	<u>n</u> ilipomaliza
14	<u>n</u> ikaenda	<u>n</u> ilienda

Jedwali hili linaonyesha kuwa katika kifungutenzi, baadhi ya wanafunzi walitumia kiambishi ngeli {ba-}badala ya {wa-} kama katika Na. 2 (*benyebalifika><waliofika) na Na. 5 (*bakashuka><wakashuka). Aidha, katika maneno Na. 4 na 6 kiambishi kipatanishi cha nomino na kivumishi {wa-}kiliwakilishwa na {ba-}(*bachache><wachache, *bengine><wengine). Upande mwingine, kiambishi cha wakati uliopita {-li-} kilitumiwa badala ya kiambishi {-me-} cha wakati uliopita muda kidogo au hali timilifu (*nilitoka><nimetoka). Katika mfano mwingine mifano inaonyesha kuwa kiambishi cha hali ya mfururizo wa matendo {-ka-} kilitumika badala ya {-li-} kuonyesha wakati uliopita

(**nikaenda*><*nilienda*). Mfano Na. 14 umedhihirisha matumizi yasiyofaa ya kiambishi cha hali ya masharti ya wakati ujao {-ki-} (**Nikimaliza*><*nilipomaliza*). Kutokana na maelezo hapo juu, makosa ya kimofolojia yaligawanyika katika aina tatu ambazo viwango vyake vya utamalaki hutofautiana. Makosa kutokana na matumizi ya viambishi kimakosa ndiyo yaliyojitokeza kwa kiasi kikubwa (57.95%), yakifuatwa na makosa ya udondoshaji wa viambishi vinavyohitajika (24.76%) na yale yanayotokana na ongezeko la viambishi kimakosa (17.28%). Aidha, kukizingatiwa jumla ya makoza ya aina zote, ni dhahiri kuwa makosa ya kimofolojia yalitamalaki kwa kiasi kisicho kidogo kutokana na sababu mbalimbali.

Makosa ya matumizi ya viambishi kimakosa ndiyo yaliyotokea kwa kiasi kikubwa zaidi ya makosa mengine ya kimofolojia. Sababu tatu muhimu zimeongoza tukio hili. Kwanza, athari za Kingwana kutokana na uzoefu wa wazungumzaji na utata walio nao kutokana na ujuzi duni kubainisha mifumo ya kisarufi ya Kingwana na Kiswahili sanifu. Hivyo, matumizi ya kiambishi kipatanishi {wa-} (a-wa) au kiambishi ngeli {wa-} (m-wa) kiliwakilishwa na kiambishi cha Kingwana {ba-} ; na maneno yote 22 ambayo yanahusisha kiambishi {wa-} yalipachikwa {ba-} (mf. baimbaji, bachache, bengine, bakaingia, bako banaelekea) badala ya {wa-} (mf. waimbaji, wachache, wengine, wakaingia, wako wanaelekea). Aidha, matumizi ya mofu njeo za wakati uliopita sana na wakati uliopita muda kidogo huzusha utata kwa wanafunzi baada ya kusoma Kiswahili sanifu. Kwa kawaida, launi ya Kingwana itumikayo nchini Burundi inatumia mofu {-me-} kwa ama wakati uliopita sana au wakati uliopita muda kidogo, au kwa hali timilifu. Upande mwingine, launi nyingine itumikayo nchini D.R Congo inadhihirisha matumizi ya {-ka-} badala ya {-li-}. Watafitiwa

walionyensha mkanganyiko kwa kubadilishana {-me-} na {-li-}, {-ka-} na {-li-} au {-me-}, na {-ki-} na {-lipo-}, na makosa 45 yalitokea kutokana na hali hii.

Kuhusu makosa ya udondoshaji wa viambishi vinavyohitajika, viambishi rejeshi (mf.: {-po-}, {-ye-}), viambishi ngeli vya nomino (*rafiki><marafiki, *lengo><malengo) na kiambishi {ku-} ndivyo vilivyodondoka kwa kiasi kikubwa. Kwanza, hali hii ilitokana na athari ya Kingwana kutohusisha virejeshi kutokana na athari za lugha ya Kirundi na Kinyarwanda, ambazo ni lugha za toni ambazo urejeshi huwakilishwa na toni. Pili, udondoshaji wa viambishi ngeli kutoka katika nomino ulitokana na athari za Kingwana kuhusisha ngeli ya I-ZI badala ya ngeli zozote. Hivyo, nomino *marafiki* ya A-WAna nomino *malengo* ya LI-YA ziliondolewa kiambishi cha wingi {ma-}na kuingizwa katika ngeli ya I-ZI. Kwa sababu hiyo, vivumishi vilivyoshirikiana na nomino hizi vimeambikwa viambishi ngeli kutokana na ngeli ya I-ZI. Tatu, udondoshaji wa kiambishi {ku-} kutoka katika vitenzi (kuweza *ichi >< kuweza kuishi, hajawahi *elimika><hajawahi kuelimika) kulitokana na wazungumzaji wa Kingwana kudondosha kiambishi hicho kutoka katika kitenzi kikuu kinapotumika sambamba na kitenzi kisaidizi. Hivyo, kudondoka kwa kiambishi hicho wanafunzi wanapotumia Kiswahili sanifu huwa ni athari ya Kingwana.

Makosa ya ongezeko la viambishi kimakosa yalitokana na sababu muhimu tatu. Kwanza, hali ya kwamba nomino ya Kingwana hulazimika kupata kiambishi awali kinachodhihirika, hususan pale ambapo Kiswahili sanifu huhusisha kiambishi awali kapa. Hivyo, nomino kama vile “shule”, “lugha”, “idara”, “nyumba”, “dada”, “kaka”, “jamaa”, n.k. zilipachikwa kiambishi ngeli {ma-} (“mashule”, “malugha”,

“maidara”, “manyumba”, “wadada”, “wakaka”, “wajamaa”, n.k). Pili, kawaida ya utokeaji wa kiambishi {-ku-} katika vitenzi vyenye silabi moja kama vile *kula* (*nikakula><nikala), kuwa (*usikuuwe><usiwe) na kuya (kuja) (*tukakuya><tukaja) ilidokeza athari za Kingwana katika Kiswahili sanifu. Tatu, utokeaji wa kiambishi cha Kingwana {-ag-} cha hali ya kuendelea kwa tendo (Nshimirimana, 2019:19) au hali ya mazoea (Sarah, 2019: 137) kwenye mzizi wa kitenzi katika matumizi ya Kiswahili sanifu kunadhirisha athari za Kingwana katika Kiswahili sanifu (*ilikuuaga><ilikuwa, *balichezauga><walicheza).

Baadhi ya tafiti tangulizi zilizoshughulikia makosa ya kimofolojia kutokana na athari ya L1 zina ufanano wa aina fulani na utafiti huu. Kwa mfano, Sarah (2019) aligundua kuwa wanafunzi wa jamii ya Wairaki wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya upachikaji wa viambishi visivyostahili katika maneno. Kiambishi {-ag-} au {-ga} kilipachikwa kwenye mzizi wa kitenzi kikieleza hali ya mazoea (*hawafanyagi><huwa hawafanyi, *napataga><huwa ninapata). Vilevile, nomino za Kiswahili zisizoweza kubeba kiambishi cha wingi zilipachikwa kiambishi cha wingi {ma-} (*madada><dada, *makaka><kaka, *makelele><kelele). Mtafiti huu aligundua pia dosari za udondoshaji wa viambishi yambwa. Naye Mushumbwa (2020) alibainisha makosa ya udondoshaji wa mofu (*tajiunga><atajiunga) au uchopekaji wa mofu zisizostahili katika maneno (msemaji *huo><huyo, shirika *ingetengeneza><lingetengeneza). Ufanano uliopo baina ya tafiti tangulizi hizi na huu ni kutambua aina za makosa ya kimofolojia, ilhali tofauti inatokana na hali kwamba kazi hizi hazikupa kipau mbele kiasi cha utokeaji wa makosa yaliyotambulika.

4.3.3 Makosa ya Kisintaksia na Kimofosintaksia

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009:34), “sintaksia ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake.” Kwa mantiki hii, kuna kanuni zinazofuatwa katika kuyapanga maneno, moja baada ya jingine, katika tungo au sentensi ili yalete maana inayokusudiwa na kukubalika katika lugha husika. Hivyo, katika sehemu hii kumewasilishwa na kujadiliwa makosa yanayoathiri muundo wa tungo au sentensi. Makosa haya yalibusu upatanisho wa kisarufi, viambishi tegemezi vilivyogeuka na kuwa maneno, kukata na kuunganisha maneno kinyume na kanuni. Jumla ya makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia yaliyotambulika na utafiti huu ni 296 na mgawanyiko wake ni kama unavyooneshwa na jedwali Na. 4.9 hapa chini.

Jedwali Na. 4.9 : Ujitokezaji wa Makosa ya Kisintaksia na Kimofosintaksia

Na.	AINA ZA MAKOSA	IDADI YA UTOKEAJI	%
	Jumla	295	100
1	Kukata Maneno Visivyo	120	40.67
2	Upatanisho kati ya Nomino na Kitenzi	32	10.81
3	Kuunganisha Maneno Visivyo	33	11.18
4	Upatanisho kati ya Nomino na Kivumishi	63	20.94
5	Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno	47	15.93

Jedwali Na. 4.9 hapo juu linaonyesha ni kwa kiasi gani utamalaki wa makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia yalitokea. Hivyo, makosa ya upatanisho kati ya nomino na kitenzi yamejitokeza kwa kiasi cha 32 kwa 295, sawa na 10.81%, ilihali makosa ya upatanisho kati ya nomino na kivumishi yalitokea kwa kiasi cha 63 kwa

295, sawa na 20.94%. Kwa ujumla makosa ya upatanisho wa kisarufi yalijitokeza kwa kiasi cha 95 kwa 295, sawa na 32.20%. Makosa ya ugeukaji wa viambishi tegemezi kuwa neno yalijitokeza kwa kiasi cha 47 kwa 295, sawa na 15.93%. Makosa ya uunganishaji wa maneno na mengine yalijitokeza kwa kiasi cha 33 kwa 295, sawa na 11.18%, ilhali makosa ya kukata maneno visivyo yalitokea kwa kiasi cha 120 kwa 295, sawa na 40.67%. Hapa chini ni uwasilisho wa kina kuhusu aina hizi za makosa.

4.3.3.1 Upatanisho wa Kisarufi Usiokubalika

Upatanisho wa kisarufi ni mbinu ya kuoanisha maneno ili yawiane vizuri. Katika lugha yoyote ile, kuna namna maneno yanavyofuatana katika tungo hali kwamba yanashirikiana kwa kupatana. Upatanisho huu hudhihirishwa na viambishi ngeli vinavyounganisha maneno husika kutokana na nomino husika. Makosa ya upatanisho wa kisarufi ya aina mbili tofauti yalitokea katika insha zilizotungwa na wanafunzi kwa kiasi cha makosa 95 kati ya jumla ya makosa yote ya kisintaksia (296), sawa na 32.20%.

4.3.3.1.1 Makosa katika Upatanisho kati ya Nomino na Kitenzi

Nomino na kitenzi vinaposhirikiana, vipo viambishi ngeli ambavyo hudhihirisha upatanisho wa kisarufi, hivi kwamba maneno hayo huwiana ili kutoa ujumbe kamili unaokusudiwa. Makosa haya ya upatanisho kati ya nomino na kitenzi yalijitokeza kwa kiasi cha makosa 32 kwa 296, yaani 10.81%. Sentensi zifuatazo ni mifano iliyotoka katika kazi za wanafunzi :

7. (a) *Gali *ikanifikisha* mjini.

→ Gari *likanifikisha* mjini.

(b) *Mahubiri ilipofika mwisho, tulimuabudu tena Mungu kwa nyimbo.

→ *Mahubiri yalipofika mwisho (...) → Mahubiri yalipoisha, (sahihi)

(c) *Simba iliuliwa na askari polisi.

→ Simba aliuliwa na askari polisi.

(d) *Kazi yake tangu aliezaliwa ni kufuga.

→ Kufuga ndiko kazi yake tangu alipozaliwa.

Mifano zaidi ya makosa ya upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kitenzi imetolewa na kulinganishwa na yaliyo sahihi katika jendwali Na. 4.9 hapa chini :

Jedwali Na. 4.10 : Upatanisho kati ya Nomino na Kitenzi

Na.	Kosa	Sahihi
1	gali <u>ikanifikisha</u>	gari <u>likanifikisha</u>
2	mahubiri <u>ilipofika</u>	mahubiri <u>yalipofika</u>
3	kabila <u>ina</u>	kabila <u>lina</u>
4	simba <u>iliuliwa</u>	simba <u>aliuliwa</u>
5	nguruwe <u>zinaishi</u>	nguruwe <u>wanaishi</u>
6	elimu <u>unasaidia</u>	elimu <u>inasaidia</u>
7	elimu <u>atufungulia</u>	elimu <u>inatufungulia</u>
8	elimu <u>lina</u>	elimu <u>ina</u>
9	tangu <u>aliezaliwa</u>	tangu <u>alipozaliwa</u>
10	watu wali <u>elimika</u>	watu wali <u>olimika</u>
11	elimu <u>linasaidia</u>	elimu <u>inasaidia</u>
12	<u>kitu</u> ambacho <u>inasaidia</u>	<u>kitu</u> ambacho <u>kinasaidia</u>
13	kutoka huko <u>vilitushinda</u>	kutoka huko <u>kulitushinda</u>
14	nomino ambal <u>olinatokana</u>	nomino ambayo <u>inatokana</u>
15	nomino <u>lina</u> maana...	nomino <u>ina</u> maana...

Jedwali Na. 4.10 linaonyesha kuwa kiambishi kipatanishi cha ngeli kilichotokea kwenye vitenzi kwa kiasi kikubwa huwa ni {i-}. Kipatanishi hiki kilijitokeza hasa badala ya {li-} na {ya-} (*Gali *ikanifikisha*><Gari *likanifikisha*, *Mahubiri *ilipofika*><Mahubiri *yalipofika*). Upande mwingine, jedwali hili hudhihirisha matumizi ya ngeli ya I-ZI inayohusisha nomino za vitu visivyo hai badala ya A-BA (katika Kingwana) au A-WA (katika Kiswahili Sanifu) ambayo inakusanya nomino za watu na wanyama (*Simba *iliuliwa*><Simba *aliuliwa*, *Nguruwe *zinaishi*><Nguruwe *wanaishi*).

4.3.3.1.2 Makosa ya Upatanisho kati ya Nomino/Kiwakilishi na Kivumishi

Kivumishi cha Kiswahili, kama ilivyo katika lugha zingine za kibantu, huambishwa viambishi ngeli kutokana na nomino husika. Hivyo, katika kirai nomino, kiambishi ngeli kinachoambikwa kwenye kivumishi huwa kilekile cha nomino hiyo au kile kinachotokana na ngeli ya nomino husika. Katika mchakato wa uwiano wa nomino na kivumishi, makosa yanayohusiana na uambatanishaji wa nomino na kivumishi yalijitokeza kwa kiasi cha 62 kwa 296, sawa na 20.94%; na zifuatazo ni baadhi ya sentensi zilizotungwa na wanafunzi.

8. (a) *Kwa namna *ingine*, ninaweza kusema kuwa elimu inasaidia (...).
→ Kwa namna *nyingine*, ninaweza kusema kuwa elimu husaidia (...).
- (b) *Nikaosha kinywa na *mwili zima*.
→ Nikapiga mswaki na kuoga mwili *mzima*.
- (c) *Polisi njiani walisimamisha *basi yetu*.
→ Tulipofika njiani, polisi walisimamisha basi *letu*.

Jedwali Na. 4.11 hapa chini linatoa mifano zaidi ya makosa ya upatanisho wa kisarufi yaliyopatikana katika kazi zilizotungwa na wanafunzi tafitiwa.

Jedwali Na. 4.11 : Upatanisho kati ya Nomino/Kiwakilishi na Kivumishi

Na.	Kosa	Sahihi
1	namna <i>ingine</i>	namna <i>nyingine</i>
2	<i>mwili zima</i>	mwili <i>mzima</i>
3	<i>basi yetu</i>	basi <i>letu</i>
4	utamaduni <i>yao</i>	utamaduni <i>wake(wao)</i>
5	elimu <i>mzuri</i>	elimu <i>nzuri</i>
6	<i>beskeli lake</i>	baiskeli <i>yake</i>
7	tumbo <i>liputu</i>	tumbo <i>tupu</i>
8	magoti <i>langu</i>	magoti <i>yangu</i>
9	<i>hiosiku</i>	<i>hiyosiku</i>
10	fasi <i>yingine</i>	nafasi <i>nyingine</i>
11	lengo <i>zetu</i>	malengo <i>yetu</i>
12	maali ya <i>kwanza</i>	mahalipa <i>kwanza</i>
13	lipi <i>nzuri</i>	lipi <i>zuri</i>
14	lipi <i>mbaya</i>	lipi <i>baya</i>
15	wajomba <i>wake</i>	wajomba <i>zake</i>

Jedwali Na.4.11 hapo juu linaonyesha virai nomino ambavyo upatanisho wa kisarufi ulitokea kinyume na kanuni za kisarufi. Kwa mfano, katika virai Na. 1 (*namna *ingine*><namna *nyingine*), 3 (**basi yetu*><*basi letu*), 5 (**elimumzuri*><*elimunzuri*), 8 (**magotilangu*><*magotiyangu*) na 12 (*Maali ya *kwanza*><Mahalipa *kwanza*), vivumishi husikahavikuambikwa viambishi vidhihirishavyo upatanisho wa kisarufi baina yake na nomino husika. Viambishi vipatanishi vilivyotumiwa havidhihirishi uwiano kati ya nomino na vivumishi vilivyoandamana nazo.

4.3.3.2 Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno

Makosa kuhusiana na ugeukaji wa viambishi tegemezi kuwa neno yalipatikana katika kazi mbalimbali zilizotungwa na wanafunzi. Katika lahaja ya Kingwana, ipo mifumo inayohusisha maneno halisi pale ambapo Kiswahili sanifu hutumia viambishi. Utafiti huu umedhihirisha kiasi cha makosa 47 kwa jumla ya makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia 295; sawa na 15.93%. Baadhi ya mifumo hiyo ilijitokeza wanafunzi walipotumia Kiswahili sanifu kama inavyodhihirika katika sentensi zifuatazo :

9. (a) *Nikabeba watoto ku masomo/ ku shule.
→ Nikawapeleka watoto shuleni.
- (b) *Nikarudi (...) mu kurudi nikakutanana najirani yangu.
→ Nikarudi (...) niliporudi (Katika kurudi) nikakutana na jirani yangu.
- (c) *Banafunzi benye balifika mapema awakuchelewa.
→ Wanafunzi waliofika mapema hawakuchelewa.
- (d) *Nikaona na wagonjwa wenye waliombewa.
→ Pia, nikaona wanagonjwa waliombewa.

Mifano zaidi imenukuliwa kutoka katika kazi za wanafunzi na kutolewa katika jedwali Na. 4.12 hapa chini.

Jedwali Na. 4.12: Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno

Na.	Kosa	Sahihi
1	<i>ku masomo</i>	<i>shuleni</i>
2	<i>ku chuo</i>	<i>chuoni</i>
3	<i>mu kurudi</i>	<i>niliporudi</i>
4	<i>benye balifika</i>	<i>waliofika</i>
5	<i>wenye waliombewa</i>	<i>waliqombewa</i>
6	<i>ndo akatusomea</i>	<i>ndipo alipotusomea</i>
7	<i>njo ivo</i>	<i>hivyo ndivyo</i>
8	<i>yenye ina watu</i>	<i>iliyo na watu</i>
9	<i>ndozenye zimesha songa mbele</i>	<i>ndizo zilizoisha songa mbele</i>
10	<i>ndo nikaona</i>	<i>ndipo nilipoona</i>
11	<i>ndo akatusomea</i>	<i>ndipo alipotusomea</i>
12	<i>nifika ku kaburimbo</i>	<i>nilipofika barabarani</i>
13	<i>bus ikanifikisha mu njia</i>	<i>basi likanifikisha njiani</i>
14	<i>twende ku kiti</i>	<i>twende kitini</i>
15	<i>ni mtu muhimu sana ndani ya inchi</i>	<i>ni mtu muhimu sana nchini</i>

Jedwali Na.4.12 hapo juu linaonyesha kuwa katika kazi zao, wanafunzi walitumia viambishi ngeli vya mahali *ku-* na *mu-* kabla ya nomino za kawaida *masomo* (shule) na *chuo* : **ku masomo=ku shule><shuleni, *ku chuo><chuoni*. Aidha, kulitumia ngeli ya mahali *mu-* badala ya kirejeshi cha mahali {-po-}(**mu kurudi><niliporudi*) wakimanisha wakati tendo lilipotendeka. Makosa mengine yanayowekwa bayana na jedwali hili yametokana na matumizi ya kivumishi {-enye}kilichoambikwa kiambishi ngeli kutokana na nomino husika na kutumiwa badala ya kiambishi rejeshi -o- (**benye balifika><waliofika, *wenye waliombewa>< waliqombewa*).

4.3.3.3 Kukata na Kuunganisha Maneno Visivyo

Katika mchakato wa maandishi, kukatia maneno pasipofaa au kuunganisha maneno visivyo huwaletea utata wasomaji na kupotosha ujumbe uliokusudiwa. Katika maandishi, inambidi mhusika kuzingatia mipaka kati ya neno na jingine ili pasiwe na utata. Maneno mawili au zaidi yanapounganishwa au neno moja linapokuwa katika sehemu mbili au zaidi hupatikana istilahi mpya lakini zisizo na maana yoyote. Makosa ya aina hii yalijitokeza mara 153 kati ya jumla ya makosa 295 ya kisintaksia na kimofosintaksia; sawa na 51.86%. Sentensi zifuatazo zilizonukuliwa kutoka katika nyaraka za wanafunzi hudhihirisha makosa ama ya kuunganisha au kukata maneno visivyo :

10. (a) *Mtu mwenye elimu ana fanya kazi nzuri sana.

→ ...*anafanya*...

(b) *Mtu aliye elimishwa ni mtu muhimu sana.

→ ...*aliyeelimishwa*...

(c) *Piya inasaidiya mtu namna yakuishi na wengine katika jamii yake.

→ ...*ya kuishi*...

(d) *Elimu ni msingi wamaisha ama wakutafuta maisha.

→ ...*wa maisha*... *wa kutafuta*...

Jedwali Na. 4.13 hapa chini linatoa mifano zaidi ya ulinganishi wa makosa ya aina hii na yaliyo sahihi.

Jedwali Na. 4.13 : Kukata na Kuunganisha Maneno Visivyo

Na.	Kosa	Sahihi
1	<u>ana fanya</u>	anafanya
2	<u>ina saidia</u>	inasaidia
3	<u>aliye elimishwa</u>	aliyeelimishwa
4	<u>nilipo kuwa</u>	nilipokuwa
5	<u>ana hubiri</u>	anahubiri
6	<u>Juma pili</u>	Jumapili
7	<u>wa faa</u>	wafaa
8	<u>tuka ingia</u>	tukaingia
9	katikamaisha	katika maisha
10	kwakujenga	kwa kujenga
11	yakuishi	ya kuishi
12	namambo	na mambo
13	kwaiyo	kwa hiyo
14	wamaisha	wa maisha
15	wakutafuta	wa kutafuta

Jedwali Na.4.13 linaonyesha kuwa baadhi ya maneno yalikatiwa mahali pasipofaa. Miongoni mwa maneno haya ni vitenzi kama inavyodhihirishwa na mifano Na. 1 (**ana fanya><anafanya*), Na. 2(**ina saidia><inasaidia*), na Na.4 (**nilipo kuwa><nilipokuwa*); na neno changamani (**Juma pili><Jumapili*). Upande mwingine, jedwali hili linadhihirisha kuwa baadhi ya maneno yaliandikwa kwa kuunganishwa. Maneno Na. 14 (**wamaisha><wa maisha*),9 (**Katikamaisha><Katika maisha*) na 11 (**yakuishi><ya kuishi*), ni mifano mwafaka ya makosa hayo.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni dhahiri kuwa makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia yalijitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na athari za Kingwana. Hivyo, katika upatanisho wa kisarufi, mifumo iliyojijengea uzoefu akilini mwa wanafunzi wa Kingwana ilitokea walipotumia Kiswahili sanifu. Katika upatanisho wa nomino na kitenzi, kwa mfano, ngeli ya I-ZI ilitumika badala ya ngeli zingine kama vile LI-YA au A-BA (A-WA, katika Kiswahili sanifu), kama ilivyodhihirishwa na mifano iliyotolewa awali. Hii ni kwa sababu ya ngeli I-ZI huwakilisha ngeli zozote katika Kingwana, na Kingwana chenyewe hubainisha ngeli ya watu na ya wanyama, ngeli ya wanyama ikiwa I-ZI na ya watu ikiwa A-BA. Ikumbukwe kuwa Kiswahili sanifu hukusanya nomino za watu na nomino za wanyama katika ngeli moja ya A-WA (A-BA katika Kingwana). Kuhusu upatanisho baina ya nomino/kiwakilishi na kivumishi, vivumishi viliondolewa viambishi vipatanishi vya ngeli au kupachikwa viambishi ngeli visivyo sahihi. Aidha, baadhi ya nomino zilitumiwa kwa umoja au kwa wingi kimakosa kwa kuongezewa viambishi visivyo sahihi au kwa kuondolewa viambishi ambavyo lazima vingekuwepo. Hii ina maana kuwa upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na kivumishi haukuzingatiwa kutokana na athari za Kingwana, kwani, kama anavyosema Kipacha (2003:209), katika upatanishi wa viambishi katika sentensi za Kingwana kuna kutopatana kwa viambishi vya nomino na kivumishi.

Kuhusu makosa ya ugeukaji wa viambishi tegemezi kuwa neno, kama mifano hapo juu inavyovionyesha, kulibainika uwakilishaji wa mofu kwa maneno asili. Sababu ya makosa haya kutokea ni kwamba, katika lahaja ya Kingwana, ipo mifumo inayohusisha maneno halisi pale ambapo Kiswahili sanifu hutumia viambishi. Kama

ilivyoonyeshwa na mifano iliyotolewa hapo juu, ngeli za mahali {mu-}, {pa-}, na {ku-} zinazotumika katika kuambisha nomino, matumizi ya viambishi {-enye} na maneno *ndo* na *njo* badala ya kiambishi rejeshi {-o-} katika Kingwana, hii ndiyo mifumo ya Kingwana iliyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Kuhusu makosa ya kukata na kuunganisha maneno kimakosa, sababu ya kutokea kwake ni uzoefu dhahiri wa kawaida katika maandishi ya wanafunzi wa Kingwana, hususan wazawa wa D.R Congo. Hivyo, maandishi yalidhihirisha utenganishaji wa viambishi tamati na shina la kitenzi katika mafungu mawili tofauti, na kosa hili lilitokea katika vitenzi 94 kati ya jumla ya maneno 120 yaliyoathiriwa na kosa hili. Aidha, uzoefu huu wa kukata maneno uliathiri maneno 30 ambayo ni changamani ambayo mofu changamano husika zilitenganishwa katika mafungu mawili tofauti, na nomino ambazo kiambishi ngeli kilitenganishwa na shina. Upande mwingine, kulitambulika uzoefu wa kuunganisha maneno yasiyo yenye hadhi sawa kisarufi, aghalabu kiunganishi au kihusishi na neno la aina nyingine.

Kazi tangulizi zilizoshughulikia makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia zinazoshabihiana na hii zinahakikisha athari za L1 za wajifunzaji katika ujifunzaji wa L2. Mulei na wenzake (2021) waligundua kuwa kipashio cha kimofosintaksia ya ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu yalidhihirisha athari za uhamishaji wa maumbo, mofofonolojia, ubebaji wa viambishi vya ngeli tofauti, uchopekaji wa viambishi, ubadilishanaji wa viambishi ngeli, uchanganyaji wa maumbo na ujumlishaji wa viambishi vya msingi vya ngeli ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano, ilidhihirika kuwa wanafunzi wa Luganda huhamisha ngeli za I-ZI na GU-GI za Luganda katika Kiswahili sanifu na kuzitumia

badala ya A-WA (*Ng'ombe zimeletwa nyumbani><Ng'ombe wameletwa nyumbani) na U-I (*Mukate gumeisha jikoni><Mkate umeisha jikoni, *Miti gimekatwa><Miti imekatwa). Vilevile, Ntawiyanga (2018) wanafunzi wengi wa Rwanda hufanya makosa mbalimbali katika upatanishi wa kisarufi kutokana ama na athari za Kinyarwanda (L1) au wanafunzi wenyewe kujumuisha kanuni za Kiswahili kwa kujirahisishia ujifunzaji wao. Ufanano mkubwa wa kazi ya Ntawiyanga na hii ni kwamba zote zinalenga kutambua aina za makosa yanayotokana na L1 ya mjifunzaji na kutathmini utamalaki wake.

4.4 Vyanzo vya Makosa ya Kisarufi katika Kiswahili Sanifu

Wanazuoni waliobobea katika uchunguzi wa makosa katika lugha walishughulikia vyanzo vya makosa hayo, aghalabu katika muktadha wa ujifunzaji wa L2. Kadiri walivyoshughulikia makosa yenyewe, ndivyo kadiri walivyojaribu kutambua vyanzo vyake. Kwa mfano, Richards (1971) alibainisha sababu za utokeaji wa makosa za aina tatu ambavyo ni (i) mwingiliano wa lugha tofauti, (ii) uamiliaji duni wa kanuni za lugha hiyohiyo moja na (iii) kutokamilika kiumilisi kutokana na wanafunzi kujaribu kujijengea nadharia kuhusu lugha lengwa kwa msingi wa ujuzi kidogo. Baada ya aina ya (ii) na (iii) kuonekana tata, Richards (1974) alitambua sababu za utokeaji wa makosa za aina mbili ambazo ni (i) mwingiliano wa lugha tofauti na (ii) kutokamilika kiumilisi. Upande mwingine, Dulay na Burt (1974) walibainisha sababu za utokeaji wa makosa katika makundi matatu ya (i) kutokamilika kiumilisi, (ii) mwingiliano wa lugha tofauti na (iii) hali ya upekee ambayo husababisha makosa ya kipekee ambayo si ya mwingiliano wala ukamilishaji.

Vilevile, James (1989, 1998); Ellis (1995); Ziahosseiny (1999); Keshavarz (2003, 2006); Şanal (2007); Darus (2009); Kazemian & Hashemi (2014) walishughulikia sababu za utokeaji wa makosa yafanywayo na wanafunzi wa L2. Wanazuoni hawa wanakubaliana kuwa sababu kuu za makosa huwa ni pamoja na (i) uhamishaji wa lugha, (ii) matumizi kupita kiasi ya kanuni fulani, (iii) ufupishaji, (iv) kwa mwanafunzi, kujali sana nyanja za kisarufi za L2 badala ya zile za L1, (v) kutozijua kanuni za lugha na (vi) mwingiliano.


Baada ya kuyachunguza makosa yaliyopatikana katika utafiti huu, imedhihirika kuwa sababu za utokeaji wa makosa yaliyotambulika ni pamoja na (i) uhamishaji wa lugha, (ii), ufupishaji, (iii) matumizi kupita kiasi ya kanuni fulani na (v) kutozijua kanuni za Kiswahili sanifu. Hivyo, katika sehemu hii, kulishughulikiwa lengo la tatu la utafiti huu, yaani kuchunguza vyanzo vya makosa ya kisarufi katika Kiswahili sanifu. Aidha, kulionyeshwa ni kwa kiasi gani chanzo au sababu fulani imesababisha makosa ya aina fulani kutokea.

Jedwali Na. 4.14 linaonyesha ni kwa kiasi gani sababu yoyote ya makosa ilisababisha utokeaji wa makosa ya aina fulani yaliyotambulika na utafiti huu.

Jedwali Na. 4.14 : Kiasi cha Makosa Kulingana na Vyanzo Vyake

Na.	Aina ya makosa	Sababu ya makosa	idadi ya makosa	Jumla ya makosa kwa kila aina	%
1	Makosa ya kifonolojia	Uhamishaji	255	365	69.86
		Ufupishaji	9	“	2.46
		Matumizi kupita kiasi ya kanuni	43	“	11.78
		Kutozijua kanuni	58	“	15.89
2	Makosa ya kimofolojia	Uhamishaji	126	214	58.87
		Ufupishaji	20	“	9.34
		Matumizi kupita kiasi ya kanuni	28	“	13.08
		Kutozijua kanuni	40	“	18.69
3	Makosa ya kisintaksia	Uhamishaji	105	295	35.59
		Ufupishaji	9	“	3.05
		Matumizi kupita kiasi ya kanuni	0	“	0
		Kutozijua kanuni	181	“	61.35
	Jumla		874	874	

Kutokana na jedwali hili, imedhihirika kuwa, katika kundi lolote la makosa, sababu zote za makosa zilizotambulika na utafiti huu zilisababisha utokeaji wa kiasi fulani cha makosa. Mchoro ufuatao unatamatisa matokeo kwa kuonyesha kwa ujumla namna zote za utokeaji wa makosa zilivyotofautiana.



Mchoro Na. 4.2: Sababu za Utokeaji wa Makosa

Kutokana na mchoro huu, ni dhahiri kuwa kwa jumla ya makosa 874 yaliyotambulika na utafiti huu, sababu ya uhamishaji ndiyo iliyosababisha makosa mengi kuliko vingine vyote, yaani makosa 486, sawa na 55.60%; ikifuatwa na sababu ya kutojua kanuni iliyosababisha utokeaji wa makosa 279, sawa na 31.92%; hiyo nayo ilifuatwa na sababu ya kutumia kanuni kupita kiasi iliyosababisha makosa 71, sawa na 8.12%, ambayo nayo ilifuatwa na sababu ya ufupishaji iliyosababisha utokeaji wa makosa 38, sawa na 4.34%. Sababu ya kwanza ya uhamishaji kuwezesha utokeaji wa makosa ya kisarufi mengi zaidi ni kwamba mifumo kadhaa ya Kingwana ilihamishwa kutoka katika lugha mbalimbali zinazotumika kwenye eneo lake. Hivyo, kuhamisha mifumo ya Kingwana kwenda Kiswahili sanifu kulitokea kama suluhisho, kwani wanafunzi husika hawakuweza kutambua tofauti kati ya mifumo ya Kingwana na ile ya Kiswahili sanifu.

4.4.1 Makosa kutokana na Uhamishaji wa Lugha

Katika uhamishaji, mifumo ya L1 hupelekwa na kutumika katika ama mazungumzo au maandishi ya L2. Mara nyingi, uhamishaji huwa sababu ya makosa yafanywayo na waamiliaji wa L2. Katika utafiti huu, yamedhihirika makosa yaliyojitokeza kutokana na sababu hii ya uhamishaji mara 486 kati ya jumla ya makosa 874, sawa na 55.60%.

4.4.1.1 Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Uhamishaji

Katika matumizi ya Kiswahili sanifu, wanafunzi wa Kingwana walihusika na makosa ya kifonolojia ambayo sababu yake huwa ni uhamishaji. Uchambuzi wa makosa ya kifonolojia umeonyesha kuwa makosa kutokana na uhamishaji yalitokea kwa kiasi cha makosa 255 kwa jumla ya makosa ya kifonolojia 365, sawa na 69.86%. Mifano ifuatayo inadhihirisha uhamishaji wa mifumo ya kifonolojia kutoka Kingwana kwenda Kiswahili sanifu :

11. (a) *Nimekutana na magari mengi balabalani *ivo* nimefika *apa* chuoni.

→ Nimekutana na magari mengi barabarani, hata *hivyo* nimefika *hapa* chuoni.

(b) *Nikakuta mwalimu bado *ajafika*.

→ Nikakuta mwalimu bado *hajafika*.

Katika sentensi 11(a) na 11(b) maneno *hivyo*, *hapa* na *hajafika* yamedondolewa fonimu /h/ (**ivo*><*hivyo*, **apa*><*hapa*, **ajafika*><*hajafika*). Sababu ya makosa hayo kutokea ni kwamba wazawa wa Kingwana hudondosha fonimu /h/ pale ambapo Kiswahili sanifu hulazimika kuitumia fonimu hiyo.

12(a) *Nilikuwa nikizani ni mchezo

→ Nilikuwa nikidhani ni mchezo.

(b) *Nikaendelea kuya na miguu.

→ Nikaendelea kuja kwa miguu.

(c) *...mrango na madirisha, vyote vimefungwa.

→ ...mlango na madirisha, vyote vimefungwa.

(d) *Jana wametosomeya baruwa kutoka cuo gikuu.

→ Jana walitusomea barua kutoka chuo kikuu.

Mifano hapa juu inadhihirisha sifa za launi mbalimbali za Kingwana ambazo huingizwa katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Sentensi 12(a) na 12(b) zinadhihirisha matumizi ya kawaida ya fonimu /z/ na /j/ badala ya /ð/ na /ʃ/ (*nikizani><nikidhani, *kuya><kuja). Upande mwingine, sentensi 12(c) na 12(d) hudhihirisha uhamishaji wa fonimu za Kingwana na lugha za kijamii zinazopakana nacho, ambazo pia huathiri Kiswahili sanifu. Kwa mfano, Kirundi na Kinyarwanda hutumia kimandende /r/ pale ambapo Kiswahili sanifu hutumia kitambaza /l/ (kurâra, umuryân̄go). Pia, lugha hizo huhusisha kanuni ya kimofonolojia ya usigano ambayo fonimu mbili ambazo si ghuna haziwezi kufuatana kwenye mipaka ya mofu (gikurú><*kikurú, gusoma><*kusoma). Hivyo, launi ya Kingwana itumikayo nchini Burundi na Rwanda iliathiriwa na mifumo hiyo ya kifonolojia; na mifumo hiyo ilitokea katika matumizi ya Kiswahili sanifu (L2) kwa wanafunzi waongeo Kingwana (L1) (*mrango><mlango, *gikuu><kikuu).

13. (a) *Nilipitiya nyakati tofahuti.

→ Nilipitia nyakati tofauti.

(b) *Mwenyezi Mungu yeye *alionilamusha*.

→ Mwenyezi Mungu ndiye *aliyeniamsha*.

(c) *Alitupa *mfano* wa kauli za Kiswahili.

→ Alitupa *mfano* wa kauli za Kiswahili.

(d) *Nilikuta bado wanafunzi wapo *inje*.

→ Nilikuta bado wanafunzi wapo *nje*.

(e) *Jambo la *inne* na la mwisho (...).

→ Jambo la *nne* na la mwisho (...).

Katika sentensi 13(a) na 13(b), baina ya /i/ na /a/ na /a/ na /u/ kuliingizwa /j/, /h/ na /l/ (**Nilipitiya* >< *Nilipitia*, **tofahuti* >< *tofahuti*, **alionilamusha* >< *aliyeniamsha*). Aidha, katika 13(b) na 13(c) baina ya konsonanti halisi mbili /m/ na /j/ au /m/ na /f/ kuliingizwa konsonanti fulani (**alionilamusha*><*aliyeniamsha*, **mfano*><*mfano*). Mifumo hiyo ya kimatamshi iliyotokana na lugha za kijamii zilizoathiri Kingwana ilitokea kuwa kama kawaida, hivi kwamba wanafunzi wa Kingwana wanapotamka au kuandika maneno ya Kiswahili sanifu huzalisha ama konsonanti kati ya irabu mbili zinazoandamana au irabu kati ya konsonanti halisi mbili zinazoandamana na kutamkika kwa namna tofauti. Hivyo, ni dhahiri kuwa lahaja ya Kingwana hudumisha mfumo wa silabi KI. Upande mwingine, katika 13(d) na 13(e) kulijitokeza fonimu /i/ kwenye maneno *nje* na *nne*. Fonimu /n'/ inayojibainisha kimatamshi na *je* na *ne* ilipachikwa fonimu /i/ na kudhoofishwa kwa fonimu /n'/ katika lahaja ya Kingwana. Kwa hiyo, wanafunzi wa Kingwana waongea Kiswahili sanifu huweka fonimu /i/ mwanzoni mwa maneno yanayohusisha fonimu /n'/.

4.4.1.2 Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Uhamishaji

Katika maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu, mifumo kadhaa ya kimofolojia ya Kingwana iliamishwa kwenda katika Kiswahili sanifu kwa kiasi cha makosa 126 kwa jumla ya makosa ya kimofolojia 214, yaani 58.87%. Kulingana na Kiswahili sanifu, lahaja ya Kingwana huwa na sifa za kimaumbo za kipekee ambazo huitenganisha na Kiswahili sanifu. Kwa mfano, lahaja ya Kingwana ama hudondosha viambishi kutoka katika maneno au huongeza viambishi katika maneno tofauti na kawaida ya Kiswahili sanifu. Sentensi zifuatazo ni mifano idhihirishayo uhamishaji wa mifumo ya kimofolojia.

14. (a) *Wakati tulikuta vyombo vyote, ...

→ Wakati tulipokuta vyombo vyote, ...

(b) *Hapana, kila siku ninaingia ninalipa mia saba.

→ Hapana, kila siku ninapoingia ninalipa mia saba.

(c) *Nilikwenda pamoja na rafiki yangu anaitwa Kaneza.

→ Nilikwenda pamoja na rafiki yangu anayeitwa Kaneza.

15. (a) *Niliwasalimia rafiki zangu.

→ Niliwasalimia marafiki zangu.

(b) *Inatubidi ku elimishwa ili tupate kufanyikisha lengo zetu.

→ Inatubidi kuelimishwa ili tupate kufanikisha malengo yetu.

Katika sentensi 14(a), 14(b) na 14(c) viambishi rejeshi {-po-} na {-ye-} vilidondoshwa kutoka katikavitenzi husika (*tulikuta >< tulipokuta, *ninaingia >< ninapoingia, *anaitwa >< anayeitwa). Kingwana cha Burundi, Rwanda na D.R Congo kiliathiriwa na lugha zenye toni (Kirundi, Kinyarwanda, Lingala, Mashi, n.k)

zinazopakana nacho ambazo urejeshi hudhihirika kwa toni hadi kikadhihirika kutohusisha viambishi rejeshi. Hivyo, Waswahili wa maeneo hayo huingiza mfumo huo katika Kiswahili sanifu kwa kudondosha viambishi rejeshi. Kuhusu 15(a) na 15(b) watafitiwa walitumia mfumo wa Kingwana udumishao matumizi ya ngeli ya I-ZI badala ya ngeli zingine, hasa kwa nomino zenye viambishi awali kapa. Hivyo, nomino *marafiki* ya A-WAna nomino *malengo* ya LI-YA zimeondolewa kiambishi cha wingi *ma-* na kuingizwa katika ngeli ya I-ZI (**rafiki*><*marafiki*, **lengo*><*malengo*). Kwa mantiki hiyo, vivumishi vilivyoshirikiana na nomino hizi vimeambikwa viambishi ngeli kutokana na ngeli ya I-ZI.

16. (a) Niliamka *nikakula*.

→ Niliamka, *nikala*.

(b) Usiache masomo ili *usikuuwe* kama mimi.

→ Usiachane na kisomo ili *usiwe* kama mimi.

(b) Inasaidia wakaaji *kukuuwa* na mwanga katika maisha yao.

→ Inasaidia wakaaji kuwa na mwanga...

(c) Bus ilikuya nikapanda *tukakuuya*.

→ Basi lilikuja nikapanda *tukaja* (*tukaelekea huku*).

Katika sentensi 16(a), 16(b) na 16(c) kiambishi kisichofaa {-ku-} kimepachikwa katika vitenzi vyenye silabi moja kula (**nikakula*><*nikala*), kuwa (**usikuwe*><*usiwe*) na kuya (kuja) (**tukakuya*><*tukaja*). Katika Kiswahili sanifu, kiambishi {ka-} kidhihirishacho hali ya mfuatano wa matendo hakiandamani na Kiambishi {ku-}. Hata hivyo, mfumo wa {ka-} kufuatana na {ku-} ni wa kawaida katika Kingwana. Hivyo, matumizi ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa Kingwana

huathiriwa na mfumo huo wa Kingwana pale ambapo kiambishi {*ku-*}kingeondolewa katika vitenzi vyenye silabi moja.

17. (a) *Hio siku *ilikuwaga* siku ya shangwe kweli.

→ Hiyo siku *ilikuwa* siku ya shangwe kweli.

(b) *Watoto bengi *balichezaga* mupira.

→ Watoto wengi *walicheza* mpira.

18. (a) *Ata *wa* mama, baba, kaka, dada wanaitaji kuwa na elimu.

→ Hata (*akina*) *mama*, *baba*, *kaka* na *dada* wanahitajikuelimika.

(b) *Nimesalimiya *wajamanibangu*.

→ Nimewasalimia *jamaa zangu*.

(c) ... *wazazi wengi upeleka watoto wao mu *mashule*.

→ Wazazi wengi hupeleka watoto wao *shuleni*.

Kuhusu 17(a) na 17(b) kulijitokeza matumizi ya kiambishi {-ag-} ambacho ni cha kawaida katika Kingwana, kikidhihirisha hali ya kuendelea kwa tendo (Nshimirimana, 2019:19) (**ilikuwaga*><*ilikuwa*, **balichezaga* >< *walicheza*). Katika sentensi 18(a), 18(b) na 8(c) nomino zenye viambishi kapa zilipachikwa viambishi, hasa vionyeshavyo wingi wa nomino (**wa* mama><*mama*, **wa* baba><*baba*, **wajamani*><*jamani*, *n.k*). Hivyo, wanafunzi wa Kingwana wanapotumia Kiswahili sanifu huhusisha hoja ya kawaida katika Kingwana kwamba katika ubantu, nomino hulazimika kuwa na kiambishi awali, aghalabu kiambishi cha wingi.

Upande mwingine Kingwana huwa na msamiati unaodhihirisha utokeaji wa viambishi ngeli ambavyo si vya kawaida katika Kiswahili sanifu. Hivyo, maneno kama “*batu, batumwa, mukulu, bugali, bugari, balikuenda, mubaya*” (Kipacha, 2003: 205); “*bile bitu, batoto, ba mujini*” (Nshimirimana, 2019:10-15) huonyesha baadhi ya sifa bainifu za kimofolojia baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kingwana. Maneno yaliyoandikwa kwa mlazo katika sentensi zifuatazo ni mifano mingine ya uhamishaji wa kimofolojia kutoka Kingwana kwenda katika Kiswahili sanifu.

19.(a) Kuabudu Mungu kwa nyimbo pamoja na *baimbaji*.

→ Mungu akiabudiwa na *waimbaji* kwa nyimbo.

(b) **Banafunzibenyebalifika* mapema *awakuchelewa*.

→ *Wanafunzi waliofika* mapema *hawakuchelewa*.

(c) **Bachache bakashuka bengine bakaingia, bengine bako banaelekea* shuleni.

→ *Wachache wakashuka, wengine wakaingia* ambapo *wengine walikuwa wanaelekea* shuleni.

(d) ...baada ya dakika hamsini *bikiwabinaiva* arafu nikala.

→...baada ya dakika hamsini, *yikiwayimeiva*, halafu nikala

(e) Juma pili nime ona mambo *mingi* sana.

→ Jumapili niliona mambo mengi sana.

(f) ... *muhubiri* wa maneno ya upendo akapita.

→ ... *mhubiri* wa injili akapita.

20. (a) *Asubuhi ya leo *nilitoka* nyumbani saa moja na dakika hamsini na tano.

→ Leo asubuhi *nimetoka* nyumbani saa 1:55.

(b) *Kwa miguu, *nilichukuwa* dakika tano kufika chuoni.

→ Kwa miguu, **nimechukua* (nimetumia) dakika tano kufika chuoni.

(c) *Siku yaleo *tulisoma* visuri.

→ Leo *tumesoma* vizuri.

Sentensi 19(a), 19(b), 19(c), 19(d), 19(e) na 19(f) zinadhihirisha uhamishaji wa viambishi vya Kingwana kwenda katika Kiswahili sanifu. Viambishi vya kawaida katika Kingwana {*ba-*}, {*bi-*}, {*mi-*} na {*mu-*} vimetumikabadala ya viambishi asili vya Kiswahili sanifu {*wa-*}, {*vi-*}, {*ma-*} na {*m-*}. Hivyo, ni dhahiri kuwa ngeli ya A-WA na KI-VI katika Kiswahili sanifu huwa ni A-BA na KI-BI katika Kingwana. Aidha, matumizi ya viambishi vipatanishi vya nomino na kivumishi {*mu-*} (**muhubiri*><*mhubiri*) na {*ba-*} (**bachache*><*wachache*, **bengine*><*wengine*) yamedhihirisha kuwa viambishi ngeli vya aina hii huwa ni MU-BA katika Kingwana. Katika 20(a), 20(b), na 20(c) kumetokea mkanganyiko kwa wanafunzi watafitiwa hivi kwamba hawakuweza kubainisha viambishi vionyeshavyo wakati uliopita na wakati uliopita muda kidogo au hali timilifu. Katika Kiswahili sanifu wakati uliopita hudhihirishwa na kiambishi {-*li-*} ambapo wakati uliopita muda kidogo huonyeshwa na mofu {-*me-*}, ilihali lahaja ya Kingwana hutumia {-*me-*} ama kwa wakati uliopita sana au wakati uliopita muda kidogo au hali timilifu. Pia, launi ya Kingwana itumikayo kwenye maeneo mbalimbali nchini D.R.Congo, huhusisha {-*ka-*} badala ya {-*li-*}. Hivyo, uzoefu wa wanafunzi wa Kingwana umewasababisha kushindwa kubainisha tofauti za kimatumizi kati ya {-*li-*}, {-*me-*} na {-*ka-*} hivi kwamba hukosea kwa kutumia *-me-* badala ya {-*li-*} au {-*li-*} badala ya {-*me-*}, au tena {-*ka-*} badala ya {-*li-*}.

4.4.1.3 Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Uhamishaji

Uchanganuzi wa makosa ya kisintaksia umeonyesha kuwa makosa kutokana na uhamishaji wa mifumo ya kisintaksia ya Kingwana katika Kiswahili sanifu yamejitokeza kwa kiasi cha 105 kwa jumla ya makosa ya kisintaksia 296, sawa na 35.59%. Kulingana na Kiswahili sanifu, Kingwana huwa na mifumo ambayo huwa ni sifa zake za kisintaksia, na sifa kubwa huwa ni kutopatana kwa maneno yaundayo tungo (Kipacha, 2003). Mifano ifuatayo inadhihirisha mifumo mahususi ya sintaksia ya Kingwana :

- a) Mwalimu Bahati analimishaga *shamba yake*. (Nshimirimana, 2019:12)
→ Mwalimu Bahati analimisha *shamba lake*.
- b) Tukiondokaga ku shule, tutaendaga ku mashamba. (Nshimirimana, 2019:12)
→ Tukiondoka kutoka shuleni, tutaenda mashambani.
- c) Lakini, zamani sana, pombe ilikufaña *kitu moya mubaya* (Kipacha, 2003:205)
→ Lakini, zamani sana, pombe ilionekanya uwe mtu mbaya.
- d) ...ñumbani *mi iko* na amani, sana *faida tena ingine mubaya*, kwa sababu ya pombe. (Kipacha, 2003:205)
→...nyumbani mimi nina amani, sana faida tena nyingine mbaya, kwa sababu ya pombe.

Sentensi zilizotolewa hapo juu zimedhihirisha mifumo ya kipekee ya lahaja ya Kingwana ambayo si ya kawaida katika Kiswahili sanifu. Hii ni pamoja na upatanisho wa kisarufi usiozingatia ngeli ya nomino husika kama inavyoonekana

katika 21(a), 21(c) na 21(d) (*shamba yake, kitu moya mubaya, mi iko, faida tena ingine mubaya*); uzalishaji wa maneno yawakilishayo mofu kama katika (*ku shule, ku mashamba*), upangaji maneno ambao hauhusishi uhusiano baina ya vipashio vifuasi hali kwamba asiye mwenyeji huambuliwa patupu (mf: *ñumbani mi iko na amani, sana faida tena ingine mubaya*), n.k.

Hivyo, katika kazi za watafitiwa, mifumo ya kisintaksia iliyohamishwa kutoka Kingwana kwenda Kiswahili sanifu inahusiana na upatanisho wa kisarufi, ugeukaji wa viambishi kuwa maneno, kukata na kuunganisha maneno visivyo. Sentensi zifuatazo hudhihirisha makosa ya kisintaksia kutokana na uhamishaji.

21. (a) *Gali *ikanifikisha* mjini.

→ Gari *likanifikisha* mjini.

(b) *Mahubiri *ilipofika* mwisho, tulimuabudu tena Mungu kwa nyimbo.

→ Mahubiri *yalipofika* mwisho (...) → Mahubiri *yalipoisha*, (sahihi)

(c) *Kila kabila *ina* utamaduni yao.

→ Kabila lolote *lina* utamaduni wake.

22. (a) *Simba *iliuliwa* na askari polisi.

→ Simba *aliuliwa* na askari polisi.

(b) *Nguruwe zetu *zinaishi* kibandani.

→ Nguruwe wetu *wanaishi* kibandani.

Sentensi na. 21(a), 21(b) na 21(c) hudhihirisha uhamishaji wa mfumo wa kimofosintaksia wa Kingwana kwenda Kiswahili sanifu. Kiambishi kipatanishi cha ngeli kilichotokea kwenye vitenzi vyote huwa ni {i-} badala ya {li-}, {ya-} na {li-}. Katika lahaja ya Kingwana, ngeli ya I-ZI huwa na uamilifu wa ngeli zingine zote,

hivi kwamba hujitokeza badala ya ama ngeli hii au ile nyingine, hasa katika nomino ambazo viambishi ngeli huwa ni kapa (mf. gari). Aidha, kuhusu 22(a) na 22(b), watafitiwa wametumia mfumo wa Kingwana pale ambapo nomino za wanyama na nomizo za watu hubainisha; nomino za wanyama zikiwekwa katika ngeli ya I-ZI, nomino za watu katika ngeli ya A-BA. Ikumbukwe kuwa Kiswahili sanifu hukusanya nomino za watu na nomino za wanyama katika ngeli moja ya A-WA (A-BA katika Kingwana).

23. (a) *Elimu inatumika *fasi yingine* sana serekarini
 → Elimu inatumika katika nafasi *nyingine* serikalini.
- (b) *Kwa namna *ingine*, ninaweza kusema kuwa elimu inasaidia (...).
 → Kwa namna *nyingine*, ninaweza kusema kuwa elimu husaidia (...).
24. (a) *Polisi njiani walisimamisha *basi yetu*.
 → Tulipofika njiani, polisi walisimamisha basi *letu*.
- (b)*Kila kabila ina utamaduni *yao*.
 → Kabila lolote lina utamaduni *wake*.
- (d) *Tulikuta bei kari sana kuliko *soko zingine*.
 → Bei ilikuwa kubwa sana kuliko katika masoko *mengine*.

Katika 23(a) na 23(b), kivumishi *ingine* hakikuambikwa kiambishi kidhihirishacho upatanisho wa kisarufi baina yake na nomino *fasi (nafasi)* na *namna*. Pale ambapo kiambishi kipatanishi kingekuwa {NY-}, kumejitokeza uhamishaji wa upatanisho wa kisarufi wa Kingwana utumiyao {(y)i-} badala ya {NY-}. Katika tungo 24(a) na 24(b), vivumishi vimeambikwa kipatanishi {i-} (umoja) (-*etu*, na *-*ao*) na {zi-} (wingi)(-*ingine*). Katika Kingwana, ngeli ya I-ZI hutumika mara kwa mara badala ya

ngeli zingine. Hivyo, katika matumizi ya Kiswahili sanifu wanafunzi wameathiriwa na mifumo ya upatanisho ipatikanayo katika lahaja ya Kingwana, na kuihamisha kwenda Kiswahili sanifu.

25. (a) *Niliendelea na safari yangu ya kuenda ku masomo.

→ Niliendelea na safari yangu nikielekea shuleni.

(b) *Gufika hapa ku chuo, tena niliwanza masomo yangu ya leo.

→ Nilipofika hapa chuoni (...).

(c) ... alafu mwalimu akafika tukaingia mu darasa

→ ... halafu mwalimu akafika tukaingia darasani.

(d) *Nikarudi (...) mu kurudi nikakutanana najirani yangu.

→ Nikarudi (...) niliporudi (*Katika kurudi*) nikakutana na jirani yangu.

Mifano iliyotolewa hapa juu imeonyesha mifumo ya kisintaksia ambayo si ya kawaida katika Kiswahili sanifu. Katika lahaja ya Kingwana, ngeli za mahali {mu-}, {pa-}, na {ku-} zinapotumika zinaweza kuambisha nomino. Katika sentensi 25(a), 25(b), 25(c) na 25(d) kumejitokeza matumizi ya viambishi ngeli vya mahali *ku-* na *mu-* kabla ya nomino za kawaida *masomo* (*shule*), *chuo*, *darasa* na nomino ya kitenzi jina *kurudi*. Kulingana na mifumo sahihi ya Kiswahili sanifu, ngeli za mahali zilitumika pamoja na nomino badala ya vielezi vya mahali (**ku masomo*=*ku shule*><*shuleni*, **ku chuo*><*chuoni*, **mu darasa*><*darasani*). Aidha, kulijitokeza ngeli ya mahali {*mu-*}badala ya kirejeshi cha wakati {-*po-*}(*mu* *kurudi*)><*niliporudi*) kumanisha wakati tendo lilipotendeka.

26. (a) *Jana, nilikuwa natoka shuleni penye nasomea.

→ Jana, nilikuwa natoka shuleni ninaposomea.

(b) ... *mwenye ameingia ndani ya nyumba yangu akachukua mali zangu.

→...aliyeingia ndani ya nyumba yangu akachukua mali zangu.

27. (a) *Ndo akatusomea alitufundisha vizuri.

→ Ndipo alipotusomea na kutufundisha vizuri.

(b) *Njo ivo safari yangu imeendeka.

→ Hivyo ndiyyo safari yangu ilivyotokea.

Katika 26(a) na 26(b), athari nyingine ya kisintaksia kutoka Kingwana ilijitokeza katika Kiswahili sanifu. Kama ilivyoelezwa awali, launi ya lahaja ya Kingwana itumikayo Mjini Bujumbura, baadhi ya maeneo ya D.R Congo na Rwanda haihusishi viambishi rejeshi. Wakati mwingine, kiambishi {-enye} kilichoambikwa kiambishi ngeli kutokana na nomino husika hutumika kuwakilisha kiambishi rejeshi fulani(*penye nasomea>< ninaposomea, *mwenye ameingia >< aliyeingia).Badala ya kiambishi rejeshi -o- wanafunzi walitumia mfumo wa Kingwana uhusishao neno -enye. Pia, katika sentensi 27(a) na 27(b), mfumo wa Kingwana uhusishao maneno ndo na njo ulitumika badala ya virejeshi (*ndo><ndipo alipotusomea, *Njo ivo><Hivyo ndiyyo).

4.4.2 Makosa Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha Lengwa

Katika utafiti huu unaohusika na makosa ya wanafunzi wa Kingwana wajifunzao Kiswahili sanifu, kutozijua kanuni za Kiswahili sanifu kulitokea kuwa sababu nyingine ya makosa yaliyotambulika na utafiti huu. Makosa yaliyotokana na kutozijua kanuni za Kiswahili sanifu yalipatikana kutoka katika nyanja za lugha zinazolengwa na utafiti huu, yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia ; na yalitokea

mara 279 kati ya jumla ya makosa 874 yaliyotambulika na utafiti huu, sawa na 31.92%.

4.4.2.1 Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha

Kutozijua kanuni za lugha kumesababisha kutokea kwa makosa ya kifonolojia, aghalabu makosa yanayotokana na udondoshaji wa fonimu. Sababu hii yakutozijua kanuni ilichochea utokeaji wa makosa ya kifonolojia kwa kiasi cha 58 kwa jumla ya makosa ya kifonolojia 365, yaani 15.89%. Hebu tutazame mifano ifuatayo ni mifano ya makosa ya kifonolojia yaliyotokana na kutojua kanuni za Kiswahili sanifu:

28. (a) Nimekutana na rafiki yangu *ambae* tunasoma *nae*.

→ ... rafiki yangu *ambaye* ... *naye*.

(b) Alituambia maneno machache *yaliomo*.

→ ... machache *yaliyomo*.

(c) *Yalionikuta* jana nyumbani

→ **Yaliyonikuta* (*niliyokutananayo*)

(d) ...ili tujuwe kazi tunazo wiki *ijao*.

→ ...wiki *ijayo*.

(e) Hali *iliojitokewa...*

→ Hali *iliyojitokeza...*

Katika tungo zilizotolewa hapa juu, watafitiwa walidhihirika kutokamilika katika matumizi ya kanuni za kimofolojia hali ambayo ilisababisha udondoshaji wa fonimu ambazo lazima zingekuwapo. Kwa ujumla, sentensi zote zilizotolewa hapo juu zimedhihirisha kutokamilika katika matumizi ya viambishi rejeshi na kiwakilishi. Katika 28(a) nomino *rafiki* ambayo ni ya ngeli ya A-WA imehusishwa na {-e}

badala ya kirejeshi {-ye} (**ambae*><*ambaye*). Pia, kiunganishi {*na*} kimeshirikishwa na {-e} badala ya kiwakilishi {-ye} (**nae*><*naye*). Katika 28(b) na 28(c), ujuzi duni wa virejeshi kutokana na ngeli ya LI-YA ulisababisha udondoshaji wa fonimu /j/ (y) kutoka katika kirejeshi {-yo} (**yaliomo*><*yaliyomo*, *Yalionikuta*><*Yaliyonikuta* (*niliyokutananyo*)). Vilevile, katika 28(d) na 28(e) ngeli husika (I-ZI) haikuzingatiwa katika matumizi ya virejeshi; fonimu /j/ (y) ilidondoshwa kutoka katika kirejeshi {-yo} (**ijao*><*ijayo*, **ilijitokewa*><*ilijitokeza*).

4.4.2.2 Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Kutozjua Kanuni za Lugha

Miongoni mwa makosa ya kimofolojia yaliyotambulika na utafiti huu, yamo yaliyotokana na ujuzi wa wanafunzi usiokamilika katika matumizi ya viambishi mbalimbali. Makosa haya yalijitokeza hasa kutokana na matumizi ya viambishi visivyofaa badala ya vile ambavyo vingekuwa sahihi katika mazingira husika. Sababu hii ilisababisha utokeaji kiasi cha makosa ya kimofolojia cha 40 kati ya jumla ya makosa ya kimofolojia 214, sawa na 18.69%. Sentensi zifuatazo zinadhihirisha mifano ya makosa kutokana na ujuzi usiokamilika katika matumizi ya viambishi husika.

29. (a) *Nchi ambapo watu walielimika *n*ie** nchi tajiri.

→ Nchi ambapo watu walielimika *ndiyo* nchi inayotajirika.

(b) *Watu walikua wengi *waliyo shirikiumo* ndani.

→ Watu *walio*shiriki humo ndani walikuwa wengi.

(c) *Ingieni kanisa muone furaha ambayo *ninayo waeleza*

→ Ingieni kanisani mpate furaha *ambayo* ninawaeleza.

(d) *Tukiwa tunatumika kazi si kama wale watu *ambaye* hawajasoma.

→ ...si kama wale watu *ambao* hawajasoma.

(e) *Padre *aliyosimama*, akatupa baraka kutoka kwa Mungu.

→ Padre *aliposimana*, alitupa baraka kutoka kwa Mungu.

30. (a) *...jana, *anamaliza* kutuombea mabalaka.

→ ...jana, *alimaliza* kwa kutuombea baraka.

(b) *...tukakutana na mwizi *anayekupigwa* fimbo.

→ ...*aliyepigwa* fimbo.

31. (a) **Nikimaliza* kununua mchere na maharage nililudi.

→ *Nilipomaliza* kununua mchele na maharage nilirudi (nyumbani).

(b) **Nikimaliza* nikaenda kuchunga gari la kunileta mjini.

→ *Nilipomaliza* niliendakusubiria gari la kunipeleka mjini.

(c) *Yalionikuta jana nyumbani *nikitoka* shule, ...

→ Niliyokutana nayo jana nyumbani *nilipotoka* shuleni, ...

Katika mifano 29(a), 29(b), 29(c), 29(d), na 29(e) kumejitokeza matumizi yasiyo sahihi ya viambishi rejeshi. Wanafunzi wa Kingwana ambao matumizi ya virejeshi ni ya hiari hukosea kwa kuvitumia bila kuzingatia ngeli ya nomino husika. Aidha, katika 29(c) kumejitokeza matumizi ya virejeshi vya aina mbili tofauti (amba-rejeshi na -o-rejeshi) katika sentensi moja (*furaha *ambayoninayo* waeleza><furaha *ambayoninawaelezea*). Katika sentensi za 30(a) na 30(b) mwanafunzi alitumia wakati wa sasa badala ya wakati uliopita (**anamaliza*><*alimaliza*, **anayekupigwa*><*aliyepigwa*); katika matumizi ya vitenzi, ushirikiano wa matendo yaliyotokea katika wakati uliopita hukuzingatiwa. Upande mwingine, sentensi 31(a) na 31(b) zimedhihisha matumizi yasiyofaa ya kiambishi cha hali ya masharti ya

wakati ujao {-ki-} (**Nikimaliza*><*nilipomaliza*, **Nikimaliza*><*Nilipomaliza*), na kiambishi cha hali ya kuendelea kwa tendo {-ki-} (**nikitoka*><*nilipotoka*).

4.4.2.3 Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Kutozijua Kanuni za Lugha

Baadhi ya makosa ya kisintaksia yalitokana na kutoamili kanuni husika katika upatanishi wa kisarufi, kanuni ziwakilishazo uwiano sahihi wa maneno katika tungo au sentensi. Sababu hii ilisababisha utokeaji wa makosa ya kisintaksia kwa kiasi cha 182 kati ya jumla ya makosa ya kisintaksia 295, sawa na 61.69%. Ifuatayo ni mifano iliyotokana na kutojua kanuni husika.

32. (a) *Elimu *lina* umuhimu mengi sana, *lina* *saidiya* kuondoa ujinga.

→ Elimu *ina* umuhimu sana, *inasaidia* katika kuondoa ujinga.

(b) *Elimu *unasadia* katika maisha.

→ Elimu *inasaidia* katika maisha.

(c) *Kutoka huko *yilitushinda* kweli.

→ Kutoka huko *kulitushinda* kweli.

(d) *Mazoezi ni *nomino ambalolinatokana* na kitenzi kuzoea

→ “Mazoezi” ni *nomino ambayoinatokana* na kitenzi “kuzoea”.

33. (a) *Nikaosha kinywa na *mwili zima*.

→ Nikapiga mswaki na kuoga *mwili mzima*.

(b) *Elimu *linasaidia* mtu kujuwa *lipi nzuri* la kufanya na *lipi mbaya* la kuachana nalo.

→ Elimu *inamsaidia* mtu kujua *lipi zuri* la kufanya na *lipi baya* la kuachana nalo.

(c) *Mtu alie kuwa na *elimu mzuri*.

→ Mtu aliye na *elimu nzuri*.

(d) *Tukaelekea katika upande *wingine*.

→ Tukaelekea (katika) *upande mwingine*.

(e) *Nyumbani mtu anapata elimu kutokea wazazi wake, *wajomba wake, changaziwake* kupitiya hadisi.

→ ... *wajomba zake, shangazi zake...*

Katika sentensi hapa juu, upatanisho wa kisarufi umedhihirisha ujuzi wa watafitiwa usio kamili katika kuonisha maneno yaundayo sentensi. Katika sentensi 32(a), 32(b), 32(c), 32(d) na 32(e) viambishi vipatanishi vya nomino na vitenzi havikuwakilisha uwiano sahihi katika mfuatano wa vipashio vya tungo kutokana na nomino husika (*Elimu *lina*><Elimu *ina*, *Elimu *unasadia*><Elimu *inasaidia*, **nomino ambalolinatokana*><*nomino ambayoinatokana*,...). Wanafunzi watafitiwa walionyesha kutokamilika katika matumizi ya ngeli za nomino za Kiswahili sanifu, na hivyo kusababisha uwiano wa nomino na kitenzi usio sahihi katika sentensi. Vilevile, katika sentensi 33(a), 33(b), 33(c), 33(d) na 33(d), matumizi yasiyo sahihi ya ngeli yalidhihirisha upatanisho wa kisarufi usio sahihi kati na nomino na kivumishi.

34. (a) *Asubuhi *nime amkanika enda* bafuni.

→ ...*nimeamka nikaenda*...

(b) *Wakati *alipo malizawa imbajiwaka anza* kusifu tena Mungu.

→ ...*alipomaliza waimbaji wakaanza* ...

(c) *Ni mambo ambayo tunafanya kila siku juma pili.

→ ...Jumapili.

(d) *Hali iko je hapo mkoani Mwaro ?

→ ...ikoje... ?

35. (a) *Katikamaisha ya kila siku elimu huwa ni muhimu.

→ *Katika maisha...*

(b) ... *kulingana *namambo* mtu anafanya ...

→ ...*na mambo...*

(c) *Husaidiya watu kwakujenga msingi wa maisha.

→ ...*kwa kujenga...*

(d) ...*mahali pakupotelea viatu hivyo

→ ...*pa kupotelea...*

(e) *Badhala yakutoka nyumbani,...

→ ...*ya kutoka...*

Katika sentensi hizi hapa juu kumetokea makosa ya kisintaksia kutokana na kukatia maneno pasipofaa na kuunganisha maneno visivyo. Katika kazi za kimaandishi, makosa haya huwaletea utata wasomaji na hupotosha ujumbe uliotarajiwa. Katika sentensi 34(a), 34(b), 34(c) na 34(d), baadhi ya maneno yalikatiwa mahali pasipofaa (*nime amka><nimeamka, *nika enda><nikaenda, *alipo maliza><alipomaliza, *waka anza><wakaanza, *wa imbaji><waimbaji, *juma pili><Jumapili, *iko je><ikoje). Uchunguzi wa data ulidhihirisha kuwa wanafunzi kutoka D.R Congo huwa na kawaida ya kukatia maneno pasipofaa, jambo ambalo huwa linadhihirisha ujuzi duni katika maandishi. Pia, imeonekana kuwa vitenzi hukakwa kwa jinsi

ambavyo viambishi tamati na shina la kitenzi hubainika kama mafungu mawili tofauti. Aidha, katika maneno changamani yaundwayo kwa mofu chanagamano (**juma pili*><*Jumapili*, **iko je*><*ikoje*), mofu hizi hutenganishwa kama mafungu mawili tofauti, ambapo kiambishi ngeli hubainishwa na shina katika nomino (**wa imbaji*><*waimbaji*, **ma rafiki*><*marafiki*).

Katika sentensi 35(a), 35(b), 35(c), 35(d) na 35(e) kulitokea uunganishaji wa baadhi ya maneno, hali ambayo ilipotosha miundo ya tungo (**namambo* >< *na mambo*, **kwakujenga* >< *kwa kujenga*, **pakupotelea*>< *pa kupotelea*, **Katikamaisha*>< *Katika maisha*, **yakutoka* >< *ya kutoka*). Mifano hii inadhihirisha uzoefu wa wanafunzi wa Kingwana kuambatanisha maneno yasiyo yenye hadhi sawa kisarufi kama vile kiunganishi na neno jingine (**namambo* >< *na mambo*, **wamaisha*>< *wa maisha*, **pakupotelea*>< *pa kupotelea*, **yakutoka*>< *ya kutoka*), kihusishi na neno la aina nyingine (**Katikamaisha* >< *Katika maisha*, *kwakujenga*>< *kwa kujenga*) au kitenzi kishirikishi na nomino (**ndiyomaana*>< *ndiyo maana*, **simwanafunzi*>< *si mwanafunzi*). Kuunganisha maneno visivyo au kukata maneno pasipofaa kumezisababisha tungo kuharibika kimuundo, na hivyo, maana za tungo zikapotea kwa sababu vipashio vilivyopatikana havitoi maana yoyote katika lugha ya Kiswahili.

4.4.3 Makosa Kutokana na Ufupishaji

Katika utafiti huu, ufupishaji ulitambulika kuwa sababu ya baadhi ya makosa yaliyojitokeza kwa wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vya Burundi. Makosa hayo yalipatikana katika viwango vyote vya lugha

vinavyoshughulikiwa na utafiti huu, yaani fonolojia, mofolojia na sintaksia; na kutokea mara 38 kati ya jumla ya makosa 874, sawa na 4.34%.

4.4.3.1 Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Ufupishaji

Katika matamshi ya wanafunzi wa Kingwana, ilidhihirika makosa ya udondoshaji wa fonimu fulani. Miongoni mwa makosa haya, yalitambulika makosa yanayotokana na uhamishaji wa mifumo zoefu kutoka Kingwana kwenda Kiswahili sanifu. Hata hivyo, imetokea wakati ambapo udondoshaji wa fonimu ulitokana na ufupishaji wa maneno, na sababu hii ilisababisha kiasi cha makosa 9 kati ya jumla ya makosa ya kifonolojia 365, sawa na 2.46%. Sentensi zifuatazo ni mifano ya ufupishaji wa kifonolojia :

36.(a) *Nikaenda *koga* nilimalisa saa 6 na nusu.

→...*kuoga*...

(b) *Kukosa maji ya *koga*, ...

→...*kuoga*...

(c) **Nilimona* mwizi akikataliwa...

→ *Nilimwona*...

(d) *Je, *unamona* yule ?

→ ...*unamwona*...

(e) *Nikaelekeya chuoni kwa mguu *paka*...

→...*mpaka*...

Katika sentensi 36(a), 36(b), 36(c) na 36(d) makosa ya udondoshaji yamedhihirisha ufupishaji wa maneno husika kwa kudondosha irabu ya kiambishi awali kinachotokea mara kabla ya irabu ya mzizi (**koga*><*kuoga*,

Nilimona*><*Nilimwona*). Katika 36(e) ufupishaji wa neno *mpaka* ulijitokeza kutokana na kosa la udondoshaji wa fonimu ya kwanza ya neno hilo (paka*><*mpaka*).

4.4.3.2 Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Ufupishaji

Miongoni mwa makosa ya kimofolojia, yamo yaliyotokana na ufupishaji wa baadhi ya maneno kwa kuondoa vipashio fulani vya kimofolojia. sababu hii ilisababisha utokeaji wa makosa ya kimofolojia 20 kati ya jumla ya makosa ya kimofolojia 214, sawa na 9.34%. Mifano ifuatayo inadhihirisha makosa ya kimofolojia yaliyotokana na ufupishaji.

37. (a) *yule *hajawahielimika*.

→ Yule ambaye *hajawahi* *kuelimika*.

(b) *Inatusaidia *kujua ishi* vizuri na watu katika jamii.

→ Inatusaidia *kujua* *kuishi*...

(c) *Kisha *tukaanzasoma* kiswahili.

→ Kisha *tukaanza* *kusoma* Kiswahili.

38. (a) *Kila siku *nafanya* kazi hii.

→ Kila siku *huwaninafanya* kazi hii.

(b) *... arafu *karudiya* nyumbani.

→ ...halafu *nikarudi* nyumbani.

Katika mifano hapa juu kumejitokeza makosa kutokana na maneno yaliyofupishwa kwa kuondolewa viambishi ambavyo ni vya lazima. Hivyo, katika 37(a), 37(b) na 37(c) mara kitenzi kikuu kiliposhirikiana na kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu kilifupishwa kwa kuondolewa kiambishi awali {-ku-}

(**hajawahielimika*><*hajawahi kuelimika*, **kujuwa ishi*><*kujua kuishi*, **tukaanzasoma*><*tukaanza kusoma*). Vilevile, katika 38(a) na 38(b) vitenzi vilifupishwa kwa kuondolewa kiambishi awali mtenda cha nafsi ya kwanza umoja na hivyo kuleta utata katika mfumo sahihi na usio sahihi (**nafanya*><*ninafanya*, **karudiya*><*nikarudi*).

4.4.3.3 Makosa ya Kisintaksia Kutokana na Ufupishaji

Katika matumizi ya Kiswahili sanifu, wanafunzi wa Kingwana walihusisha ufupishaji wa baadhi ya maneno yaundayo sentensi husika. Makosa kutokana na sababu hiiyalikuwa 9 kati ya jumla ya makosa ya kisintaksia 295, sawa na 3.05%. Ifuatayo ni mifano ya sentensi ambamo ufupishaji ulijitokeza.

39. (a) **Njo* ivo safari yangu imeendeka.

→ Hivyo ndivyo safari yangu ilivyotokea.

(b) *Apo sasa waimbaji *njoowalianza* kuimba.

→ hapo sasa *ndipo* waimbaji *walipoanza* kuimba.

(c) *Hao *ndo* wasema kanisani.

→ Hao *ndio wanaosema* kanisani

(d) ...*na *ndo ilikua* mwanzo wa kanisa.

→... na *ndipo ilipokuwa* mwanzo wa kanisa.

Katika 39(a), 39(b), 39(c) na 39(d) kulitumiwa mfumo wa kiufupi wa Kingwana uhusishao vipashio *ndo* na *njo(o)* katika sentensi. Uchunguzi juu ya vipashio hivi *ndo* na *njo(o)* ulionyesha kuwa matumizi yake husababisha ufupishaji wa vipashio vyenyewe na sentensi pia. Aidha, uchunguzi huo ulionyesha kuwa *ndo* na *njo(o)* hutumika badala ya vipashio vihusishavyo viambishi rejeshi (**njoo*><*ndipo* ...

walipoanza, *Njo><Hivyo ndivyo, *ndo><ndio wanaosema, *ndo><ndipo ilipokuwa).

4.4.4 Makosa Kutokana na Sababu ya Matumizi ya Kanuni Kupita Kiasi

Utumiaji wa kanuni fulani kupita kiasi huwa ni hali ambayo mfumo fulani au kanuni fulani ya lugha huzingatiwa kuliko mifumo na kanuni zingine. Katika uamiliaji wa lugha, matumizi kwa kiasi kikubwa ya kanuni fulani huwa sababu ya makosa kwa wanafunzi au wajifunzaji wowote wa L2. Hali hii hujitokeza pia kwa watoto wanapoamili L1 (James 1998 : 178-179). Sababu hii ya ujitokezaji wamakosa ilisababisha makosa ya kisarufi kwa kiasi cha 71 kwa jumla ya makosa 874, sawa na 8.12%. Makosa yaliyotokana na sababu hii yalijitokeza katika nyanja ya fonolojia na mofolojia.

4.4.4.1 Makosa ya Kifonolojia Kutokana na Matumizi Kupita Kiasi ya Kanuni

Katika matumizi ya Kiswahili sanifu watafitiwa walidhihirisha mkanganyiko kutokana na kanuni za kimatamshi zilizojenga uzoefu akilini mwao na kanuni za kimatamshi mpya walizozipata baadaye darasani. Hivyo, sababu hii ilisababisha utokeaji wa makosa ya kifonolojia kwa kiasi cha 43 kati ya jumla ya makosa ya kifonolojia 365, sawa na 11.78%. Sentensi zifuatazo ni mifano ionyeshayo hali hii :

40.(a) *Safari yangu leo imekua nzuri sana.

→ Leo, safari yangu imekuwa nzuri sana.

(b) *Mwalimu alikuipo akatufundisha hadi saa tisa mchana.

→ Mwalimu alikuwepo; alitufundisha hadi saa tisa mchana.

(c) *Inaongeza akili ya gisi unaeza kujikamata kazini

→ ... jinsi unavyoweza...

41.(a) *Kwa mda mchache ...

→ Kwa *muda* mchache ...

(b) *Lakini sikufika kwa mda.

→ Lakini sikufika kwa *muda*.

(c) *Mda wa kutufafanulia haukuepo.

→ *Muda* wa kutufafanulia *haukuwepo*.

Katika 40(a), 40(b) na 40(c) kumedondoshwa fonimu konsonanti /w/ kutoka katika maneno ambamo kutokea kwa fonimu hii ni kwa lazima. Mtafiti ameelewa kuwa wanafunzi walikanganywa na mfumo mpya kwa wanafunzi unaohusisha mfuatano wa irabu mbili katika neno moja. Hivyo, miundo kama *kukua*, *kuchukua*, *kutembea* na *kukimbia* iliwasababisha wazingatie kwa kiasi kikubwa na kuondoa fonimu /w/ na /y/ popote zinapojitokeza ili kufanikisha mfuatano wa irabu mbili au zaidi katika neno moja. Vilevile, katika sentensi 41(a), 41(b) na 41(c) kulidondoshwa fonimu /u/ kutoka katika neno *muda*. Watafitiwa walikanganywa na kanuni isemayo kuwa umbo la ndani la kiambishi {*mu-*} huwa kwa umbo lake la nje {*m-*} kinaposhirikiana na konsonanti halisi (mf.: *mu+ti= mti*, *mu+kate= mkate*). Hivyo, watafitiwa waliijumuisha kanuni hii kwa maneno kama *muda* ambayo irabu /u/ haidondoshwi.

4.4.4.2 Makosa ya Kimofolojia Kutokana na Matumizi Kupita Kiasi ya Kanuni

Hali ya matumizi ya kanuni za kimofolojia zihusikazo katika Kiswahili sanifu ilitokea kuwa sababu ya baadhi ya makosa ya kimofolojia; na makosa kutokana na chanzo hiki yalitokea kwa kiasi cha 28 kati ya jumla ya makosa ya kimofolojia 214, sawa na 13.08%. Yaliyodhihirika ni pamoja na matumizi ya baadhi ya viambishi vya wakati au hali kama inavyoonekana na mifano ifuatayo:

42. (a) *Padre aliyosimama, *akatupa* baraka kutoka kwa Mungu.
 → Padre aliposimana, *alitupa* baraka kutoka kwa Mungu.
- (b) *Muuzaji mmoja *akanisogelea* akanionesha viatu.
 → Muuzaji mmoja *alinisogelea* ...
- (c) **Nikimalizani*kaenda kuchunga gari la kunileta mjini.
 → *Nilipomalizani*lienda kusubiria gari la kunipeleka mjini.
- (d) **Akimaliza*a*kafikili* kwamba...
 → *Alipomaliza*a*lifikiri* kwamba...
- (e) *...Aisha *huamka* kila siku asubuhi.
 → ... Aisha *aliamka* kila siku asubuhi.

Katika mifano hapo juu kumedhihirika namna matumizi ya kiambishi cha hali ya mfururizo wa matendo {-ka-} kilivyojitokeza kwa kiasi kikubwa tena kisichofaa badala ya {-li-} kwa kuonyesha wakati uliopita (**akatupa*><*alitupa*, **akanisogelea*><*alinisogelea*, **akafikili*><*alifikiri*, **nikaenda*><*nilienda*). Wanafunzi wa Kingwana waliokuwa wamefundishwa hali ya mfururizo wa matendo wamekanganywa kwa kutotambua tofauti iliyopo katika matumizi ya {-ka-} na {-li-}. Upande mwingine, imedhihirika matumizi yasiyofaa ya kiambishi cha hali ya masharti ya wakati ujao {-ki-} kikionyesha wakati tendo lilipolazimika kutokea katika wakati uliopita (**Nikimaliza*><*Nilipomaliza*, **Akimaliza*><*Alipomaliza*, **Nikimaliza*><*nilipomaliza*). Watafitiwa walitumia kimakosa kiambishi {-ki-} kwa kiasi kikubwa badala ya viambashi sahihi ambavyo vingelazimika kutokea. Aidha, matumizi ya kiambishi {hu-} cha hali ya mazoea badala ya kiambishi {-li-} yamedhihirisha uamilifu wanaoupa msemu wa *kila siku*, bila kujali wakati husika.

4.5 Uhusiano baina ya Matokeo na Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya UM iliyoasisiwa na Stephen Pit Corder (1967). Kama ilivyoelezwa awali, nadharia hii inatumika kuchunguza jinsi gani makosa katika lugha yanaweza kushughulikiwa, na hatua zake huwa ni kukusanya data, kutambua, kuainisha, kueleza na kutathmini makosa. Nadharia hii ilimwongoza mtafiti katika kuufanyia kazi utafiti huu kwa kukusanya data kutoka katika kazi zilizofanywa na wanafunzi wa vyuo vikuu vitano vya Burundi vilivyowakilisha vingine, kuzitambua kwa ajili ya kuziainisha, kuzieleza na kuzitathmini ili kuelewa kiasi na sababu za utokeaji wa kila aina ya makosa. Katika mchakato wa makosa hayo, kuligunduliwa utokeaji wa aina mbalimbali za makosa zilizokusanywa katika makundi makubwa matatu ya makosa ya kifonolijia, kimofolojia na Kisintaksia na kimofosintaksia.

Hivyo, nadharia hii ilikuwa mwongozo thabiti uliomwezesha mtafiti kupata majibu ya maswali ya utafiti huu na hivyo kukamilisha malengo yake; na matokeo ya utafiti huu yenyewe yalidhihirisha uwiano wake na nadharia hii.

4.6 Hitimisho

Sura hii imejishughulisha na uchambuzi wa data zilizokusanywa uwandani kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Kingwana wajifunzao Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni. Data hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu za mapitio ya nyaraka, hojaji na ushuhudiaji. Malengo ya utafiti huu yamezingatiwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Nadharia ya UM iliongoza utafiti huu na mikabala ya kimaelezo na kitakwimu ikatumika. Mkabala wa kimaelezo umehusika kwa sababu ya tukio la data za kiuthamano ilhali mkabala wa kitakwimu umehusika

kutokana na data za kiwingidadi katika utafiti huu. Nadharia ya UM iliyotumika katika utafiti huu imesaidia katika kuchanganua data na kutoa majibu kwa maswali ya utafiti huu. Pia, imesaidia katika kulinganisha Kiswahili sanifu na lahaja ya Kingwana.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii ina lengo la kutamatisha kwa kueleza kwa ufupi yaliyofanyika katika utafiti huu unaohusu “Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu kama Lugha ya Kigeni: Uchunguzi kifani wa baadhi ya Vyuo Vikuu vya Burundi”. Sura hii ambayo inanzia kwa utangulizi imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni muhtasari na mapendekezo. Mwishoni, mtafiti ameikamilisha sura hii kwa hitimisho la utafiti kwa ujumla.

5.2 Muhtasari

5.2.1 Muhtasari kwa Ujumla

Utafiti huu umefanyika kwenye vyuo vikuu vitano vinavyofundisha Kiswahili kama kozi muhimu ya lazima katika miaka miwili au mitatu ya shahada ya kwanza : Chuo Kikuu cha Burundi, Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika, Chuo Kikuu cha Mwanga cha Bujumbura, Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu na Chuo Kikuu cha Mwaro. Waliohusishwa ni wanafunzi wa mwaka wa pili na tatu ambao ni wazawa wa mjini Bujumbura na maeneo mbalimbali ya D.R Congo ambapo lahaja ya Kingwana inatumiwa. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa la kutathmini makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya kigeni katika baadhi ya Vyuo Vikuu vya Burundi. Utafiti huu ulifanyika katika sura nne.

Sura ya kwanza kabisa ilihusika na usuri wa mada ya utafiti huu, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti yakiwemo lengo kuu la utafiti na malengo mahususi; maswali ya

utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Sura hiyo iliweka bayana misingi ya utafiti huu.

Sura ya pili ilihusika na kazi tangulizi zilizotungwa na watafiti mbalimbali juu ya mada zinazojenga uhusiano wa karibu na utafiti huu. Maandishi yaliyofafanuliwa yanahusu ujifunzaji wa lugha ya pili, makosa katika lugha na uhusiano wa lugha ya kwanza na lugha ya pili katika muktadha wa ujifunzaji. Baada ya ufafanuzi na ulinganishi wa maandishi haya, pengo la utafiti limebainika. Aidha, sura hiyo iliweka bayana mkabala wa kinadharia ulioongoza utafiti huu. Nadharia ya “Uchanganuzi Makosa” (UM) iliyoasisiwa na Stephen Pit Corder (1967) ili kutambua, kuainisha makosa na kufafanua sababu za utokeaji wake imedhihirika kuwa muhimu zaidi katika utafiti huu, na hivyo ilielezwa katika sura ya pili.

Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Mara baada ya utangulizi mfupi, kulijadiliwa eneo la utafiti na watafitiwa, sampuli lengwa ya watafitiwa na usampulishaji. Mbinu za kukusanyia data zilizotumika katika utafiti huu ni pamoja na mbinu ya mapitio ya nyaraka ambayo kwa muktadha huu ni insha zilizoandikwa na watafitiwa, hojaji na ushuhudiaji. Hojaji ilitumika kwa ajili ya kushadidia matokeo ya njia ya kwanza ya upitiaji wa nyaraka. Aidha, sura hii iliweka bayana mikabala ya uchanganuzi wa data iliyotumika, yaani mkabala wa kimaielezo na mkabala wa kitakwimu. Vilevile, sura hii imeonyesha maadili ya utafiti.

5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Kutokana na data zilizokusanywa na malengo mahususi ya utafiti huu, kulibainika aina za makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa lahaja ya Kingwana watumiapo

Kiswahili sanifu, ujitokezaji wa makosa ya kisarufi katika Kiswahili sanifu na sababu zinazochochea ujitokezaji wa makosa hayo.

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirika kutokana na malengo mahususi ya utafiti huu. Lengo la kwanza lilikuwa kubaini aina za makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu. Uchunguzi huu uliweka bayana makundi makuu matatu ya makosa ambayo ni makosa ya kifonolojia, makosa ya kimofolojia na makosa ya kisintaksia. Makosa ya kifonolojia ni pamoja na udondoshaji wa fonimu, ubadilishanaji wa fonimu na uzalishaji wa fonimu katika mazingira yasiyofaa. Makosa ya kimofolojia ni pamoja na udondoshaji wa viambishi vinavyohitajika, ongezeko la viambishi kimakosa na matumizi ya viambishi kimakosa. Makosa ya kisintaksia ni pamoja na upatanisho usiofaa kati ya nomino na kitenzi au nomino na kivumishi, ugeukaji wa viambishi tegemezi kuwa neno, kukata na kuunganisha maneno visivyoy.

Lengo la pili lilikuwa la kutathmini viwango vya ujitokezaji wa aina mbalimbali za makosa hayo. Uchunguzi ulionyesha kuwa idadi ya jumla ya makosa ilikuwa 874. Imedhihirika kuwa makosa ya kifonolojia yamejitokeza kwa kiasi cha 365 kwa 874, sawa na 41.76%. Upande wa makosa ya kimofolojia, haya yamejitokeza kwa kiasi cha 214 kwa 874, sawa na 24.48% ilhali makosa ya kisintaksia na kimofosintaksia yamejitokeza kwa kiasi cha 295 kwa 874, sawa na 33.75%.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza sababu za utokezaji wa makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa Kingwana katika Kiswahili Sanifu. Uchunguzi ulionyesha kuwa makosa hayo yalitokana na (i) uhamishaji wa lugha,

(ii)ufupishaji, (iii) matumizi kupita kiasi ya kanuni fulani ya lugha na (v) kutozijua kanuni za Kiswahili sanifu. Makosa kutokana na uhamishaji wa lugha yalijitokeza kwa kiasi cha 55.60%. Makosa yaliyotokana na ufupishaji yalidhihirika kwa kiasi cha 4.34%. Makosa kutokana na matumizi kupita kiasi ya kanuni fulani ya lugha yalijitokeza kwa kiasi cha 8.12% ilihali makosa kutokana na kutozijua kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu yalijitokeza kwa kiasi cha 31.92%.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu uliochunguza makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu kwenye vyuo vikuu vya Burundi ulibainisha aina za makosayanayojitokeza katika Kiswahili sanifu kutokana na athari za Kingwana. Makosa yaliyobainika yalikusanyika katika makundi makubwa matatu ya makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Utafiti huu pia ulionyesha kiasi cha ujitokezaji wa kila aina ya makosa, na sababu za makosa hayo kutokea.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameweka bayana makosa mbalimbali ya wanafunzi wazawa wa Kingwana, utamalaki wake na vyanzo vyake. Imedhihirika kuwa wanafunzi wa Kingwana hupata shida zinazohusiana na kutotambua tofauti kati ya mifumo sahihi ya Kiswahili sanifu na ile ya Kingwana ambayo tayari ilijenga uzoefu akilini mwao. Hivyo, inawabidi walimu kutia mkazo katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kubainisha mifumo ya kilahaja inayoathiri Kiswahili sanifu. Kuhusiana na hilo, mazoezi ya kuandika na kuzungumza wakijaribu kuyasahihisha makosa wanayoyafanya yangewafaa sana wanafunzi. Aidha, inawabidi walimu kuimarisha uhusiano kati ya masomo yaliyotangulia na yaliyofuata kwa kuwasiliana wao kwa

wao ili kujua ni kipi kilifundishwa na kipi kitafuata. Pili, ingawa serikali ya Burundi ililazimisha ufundishaji wa Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu, inahitajika sera ambayo ingeongoza uandaji wa mitaala inayohusisha mahitaji yote katika ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Aidha, inawabidi viongozi wa vyuo kuajiri walimu wenye uwezo kabisa wa kufundisha vyuo vikuu na kufuatilia kama masomo yanatolewa kama programu zilivyopangwa. Wanafunzi nao, wanatakiwa kufanya bidii kwa kusoma vitabu vya Kiswahili na kufanya mazoezi ya mazungumzo wakijaribu kujiimarisha wenyewe katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Upande mwingine, utafiti huu haukuweza kuchunguza makosa yote yanayofanywa na wanafunzi wa Kingwana wanapotumia Kiswahili sanifu. Umejikita tu katika uchunguzi wa makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Hivyo, tafiti fuatishi zinahitajika. Kwanza, utafiti juu ya makosa ya kisemantiki ungeonyesha makosa ya kimaana yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu kutokana na athari za lahaja ya Kingwana. Pili, utafiti juu ya launi mbalimbali za Kingwana ungedhihirisha utofauti wa mifumo ya kisarufi ndani ya lahaja ileile moja ya Kingwana. Mwisho, katika nchi za Afrika ya kati, aghalabu Burundi, Rwanda na D.R Congo, inabidi vyuo vifundishe somo la lahaja za Kiswahili. Ingekuwa fursa ya kutoa mwanga juu ya matumizi ya msamiati mpya na mifumo mipya inayotokana na kuenea kwa Kiswahili. Aidha, ufundishaji wa somo la lahaja ungechangia katika kuzuia mchanganyiko wa mifumo mbalimbali ya lahaja mbalimbali za Kiswahili inayotumiwa na Waswahili kwa kuiingiza katika Kiswahili sanifu bila wao kutambua hadhi yake.

MAREJELEO

- Ame, P.M. (2017). *Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika katika Shule za Tumbatu Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Aruba, B.K. & al. (2017). Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili ya Wanafunzi wa Shule za Upili Nchini Kenya. *Journal of Arts and Education*, Serial Publishers.
- Atkinson, D. (1987). The mother tongue in the classroom: a neglected resource? *ELT Journal*, 41(4): 241-247, <http://eltj.oxfordjournals.org/content/41/4/241.full.pdf>
- Auerbach, E. (1993). Reexamining English Only in the ESL Classroom. *TESOL Quarterly*, 27(1): 1-18, http://www.ncela.gwu.edu/files/rcd/BE019020/Reexamining_English_Only.pdf.
- Berwick, R. C. & al. (2011). Songs to Syntax: The Linguistics Birdsongs. *Trends in Cognitive Sciences*; Vol. 15. No.3. Amsterdam: Elsevier-Cell Press.
- Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar Es Salam: Tanzania Publishing House.
- Buliba, A., & al. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Brown, D.H. (2000). *Principles of Language Learning and Teaching*. (4th ed.). London: Longman.
- Casco, J. A. S. (2007). *Standard Swahili: Is It Still a Prevailing Category?* México: El Colegio de México, Centre for Asian and African studies.
- Chacha, L.M., & Ngugi, P. (2004). *Sociolinguistics*. Nairobi: Kenyatta University.

- Chen, L. L. (2006). The effect of L1 and CAI on grammar learning: An Error Analysis of Taiwanese beginning EFL learners' English essays. *Asian EFL Journal*, 9(2), 1-19.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. The Hague: Mouton.
- Cioroianu, C.E.B. (2015). Analysis of Frequent Errors while Learning Romanian as a Foreign Language. *Annals of the University of Craiova*. Craiova: The University of Craiova.
- Cook, V. (1999). *Linguistics and Second language Acquisition*. London: The Macmillan Press LTD.
- Corder, S.P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.
- (1971). Idiosyncratic Dialects and Error Analysis. In Richard J. (Ed) *Error Analysis: Perspective in Second Language Acquisition*. London: Longman.
- (1973). *Introducing applied linguistics*. Middlesex: Penguin.
- (1974). Error Analysis. In Allen, J. P. B. & Corder, S. P. (Eds.), *Techniques in Applied Linguistics*. London: Oxford University Press.
- (1981). *Error Analysis and Interlanguage*. London: Oxford University Press.
- Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman.
- Darus, S. (2009). Error analysis of the written English essays of secondary school students in Malaysia: A case study. *Eur. J. Soc. Sci.*, 8(3), 483-495.
- Dubois, J. & al. (2002). *Dictionnaire de linguistique*. (2^e éd). Paris: Larousse-Bordas.

- Dulay, C. & Burt, K. (1974). Error and strategies in child second language acquisition. *TESOL Quarterly*, 8, 129-138.
- Ellis, R. (1995). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.
- Erdoğan, V. (2005). Contribution of Error Analysis to Foreign Language Errors. *Theory and Practice in Language Studies*, Vol. 2, No. 8, Shiraz: Islamic Azad University.
- Fisiak, J. (1981). *Contrastive Linguistics and the Language Teacher*. Oxford: Pergamon Press.
- Forman, R. (2005). *Teaching EFL in Thailand: A bilingual study*, Doctoral Dissertation. (unpublished) University of Technology, <http://eprints.lib.uts.edu.au/dspace/bitstream/handle/2100/552/02whole.pdf>; jsessionid=1BF811FDD60F6A53318CE7201B340945?sequence=2FrancisGroup.
- Gardner, M. P. (1985). Mood States and Consumer Behavior: A Critical Review. *Journal of Consumer Research*. Vol. 12, No.3. London: Oxford University Press.
- Habwe, J., & Karanja, P. (2012). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Harbord, J. (1992). The Use of the Mother Tongue in the Classroom. *ELT Journal*, 46(4), 350-355.
- Harmer, J. (1998). *The Practice of English Language Teaching*. Harlow: Pearson Education.
